**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |

| | |
|---|---|
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 32. Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 43.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 44.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 45.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 49.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

| | |
|---|---|
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Tano – Tarehe 16 Oktoba, 2012**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kama ilivyo kawaida Baraza letu huwa linapata bahati ya kutembelewa na wageni mbali mbali kutoka nchi mbalimbali Afrika na nje ya Afrika. Kwa hivyo, leo hii tunao wageni ambao wametutembelea katika Baraza letu na wageni hao ni Wabunge kutoka Chama cha *ANC* ya Bunge la *Free State* nchini Afrika ya Kusini. Idadi yao ni watano ambao ni kama ifuatavyo:-

1. Hon. Phel Paekies - Mnadhimu wa Serikali katika Bunge (Kiongozi wa Msafara)
2. Hon. Cornelius Van rooien - Naibu Mnadhimu
3. Sindiswa Magwandana - Whip Constituency
4. Hon. Aupa Khoabane - ANC Free State Spokesperson and Head of Political Education
5. Hon. Maroele Seruoe - ANC CAUCUS Leader.

*Honourable could you please stand up to salute to the members? You are most welcome.*

Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu wa leo wapo hapa tangu siku ya Jumamosi wametembea maeneo mbali mbali wamekuwa pamoja na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed jana na mimi jioni hiyo jana nilikuwa na mazungumzo nao, leo wamependa kuja kuona namna gani tunafanya shughuli zetu katika shughuli zetu za kawaida. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe *and our guests you are most welcome to Zanzíbar.*

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

**Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya Mwaka 2005 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu naomba kwa ruhusa yako kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzíbar kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 35**

**Tatizo la Echo katika Ukumbi wa Baraza**

**Mhe. Salim Abadía Hamad** – Aliuliza:-

Hakuna kitu muhimu zaidi kama kusikizana vilivyo katika ukumbi huu wa Baraza wakati wa vikao, lakini bado tunasumbuka sana kutokana na "*ECHO*" na mambo mengine ya kiufundi.

(a) Je, tatizo hili linasababishwa na nini.
(b) Ni hatua gani zilizochukuliwa kuondosha tatizo hili

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niwapongeze Wajumbe wenzetu wa Baraza hili tukufu walioteuliwa na Rais jana katika nafasi mbali mbali tukianzia na Mhe. Shawana Bukheti Hassan, Mhe. Mtumwa Kheir na Mhe. Mohamed Said Mohamed. Nawatakia heri na mafanikio katika kazi zao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inakiri kuwepo kwa tatizo la kutosikilizana vizuri katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi. Tatizo hilo linasababishwa na kutokuweko vifaa maalum vya sauti wakati wa ujenzi wa ukumbi huu. Vifaa hivyo vya Sauri huwekwa katika kuta pamoja na *tiles* zinazowekwa katika sakafu. Mhe. Spika, kukosekana kwa vifaa hivyo wakati wa ujenzi kumesababisha tatizo la kutokusikilizana vizuri katika ukumbi wetu. Hata hivyo, ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Idara ya Ujenzi inaangalia uwezekano wa kuviweka vifaa hivyo hivi sasa ili kuondoa tatizo hilo.

(b) Mhe. Spika, ofisi yangu kupitia Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliwahi kuchukua hatua za kuondosha tatizo hilo. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuongeza vipaza sauti ndani ya ukumbi kama tulivyoshauriwa na wataalamu ili kuongeza uwezo wa kusikilizana ndani ya ukumbi huu. Baada ya hatua hiyo tatizo hilo limepungua ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwanzo lakini jitihada zaidi zitachukuliwa kuondosha tatizo hili ili tuweze kusikilizana vizuri katika ukumbi wetu huu.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, kwanza nitoe shukurani za jibu zuri na juhudi Mhe. Waziri kwa kupitia wizara yake aliyoichukua katika kuweka hii hali iwe nzuri. Mhe. Spika, hili ni jengo la Baraza la Wawakilishi na hapa tunakutana kwa mambo na kusikizana ndio jambo muhimu kweli kweli na jengo hili ni la kudumu litaendelea milele *Inshaallah*. Katika hali ya jengo hili lilivyo kwa sababu ya *Echo*, hatusikizani, hatufahamiani vizuri mpaka inafika wakati mtu anapopewa maelezo ya masuala yake na kadhalika hubidi msikilizaji aweke sikio kwenye kitako cha *mike* ili uweze kusikia ufundi ambao sijui ulipatikana wapi. Hivyo, hakuna uwezekano wa kufanya *re-construction* katika huu ujenzi tukaona kuwa kumewekwa kwa makusudi vitu ambavyo vitakuwa vinakunywa ile *echo* ili tuweze kusikilizana vizuri zaidi ya juhudi hizo za hapa na pale ambazo zinachukuliwa na hazijaleta ufanisi wa kutosha.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba nia na madhumuni ni kuondosha tatizo hili na hivi sasa wizara yangu kupitia Baraza la Wawakilishi linashirikiana na wataalamu kuona tatizo hili linaondoka. Ni nia yetu katika mwaka huu wa fedha kuliondoa tatizo hili, tutafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Ni kweli sote hapa haturidhiki na hali hii sisi tulioko huku mbele tuliopata fursa ya kujibu maswali mbali mbali ya waheshimiwa Wajumbe inakuwa vigumu pia kuwasikia wakati wanapotuuliza, halikadhalika na sisi kutusikia wakati tunapojibu. Kwa kweli hilo ni tatizo gumu na linafaa liondoshwe. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane tuhakikishe kwamba tatizo hili linaondoka, nataka niwahakikishie Wajumbe kwamba nia na dhamira ni kuondoa tatizo hili.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya usalama na uzima. Kwa kuwa Mhe. Spika, suala hili ni la siku nyingi sana je, haoni Mhe. Waziri kwamba hiki ni chombo kikubwa na kuhakikisha kwamba hao wataalamu wanatafutwa kwa hali na mali ili kuweza kusawazisha suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, nakubaliana naye kuwa muda ni mrefu, nakubaliana naye kuwa hiki ni chombo kikubwa, nakubaliana naye kwamba wataalamu tuwatafute kwa hali na mali tuhakikishe kwamba Baraza letu linasikilizana vizuri na hilo ndilo litakalofanya kuliongezea hadhi na heshima Baraza letu.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu na kwa kuwa linatia aibu Baraza letu kwa sababu inabidi mawaziri wasikilize kwa kuinamisha masikio na warudie tena mara ya Pili na hiyo inakuwa si busara nzuri kwa chombo kama hiki, na kwa kuwa kuna baadhi ya Mabaraza wanakuwa na *mic* za kusikiliza kwenye masikio,

*phone*. Je, haoni Mhe. Waziri wakati tunasubiri tukatafutiwa *phone* za kusikilizia ili tupate habari vizuri kuliko kukaa hivi ikawa hatusikii watu tunarudia jambo mara kumi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naelewa kwa nini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanakuwa na malalamiko haya ya hali hii, kwa sababu yanatukuta sote na sote tusingependelea kuona hali hii. Ni kweli ni usumbufu kwa Waheshimiwa kuinama kusikiliza katika spika wakati inakuwa ni vigumu sana. Mashauri mbali mbali yaliyotolewa na Waheshimiwa tutayafanyia kazi, lakini cha msingi ni hili la kuondoa hili tatizo. Kama nilivyosema tunao wataalamu wanatushauri na wanatuelekeza njia ambazo itatokea uwezekano wa kuondoa tatizo hili. Naomba Waheshimiwa mvute subira na *Inshaallah* pengine kikao kijacho hali ikawa imetengenea vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa.

**Nam. 37**

**Kuharibika kwa Mashine ya *CT Scan***

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:**

Kwanza kabisa Mhe. Spika, nami naomba uniruhusu kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzíbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na vile vile Makamo Mwenyekiti mtarajiwa wa CCM kwa uteuzi alioufanya hapo jana, na ni watakie kheri kila aliyepewa fupa hilo niwaombee dua waendelee na kazi vizuri kupata kwao ndio kupata kwetu. Kabla ya kuliondoa swali langu nambari 37 kwanza nataka niipongeze Wizara ya Afya kwa kuwa makini kwa suala hili na nimpongeze kwa dhati kabisa waziri asiyeyumba Mhe. Waziri wa Afya kwa uzalendo wake aliouonesha muda mfupi tu kwa wizara hii. Kwa hivyo Mhe. Spika, swali hili naomba liondolewe na nawatangazia Wajumbe pamoja na wananchi wanaotusikiliza kuwa hivi sasa *CT Scan* tayari imeshaanza kazi baada ya miezi minne mpaka mitano. Nashukuru Mhe. Spika naomba kuondoa swali hili.

*(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali ameliondoa)*

**Mhe. Spika:** Swali limeondolewa tunakushukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Naibu Waziri wa Afya unaweza kuendelea na ile kazi uliyoniambia.

**Nam. 53**

**Matumizi ya Vitambulisho katika Upatikanaji wa *Ticket* za Kusafiria**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Mamlaka ya Usafiri nchi kavu na Baharini Tanzania Bara wameweka utaratibu wa abiria kuuziwa tiketi baada ya kuonesha kitambulisho, lakini Zanzibar abiria wamekuwa wakisafiri bila ya utaratibu huo.

(a) Kwanini serikali imeshindwa hadi sasa kutekeleza ahadi yake ya kutumia utaratibu kama huo.

(b) Kwa kuzingatia umuhimu wa kitambulisho katika kumtambua mtu yanapotokea majanga kama ya ajali. Je, serikali ina mpango gani wa kusimamia ahadi yake ya watu kukata tiketi kwa kutumia vitambulisho.

(c) Baada ya serikali kutangaza kupiga marufuku uuzaji wa tiketi mitaani. Je, mpango huo umefanikiwa kwa kiwango gani katika utekelezaji wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye vifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali haijashindwa kutekeleza ahadi yake ya kutumia utaratibu wa abiria kuuziwa tiketi baada ya kuonesha kitambulisho. Utaratibu huo upo na unaendelea na hivi sasa ndio unaotumika.

(b) Kwa kuzingatia umuhimu wa kitambulisho katika kumtambua mtu yanapotokea majanga kama ajali na kusimamia ahadi zake, serikali imefanya kikao na wamiliki wote wa meli zinazosafirisha abiria, kikao hicho kwa mara ya kwanza kimefanyika tarehe 13/06/2009. Utaratibu wa kuuza tiketi kwa kutumia vitambulisho utaratibu huo umekubaliwa kati ya wamiliki wa vyombo pamoja na mamlaka husika. Mamlaka ya Usafiri Baharini mara kwa mata imekuwa ikitoa matangazo kupitia vyombo vya habari kuwataka wananchi wanaosafiri kwa kutumia vyombo vya baharini kuonesha vitambulisho vyao wanapokwenda kununua tiketi.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kuviagiza na kuvihimiza vyombo vyote vinavyohusika kusimamia na kutekeleza kwa dhati kabisa vya kuona kwamba serikali inawalazimisha sasa hivi wananchi wote wanaosafiri lazima wende wakakate tiketi baada ya kuonesha vitambulisho.

(c) Mhe. Spika, baada ya serikali kutangaza kupiga marufuku uuzaji wa tiketi mtaani, mpango huo umefanikiwa kwa kiwango kikubwa, hivi sasa Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa kushirikiana na Makampuni ya Meli zimeanza kuwasajili mawakala wa kuuza tiketi pamoja na kuwa na ofisi zenye kuridhisha. Hata hivyo, bado wapo baadhi ya watu wachache wanaoendelea kufanya biashara hizo kinyume na utaratibu uliowekezwa na serikali.

Mhe. Spika, naomba nirejee tena kutoa wito kwa taasisi mbali mbali za serikali ikiwemo Jeshi la Polisi, Baraza la Manispaa na kadhalika kuendelea na utaratibu ule ambao serikali umekubaliana nao wa kukata tiketi katika mazingira yaliyoridhiwa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, watu hupiga kelele sana hapa Barazani baadhi ya Wajumbe wako, pamekuwa na sheria nyingi lakini utekelezaji wake haupo. Nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa lugha nyepesi sana na laini ni sababu gani zilizopelekea hadi sasa kutokutungwa kanuni za kusimamia sheria ya usafiri baharini. Kwa mamlaka yenyewe tangu kuanzishwa karibu miaka mitano hivi sasa.

Pili, kukosekana kwa kanuni hizo serikali haioni ndio chanzo cha sheria kutokufuatwa kinachopelekea hata wauzaji tiketi kuuza njiani.

Tatu, kwa kuwa Sekta ya Usafiri Baharini ni muhimu lini Mamlaka ya Usafiri Baharini itaondoa tatizo la kukosekana kwa mtandao wa mawasiliano redio ili kupunguza ubovu wa meli wakati mwengine hata kuweka baadhi ya watendaji Kisiwani Pemba kabla ya kuondoka meli ikakaguliwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar katika mwaka 2011 ilifanya maamuzi ya kuanzisha Mamlaka hii ya *Zanzíbar Maritime Authority*. Sheria zilikuwepo lakini Mamlaka imeundwa rasmi mwaka 2011. Katika utekelezaji wa kazi zake mamlaka hii ina upungufu wa kanuni nyingi na twabaan kanuni hizo hazitopungua 40.

Katika utekelezaji wa shughuli hizi mamlaka imeanza utaratibu wa kwanza kutunga kanuni na naamini kwamba changamoto iliyopo itapatiwa ufumbuzi muda mfupi. Kanuni hizo zote haziwezi kutungwa kwa mara moja wala kwa siku moja, lazima tuangalie utekelezaji wake unahitaji vitu vingi, kuna kanuni ambazo zinahitaji wataalamu, kuna kanuni ambazo zinahitaji ushauri, lakini kuna kanuni ambazo zinahitaji na fedha katika utungaji wake. Sasa Mhe. Spika, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba dhamira ya serikali ni kuona kwamba sheria ile inatekelezwa vizuri na ili sheria itekelezwe vizuri inahitaji nyezo zikiwemo hizo kanuni. Kwa msingi huo namuomba Mhe. Mwakilishi ajenge imani na aendelee kuiamini serikali katika hili tutalitekeleza.

Mhe. Spika, katika mnasaba huu wa kanuni nakubaliana naye kwamba kukosekana kwa kanuni kutaviza utekelezaji na ufanisi uliokusudiwa wa uanzishwaji wa Mamlaka hii. Napenda kumuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba, serikali tumeliona hilo na tunaahidi kwamba tutatunga kanuni hizo moja baada ya nyengine ili kukamilisha mapungufu yanayojitokeza.

Suala la tatu Mhe. Spika, katika utaratibu wetu hivi sasa tayari vyombo vyote vya abiria vinavyofanya safari za kusafirisha abiria tumeshatoa maelekezo yao kwamba lazima chombo kiwe kina vifaa ambavyo vitaweza kuwatambua wapi walipo ili iwe rahisi yanapotokea majanga kuweza kutoa taarifa katika vyombo husika.

Lakini la pili naomba tena tuwaombe manahodha na wafanyakazi katika mashirika na vyombo vyetu vya kusafirisha abiria wawe makini katika kusimamia na kutekeleza sheria za kimataifa zinazohusiana na masuala ya usafiri ikiwa ni pamoja na kuwa na uthubutu na umakini wa kutoa taarifa katika vyombo husika pale wanapopatwa na majanga na wasiwe na tabia ya kunyamaza kimya bila ya kutoa taarifa katika maeneo husika ili kuweza kuvijuvywa vyombo vinavyohusika.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lakini kwanza natanguliza pongezi za dhati kwako wewe Mhe. Spika, kwa namna unavyojua na kutuelekeza kuhusu hivi vitambulisho. Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba kuuliza swali. Kwanza napenda kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa jibu lake kuwa wamepitisha kwa pamoja kuwa huwezi kusafiri mpaka uwe na kitambulisho na kitambulisho ninachokielewa mimi kama ndicho ni kile cha Mzanzibari Mkaazi na tunajua kuna watu wengi hivi sasa wenye umri hata kuanzia miaka 40 na kupindukia hawana vitambulisho hivi na kuna wengine wameshafikia wakati wa kuchukua vitambulisho lakini mpaka leo kuna ugumu sana wa kupewa, hii ni sawa sawa na kusema kwamba wamekatiwa haki zao kama ni Wazanzibari. Je, wizara yake imefanya ushauri gani na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuona kuwa tatizo hili limeondoka hasa masheha ikiwa ndio vikwazo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, wakati serikali chini ya Mamlaka ya *ZMA* inafanya kikao husika cha kuwataka wasafiri wanapokwenda kukata tiketi kuwa na vitambulisho jambo hili lilichukua muda mrefu katika kujadili. La msingi tulilokubaliana ni kwamba kitambulisho hatutohusisha kitambulisho kimoja, vitambulivyo ambavyo tumekubaliana navyo kikiwemo hicho cha Mzanzibari Mkaazi, Leseni ya Udereva, Pasi ya Kusafiria, Barua ya Sheha, hivi vyote kwa ujumla vitaainisha kwamba wewe *particular* zako ulizoziainisha katika kitambulisho hicho zinatosha kukuwezesha wewe kupewa tiketi. Kwa hivyo, kama kuna matatizo katika upatikanaji wa vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi naamini kwamba Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amelisikia hilo na atakuwa na majibu mazuri na naamini katika sheria hii tunayoibadilisha basi hayo matatizo yaliyopo yatapatiwa ufumbuzi.

**Nam. 5**

**Kupunguzwa Gharama za Kuunga Umeme**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla yakujibiwa swali langu nambari 5 naomba niwapongeze wale wateule watatu wa Mhe. Rais aliowateua Jana. Kwa kweli uteuzi wake umesibu sasa tunachokisubiri ni sisi Wawakilishi utumishi ulio makini na wenye kutukuka mno kwa hawa. Baada ya maelezo hayo naomba swali langu sasa lijibiwe.
Kutokana na utandawazi, suala la upatikanaji wa umeme kwa kila mwananchi ni jambo la msingi mno. Na kwa kuwa gharama za kuunga umeme ni kubwa mno kiasi ambacho wananchi wengi wanashindwa kumudu, ingawa wanao uwezi wa kulipa matumizi yao ya *units* za kila mwenzi.

Je, ni lini serikali itawapunguzia wananchi hawa gharama hizo ili wapate huduma hii na hatimae waende sambamba na utandawazi.

**Mhe. Naibu Waziri wa ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye kama hivi ufuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika linaendelea na mpango wake wa kuwaungia umeme wananchi kwa njia ya mkopo. Shirika pia linaendelea kujenga *main line* za umeme ulio mbali kwa wale wananchi wanaounda vikundi katika vijiji kwa gharama za shirika na wananchi wao wanapaswa kugharamia gharama ndogo tu, pamoja na gharama za kuunganishiwa umeme ndani ya majumba yao.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu ambayo hayakuniridhisha ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika jimbo langu sehemu ya Mchangani iliyoko Vitongoji pale,

wametakiwa walipe shilingi milioni mbili masafa ya nguzo moja tu, jamba ambalo hawana uwezo nalo na kwa kuwa shirika hili ni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar sasa kwa kuwa hawa watu hawawezi gharama kubwa kiasi hicho yeye anasema anawakopesha, lakini kuwakopesha lazima baadae walipe. Je, si ingekuwa vyema kuwapunguzia gharama kusudi wakaweza tulipa ili serikali ikanufaika na wananchi wakanufaika.

Pili, kuendelea kuwanyima umeme hawa kwa kushindwa tulipa gharama je, si kwenda kinyume na ile dhamira halisi ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kupeleka huduma kwa wananchi wake bila ya matatizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, lengo la wizara yangu kupitia Shirika la Umeme ni kuwasambazia wananchi huduma hii ya umeme katika vijiji vyote na kama kuna kijiji au kuna mwananchi ambaye kalipishwa gharama ya nyuzo moja shilingi milioni mbili basi niseme hilo ni koseo. Mimi niko tayari kulifuatilia suala hili ili tulipatie ufumbuzi na ningeomba sana nishirikiane na Mhe. Mwakilishi kwa kulifuatilia suala hili.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Nashukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi hii katika Baraza lako tukufu. Kwanza nampongeza Mhe. Rais kwa uteuzi wake na wale wote waliochaguliwa nawaombea kazi njema. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri kama tunavyojua nishati ya umeme ni muhimu sana katika maisha yetu ya binadamu. Katika Jimbo la Bububu baadhi ya maeneo umeme wake ni mdogo sana hasa katika maeneo ya Kiboko yao, maana yake ninasema hivi hata ile mashine ya kupandishia maji basi inakuwa haiwaki muda wa usiku na nafikiria *transformer* iliyokuwepo pale imezidiwa kwa ongezeko la watu, nyumba zimekuwa nyingi. Kwa hivyo ninahisi *transformer* ile imekuwa ni ndogo, ibadilishwe *transformer* nyengine.

Lakini hapa ninasema kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Bububu nitachangia shilingi milioni tano kwa kununua *transformer* mpya kuisaidia wizara yako ili wananchi ….

**Mhe. Spika:** Swali mheshimiwa baada ya maelezo hayo.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu**: Ili wananchi wa pale wa eneo la Kiboko yao kununuliwa *transformer* nyengine lakini hapo hapo naomba Mhe. Naibu Waziri kama ni Mwakilishi nitachangia shilingi milioni mbili, swali langu wizara isaidie ili kununua *transformer* nyengine ili iwawekee pale wananchi wale wafaidike na umeme uliokuwa mkubwa na mzuri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikiri kwamba maeneo ya Bububu na maeneo mengineyo mengi tu ya Zanzibar kwamba kuna baadhi ya wakati unapatikana umeme mdogo.

Lakini hili niseme kwamba halisababishwi na *transformer* isipokuwa hili linasababishwa na *line* ambayo iliyokuwepo baharini kwa hivi sasa tunayoitumia ambayo ina uwezo wa *megawatts* 45 au 40 ambazo hazitoshelezi kwa Zanzibar.

Lakini nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya muda mdogo tunategemea sana na baada ya kutandika *line* mpya ya umeme, basi tatizo hili litaondoka kwa Zanzibar nzima na si kwa eneo la Bububu tu. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Mwakilishi astahamili juu ya tatizo hili na iwapo itakapofikia kipindi cha kati kati ya mwezi wa Disemba basi nimthibitishie kwamba tatizo hili litaondoka kwa Zanzibar nzima.

**Mhe. Spika**: Mhe. Waziri majibu ya nyongeza.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea jibu moja la nyongeza ambalo mheshimiwa pia amelizungumzia hapa, nalo ni suala la mchango wake wa shilingi milioni tano.

Mhe. Spika, tunakubaliana na mchango huo na inshaallah itasaidia katika kuboresha huduma ya umeme katika jimbo lake la Bububu na ninawaomba Waheshimiwa wengine wafuate *spirit* hiyo, kwa sababu sera yetu Mhe. Spika, ni kujenga pamoja na kujitolea kwa hali na mali.

Kwa hivyo Waheshimiwa nao wajitolee katika suala la kuhakikisha wanaboresha huduma hii inapatikana kwa wananchi wetu. Ninamshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa mchango wake huo. Ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme hivi karibuni liliwataka baadhi ya watu wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuleta nambari zao ili kufungiwa umeme wa TUKUZA, lakini hadi hii leo kuna baadhi ya watu bado hawajafungiwa umeme huo.

Jee, kuna sababu gani ambazo suala hili bado halijatendeka. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli Shirika la Umeme limewataka Wawakilishi wote kutoa nambari zao za akaunti za umeme, yaani kwa kuwafungia mita za TUKUZA ili kuwaondoshea usumbufu wa kwenda kulipa au kukatia umeme na wafanyakazi wetu wa shirika.

Kwa hivyo shirika langu lipo katika jitihada na linajipanga vizuri kwa ajili ya kuwamalizia, wengine ni kweli tumeshawafungia lakini bado tunaendelea na juhudi hizo za kuwafungia wale ambao waliobakia. Hivyo ningemuomba Mhe. Mwakilishi astahamili bado shirika lina malengo hayo na tutahakikisha kwamba tunalitekeleza hilo.

Lengo la shirika langu ni kuwafungia wananchi wote mita za TUKUZA na kubadilisha mfumo huu tuliokuwa nao hivi sasa. Namuomba astahamili hilo lipo njiani. Ahsante sana.

**Nam. 59**

**Ajira kwa Wageni katika Sekta ya Utalii Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** – Aliuliza:

Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikiimarisha sekta ya utalii kwa malengo ya kuinua uchumi na kuongeza kipato na ajira kwa wananchi wake lakini kumekuwepo na malalamiko ya nafasi nyingi za kazi kunufaisha watu kutoka nje ya Zanzibar.

a) Jee, ni Wazanzibari wangapi wameajiriwa katika sekta ya utalii Zanzibar
b) Pamoja na kuwa Tanzania ni taifa moja Watanzania Bara wangapi wameajiriwa katika sekta hiyo Zanzibar.
c) Jee, ni Wakenya, Waganda na Waafrika Kusini wangapi ambao pia wamenufaika na ajira katika sekta ya utalii Zanzibar

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo** – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na ZIPA kwa kushirikiana na BOT, Afisi ya Mtakwimu Mkuu jumla ya watu 10,500 wameajiriwa moja kwa moja na sekta ya utalii ambayo ni asilimia 87 ya wawekezaji wote hapa Zanzibar.

a) Mhe. Spika, Wazanzibari walioajiriwa ni 10,110 sawa na asilimia 67.4.
b) Watanzania Bara walioajiriwa katika sekta hiyo ya utalii ni 3,990 sawa na asilimia 26.6.
c) Wageni wa nchi nyengine walioajiriwa ni watu 900 sawa na asilimia 9.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa vile leo tumepata wageni kutoka South Africa ambao wamekuja hapa kututembelea. Jee, ni Wa - South Africa wangapi ambao wapo Zanzibar wanafanya kazi ya utalii.

Mhe. Spika: Watu wenyewe Waheshimiwa Wabunge hivi sasa wameshaondoka lakini hata hivyo Mhe. Waziri majibu.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumjibu Mhe. Nassor Salum Ali swali lake la nyongeza kwamba Wa-South Africa wangapi, kwa kweli mheshimiwa takwimu tuliyoikusanya na tukaipata ni kwamba kwa ujumla ukiachia mbali Wazanzibari na Watanzania Bara, kwa ujumla wageni wengine ni 600 ambao ni watu 900.

Kwa hivyo akitaka *specific* kwa watu wa Afrika ya Kusini basi atuachie tuwasiliane na Idara ya Kazi tutampatia kwa maandishi.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona kwa kuwa nimevaa miwani.

Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri nina maswali mawili (a) na (b).

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametupa takwimu ambazo Wazanzibari asilimia 10 na Bara asilimia 3. Jee, Mhe. Waziri hiyo umefanya uhakiki wa usahihi kuwa ni kweli asilimia hiyo.

Lakini pili Mhe. Spika, utakubaliana na mimi kuwa hiyo takwimu yako sio ya kweli.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimjibu Mhe. Mshimba ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Kitope na ambapo kuna shughuli nyingi za kitalii kwamba sisi katika wizara tumechukua takwimu kwa mujibu wa utafiti uliofanywa. ZIPA, BOT na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali tunawaamini na ndio maeneo ambayo wamebobea katika ukusanyaji wa takwimu na kuzitumia.

Sasa kama yeye ana wasi wasi na takwimu hizi basi wacha nichukue nikafanye utafiti wa kina lakini labda tushirikiane mimi na yeye twende tukachambue takwimu hizi, lakini sisi kama wizara tunategemea Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kutupatia data ambazo zinatumika katika mambo mbali mbali ya nchi yetu.

Kwa hivyo kuwa na wasi wasi si jambo baya, hivyo labda tushirikiane mimi na yeye tukafanye uchambuzi wa ziada.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Kwa vile tuna wasi wasi mwingi wa kuwa Wazanzibari sio katika mahoteli. Jee, amejiandaaje kutoa vipande yaani beji kuvaa katika mahoteli kujua kila mtu nchi anayotoka katika hoteli ile.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nashukuru na naomba nimjibu Mhe. Mussa swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo kwamba wazo lake tunalichukua, tutashirikiana Wizara ya Kazi pamoja na wenye hoteli, ikiwa tunaliona ni mnasaba basi tutalifanyia kazi.

**Nam. 57**

**Kuku Kutoka Nje ya Nchi**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** – Aliuliza:

Kumekuwepo na wimbi kubwa la nyma ya kuku kutoka nje ya nchi kuingizwa ktika soko la Zanzibar na kuathiri wafugaji wa ndani.

a) Jee, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wafugaji hao wa ndani ya nchi.
b) Kwa kuwa maradhi ya mifugo ni hatari kwa afya ya binadamu. Jee, nyama zinazoingizwa nchni zinapimwa usalama wake na taasisi gani kabla ya wananchi kuuziwa nyama hizo na Wizara inatoa tamko gani kuwathibitishia wananchi kuhusu usalama wa nyama hizo.
c) Jee, serikali katika kipindi cha mwaka mmoja imeweza kupata kiasi gani cha mapato kwa kuku wanaoingizwa katika soko la Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi –** Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 kama ifuatavyo ambalo linahusiana na wimbi kubwa la nyama kuku kutoka nje ya nchi kuingizwa katika soko la Zanzibar, kitu ambacho kwa kweli kinaathiri wafugaji wa ndani na swali lake lilikuwa jee serikali ina mpango gani kuwalinda wafugaji hao ndani ya nchi.

Ni kweli kwamba kuna athari ambayo inapatikana lakini hata hivyo serikali ina mpango wa kuwasaidia wafugaji wetu wa kuku kwa kuwapatia taaluma ya uzalishaji wa kuku wa bidhaa bora zinazovutia soko kwa ufanisi.

Wizara yangu imekwisha andaa waraka maalum kuhusu mpango wa kuimarisha ufugaji wa kuku hapa Zanzibar na kuomba kusaidia pembejeo za uzalishaji mifugo ikiwemo chakula na madawa ili wafugaji wetu nao waweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuweza kuuza bidhaa zao kwa bei ya kuvutia ili waweze kushindana na wazalishaji kutoka nje.

Waraka huo umekwisha kuwasilishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na baadae utawasilishwa serikalini.

Lakini vile vile aliuliza kwa kuwa kuna maradhi ya mifugo ambayo ni hatari kwa afya za binadamu, jee nyama zinazoagizwa nchini zinapimwa usalama wake.

Kwa ufupi ni kwamba hakuna nyama ambayo inayokuja bila ya kupimwa usalama wake na jukumu hili kwa bahati mbaya halipo mikononi mwetu Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Jukumu hili la usalama wa bidhaa za chakula kwa kweli lipo chini ya Wizara ya Afya kupitia Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi.

Lakini hata hivyo kwa sababu sisi ni wafugaji na wavuvi bado tunashirikiana na Bodi hiyo ili kuona kwamba shughuli hiyo inakwenda salama kabisa. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi bidhaa zote zinazoingia hapa na hususan bidhaa ya kuku basi zipo chini ya usalama mkubwa.

Lakini swali lake jengine anasema serikali katika kipindi cha mwaka mmoja imeweza kupata kiasi gani cha mapato.

Ni kweli vile vile niseme suala hili halipo ndani ya mikono yetu ni suala ambalo lipo chini ya Taasisi Maalum ya Ukusanyaji wa Mapato ambayo munaelewa nyote ni ZRB. Lakini hata hivyo labda nikupe wastani tu wa mapato unaoingizwa kwa makontena.

Makontena 45 ambayo yanakuwa karibu tani 1199 kwa mwaka na ushuru kwa kila kontena ni wastani wa shilingi milioni 8 mpaka 10. Hiyo ni kwa kontena moja.

Aidha yapo mapato mengine yanayopatikana na kazi za ukaguzi vile vile, kuna laki tatu kwa kontena moja na kazi nyengine za kibiashara ambazo zinapata mapato kwa watu binafsi au serikali.

Kwa ufupi ni kwamba kuja kwa kuku hawa kuna ajira kubwa vile vile, sio kwamba tu serikali inapata mapato lakini vile vile kuna kazi ambazo wananchi wetu wanazipata kutokana uagizishwaji huo wa kuku.
**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na nakushukuru kwa majibu hayo.

Wafugaji hivi sasa Wazanzibari au Wazanzibari wazalendo wamekuwa na kilio na kuathiri soko lao la ndani. Jee, serikali inatoa kauli gani kuwalinda kama Serikali ya Muungano inavyolinda viwanda vyake vya sukari, sukari inayotoka nje pale ushuru wake unakuwa ni mkubwa.

Jee, unawashauri vipi kulinda soko hili. Pili, kwa kuwa kuku hao sehemu wanakotoka kuna maradhi, kesi ngapi zimesharipotiwa mpaka muda huu.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, nafikiri kama nilivyotangulia kusema awali kwamba serikali imeliona hilo na inawajali sana wafugaji wake na ndio maana tumesema tutoe taaluma hii kwa wafugaji wetu ili na wao waweze kushindana.

Kwa sababu kwa mujibu wa sheria za biashara hatuwezi kuzuia kwa sababu biashara ipo huru, tokea mwaka 1984 imekuja sera hiyo ya *trade liberalisation* na mwaka 1989 wakaimarisha zaidi na bado inataka kuimarishwa zaidi.

Kwa hivyo hatuwezi kuzuia biashara hiyo. Cha kufanya ni nini. Ni kuwashajihisha wafugaji wetu kwa kuwapa pembejeo kama nilivyoelezea awali hapa ili na wao waweze kupata ile gharama nafuu ya uzalishaji ili waweze kushindana, kwa sababu biashara huwezi kuiondoa hivi hivi isipokuwa na wewe ushindane.

**Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambayo ameyatoa hapa, ningelimuomba Mhe. Waziri aelezee Baraza hili tukufu mahitaji ya kuku kwa Zanzibar ni asilimia ngapi, wazalishaji wetu wanaozalisha kuku Zanzibar wanazalisha asilimia ngapi.

Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kwa kweli tumefanya utafiti huo wa kina na mahitaji ya kuku kwa ujumla ndani ya Zanzibar ni tani laki sita mia mbili na arobaini, hayo ni mahitaji ya jumla. Lakini ni tani ngapi tunazozalisha sisi hapa.
Sisi tunazalisha tani laki moja, mia tisa na arobaini na nne, utakuta pana utofauti zaidi ya laki nne na ushee, hizo maana yake hazipo. Sasa nani wa kuzizalisha. Tukasema hapana waachiwe wafanyabiashara waagizishie kwa sababu kwa kuzinatia kwamba utalii unakua, idadi ya mahoteli inaongezeka na huwezi ukawazuia watu na wao wana mahitaji yao. Kwa hivyo ni lazima tuwaachie huru ili waagizie.

Hapo itakapofika level kwamba sasa wazalishaji wetu wamefikia kiwango hicho bila shaka *automatically* tutazuia wenyewe kwa kweli itasimama. Ni sawa sawa na wewe maana yake fardhi yako ndani ya nyumba kilo tatu, lakini uwezo wako ni kilo moja. Jee, utawalisha kilo moja kila siku, utasababisha mgogoro.

Kwa hivyo utalazimika ni lazima uagizishie kilo mbili zaidi ili kukidhi familia na hiki ndicho kinachotokezea ndani ya Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, nashukuru kupata hii nafasi.

Mhe. Spika, inasemekana kama chakula na dawa zinazofika hapa Zanzibar zimekwishaharibika na wafugaji wetu wanapotumia chakula hiki na dawa wanapoteza mifugo yao kwa wingi. Jee, wizara yako inalijua hili.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, nashukuru naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kweli sijapata taarifa hiyo kwamba chakula kinachotoka nje kinakuwa na madhara au kinakuwa kimeharibika, lakini kwa sababu ndio umeshanipa changamoto wacha nipe muda nilifanyie utafiti kama kweli au laa.

Lakini cha msingi hapa si chakula kuharibika, cha msingi ni kwamba bei ya chakula na dawa ni ghali. Ndio maana tukasema wacha tuwashajihishe wafugaji wetu tupeleke waraka serikali ili tupunguze bei ili wafugaji wetu na wao wapate nafuu ya uzalishaji ili waweze kushindana na kuku wanaotoka nje.

Nashukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Salma Mussa Bilali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri serikali imekuwa ikihimiza wananchi kila siku kuanzisha vikundi mbali mbali vya uzalishaji vikiwemo vya kuku wa nyama na mayai, na kwkila siku kuanzisha vikundi mbali mbali vya uzalishaji vikiwemo vya kuku wa nyama na mayai, na kwa kuwa serikali bado inataka kuendelea kuwaruhusu hao wafanyabiashara hawa kuku aina ya paja nono.

Jee, Mhe. Waziri haoni kwamba kuendelea kuwaruhusu kuku kuingizwa ni kuwavunja moyo wazalendo wazalishaji wa kuku hapa na kuwapunguzia soko na ile dhana ya kuwaondoshea umaskini anaivunja nguvu.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika, nimelisikia swali lake na kwa kweli nimelijibu katika swali mama kwamba ni kweli inavunja moyo, lakini tutizame kwa sababu tumeshatoa takwimu hapa, mahitaji ya nchi nzima ni kiasi gani.

Maana nimetoa mfano hapa kwa familia yako, wewe fardhi yako ndani ya familia yako pengine ni ratili tatu au kilo tatu tuseme, lakini uzalishaji wako ni kilo moja tu, jee utaiacha hiyo familia yako ikae na njaa muda wote si utasababisha mgogoro ndani ya familia. Sasa ndicho kinachotokea.

Halafu isitoshe kwa sababu hapa tuna sheria ya biashara huru, hatuwezi kumzuia mfanyabiashara asilete biashara wakati tumempa uhuru huo. Cha kufanya nini ni kumshajihisha mfugaji au mkulima wetu au mfanyabiashara ndio haki hizi ambazo tumezitaja hapa, tutawapa mbegu bora za kuku, tutapunguza gharama za uzalishaji, chakula, dawa *of course* baada ya muda atakuwa ile gharama yake ya uzalishaji itakuwa ni ndogo na kwanza atakuwa anapata *good quality*.

Kwa hivyo ataweza kushindana na sio tumwambie kwamba tuzuie biashara, hiyo haiwezekani hivyo, hii ni biashara huru hatuwezi kuzuia. Ahsante sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya 2005

*(Kusomwa kwa mara ya Pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii ya leo tukiwa wazima wa afya tukiendelea na shughuli zetu. Sasa naomba kwa ruhusa yako niwasilishe marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ya Afisi ya Usajili na Kazi Vitambulisho Zanzibar.

Mhe. Spika, pili naomba nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ikiongozwa na Mhe. Mwenyekiti wake; Mhe. Hamza Hassan Juma akisaidiwa na Makamo Mwenyekiti Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi pamoja na kamati nzima, kwa kweli tulikuwa na mjadala mzuri, majadiliano mazuri na hatimaye tukafanya marekebisho na tukakubaliana kwamba mswada huu sasa uteremke bondeni kwa majadiliano. Tunaishukuru sana kamati majadiliano tuliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, historia inaonesha kwamba katika mwaka 1966 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha sheria ya Kuanzisha Utaratibu wa Utoaji wa Vitambulisho kwa Wananchi na Wageni.

Vitambulisho kwa wananchi vilijulikana kama pasi ya uraia na kwa wageni ilijulikana kama pasi ya wakaazi. Hata hivyo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii, matumizi ya vitambulisho hivi yalitoweka.

Mhe. Spika, mnamo mwaka 2005 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho chini ya sheria ya Nam. 7 ya 2005. Lengo kuu la kuanzisha Afisi hiyo ilikuwa ni kuwasajili Wazanzibari wakaazi. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kimaendelea yanatokea katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa soko la pamoja la Afrika ya Mashariki, kuongezeka shughuli za uwekezaji na kuimarika la utalii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeridhia utoaji wa vitambulisho sio tu kwa Wazanzibari Wakaazi bali

pia kwa wageni wanaokaa Zanzibar. Hatua hii inaenda sambamba na matamshi ya sera za usajili na utoaji wa vitambulisho iliyoanza kutumika mwaka 2008.

Mhe. Spika, utaratibu wa kuwasajili wageni wanaoingia hivi sasa unafanywa na Idara ya Uhamiaji chini ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 1995 ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha usajili wa wageni wanaofanyakazi Zanzibar hufanywa na Kamisheni ya Kazi wakati wa kutoa vibali vya kazi. Hivi karibuni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuja na utaratibu wa sheria itakayotoa kadi kwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutoa vibali kwa wageni wote wanaoishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Taifa ya Utoaji Vitambulisho (NIDA).

Mhe. Spika, ingawa zipo taratibu mbali mbali za usajili na utoaji wa vitambulisho kwa wageni, lakini utaratibu unaopendekezwa wa kuipa uwezo Afisi ya Usajili na Kadi ya Vitambulisho Zanzibar kutoa vitambulisho na kuwasajili wageni katika *database* yake hazitozuia wala hazitoingiliana au hazitoingilia mamlaka hizo katika uendeshaji wa kazi zake.

Mhe. Spika, madhumuni makuu ya waraka huu ni kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ili itoe uwezo kwa Ofisi ya Usajili na Utoaji Vitambulisho Zanzibar, kufanya usajili na utoaji vitambulisho kwa wageni wanaoishi Zanzibar. Hatua hii itasaidia kisheria kukusanya taarifa binafsi za wageni na kuhifadhiwa katika mtandao ulio salama pamoja na kuruhusu uchukuaji wa alama za vidole kwa wale wote watakaosajiliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi wa nani Mzanzibari. Kumekuwa na maswali mengi kwamba tutofautishe nani Mzanzibari na nani Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, tafsiri ya Mzanzibari kwa mujibu wa sheria nambari 5 ya mwaka 1995 ni kama ifuatavyo:-

1. Mzanzibari kwa asili. Mzanzibari kwa asili anakuwa na sifa zifuatazo:-
   (a) Amekuwa akiishi Zanzibar kabla na hadi tarehe 12/01/1964.
   (b) Amezaliwa Zanzibar na alau mmoja kati ya wazazi wake ni Mzanzibari.
   (c) Amekuwa ni Mzanzibari kabla ya tarehe 26/04/1964 na ambaye hajapoteza uraia wa Tanzania.

2. Mzanzibari wa Kujiandikisha. Mtu huyu ni yule ambaye ni Mtanzania na ametimiza masharti yote yafuatayo:-

   (a) Ameishi Zanzibar kwa miaka isiyopungua 10 mfululizo.
   (b) Anaweza kuandika na kusoma.
   (c) Ana tabia nzuri.
   (d) Ameingia Zanzibar kihalali na kufuata sheria na kanuni za Zanzibar.
   (e) Amefikia umri wa miaka 18 na mwisho,
   (f) Anakusudia kuishi Zanzibar na anaweza kuwa Mzanzibari.

Sasa nani Mzanzibari Mkaazi. Mzanzibari Mkaazi ni mtu mwenye sifa ya Mzanzibari hizo nilizozitaja hapo juu, kama ilivyofafanuliwa katika sheria nambari 5 ya mwaka 1985. Pia awe ametimiza sharti la kuwa na makaazi ya kudumu Zanzibar. Hilo ndio suala la msingi, anam-*qualify* Mzanzibari Mkaazi. Naomba kusisitiza, awe ametimiza sharti la kuwa na makaazi ya kudumu Zanzibar.

Nimeona nitoe ufafanuzi kwa sababu tumekuwa tukiulizwa maswali mengi, tofauti ya Mzanzibari na Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, Mapendekezo ya Marekebisho na Sababu zake. Mhe. Spika, inapendekezwa kwamba ili serikali iweze kutoa vitambulisho kwa wageni sheria nambari 7 ya mwaka 2005, ni lazima ifanyiwe marekebisho katika vifungu nambari 2, 6, 7, 10, 12 na 14 iendane na mambo ambayo serikali inataraji kuyatekeleza kisheria.

Lengo la serikali ni kufanya marekebisho ya sheria nambari 7 ya mwaka 2005 inatokana na sababu zifuatazo:-

1. Sheria nambari 7 ya mwaka 2005 inayotumika hivi sasa hairuhusu usajili wa wageni. Kwa kufanya marekebisho haya, itaweza kuwasajili wageni na kuwapa vitambulisho kwa mujibu wa sheria.

Tunakumbuka Waheshimiwa Wajumbe mara nyingi sana mmekuwa mkiniuliza na mkiilalamikia serikali kwamba kuna wageni wanapata vitambulisho vya Uzanzibari na hawastahiki. Hilo tumelifuatilia na tumeona kweli, wapo wanaovipata hivyo vitambulisho kwa kimakosa. Kwa hivyo, tumejaribu kuwafuatilia kesi zao ziko Uhamiaji na wengine wako polisi. Sasa tumeona dawa au suluhisho la hili ni sheria hii na vitambulisho vitakavyotolewa vitakuwa ni tofauti, vile ni vya Mzanzibari Mkaazi na wageni.

Kwa hivyo, naomba nisambaze aina ya hivyo vitambulisho ambavyo vitatolewa ili mpate kuviona. Naomba aanze Mhe. Spika, halafu wengine nao wapate kukiona.

2. Mhe. Spika, sababu ya pili serikali itakuwa na uwezo wa kisheria kukusanya taarifa binafsi za mgeni na kuhifadhiwa katika mtandao ulio salama, pamoja na kuruhusu uchukuaji wa alama za vidole vya muombaji.

3. Kuifanyia marekebisho sheria nambari 7 ya mwaka 2005, itapelekea utekelezaji wa sera ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, ambayo katika sura ya 3, kifungu nambari 19 cha sera hiyo imeelezea utoaji wa vitambulisho kwa wageni. Hayo marekebisho ya sheria tunayoyafanya tayari yameshatamkwa katika sera yetu, ambayo serikali imeshaikubali.

4. Serikali hivi sasa imeweza kuwatambua Wazanzibari Wakaazi na wapi walipo, kwa kufanya marekebisho hayo, serikali itaweza kuwatambua wageni wote waliopo hapa Zanzibar, pamoja na kujua wapi wapo na wanafanya shughuli gani wakiwa hapa nchini mwetu.

5. Serikali itaweza pia kumtambua mgeni yeyote kiurahisi zaidi, endapo atapata matatizo ama akifariki na maiti yake ikiwa imeharibika sana. Kama ilivyotokezea juzi katika ajali ya Meli ya MV Skagit.
6. Kuwasajili wageni kutaipelekea serikali iwe na *data base* ya wageni, ambayo pia itatusaidia sana taasisi nyengine za serikali kama vile ZRB, ZSSF, ZIPA, Kamisheni ya Kazi na Idara ya Uhamiaji kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

7. Mhe. Spika, katika hali ya sasa imekuwa ni vigumu kwa serikali kudhibiti wimbi la wageni waliopo hapa nchini, kama nilivyosema hapo awali ambao wanaishi kinyume na sheria na hivyo kushindwa kuimarisha ulinzi na usalama wa Zanzibar, kwa kufanya marekebisho kwa sheria hiyo na ikaweza kuwasajili wageni, itapelekea kudhibiti vyema wimbi la wageni waishio Zanzibar pamoja na kuimarika kwa ulinzi na usalama.

8. Pia kwa kuwasajili wageni na kuwapa vitambulisho itasaidia sana katika mipango ya kiuchumi na maendeleo ya serikali.

9. Serikali hivi sasa inaelekea katika utekelezaji wa uendeshaji wa shughuli zake kwa njia ya mtandao, yaani E-*govement*. Ili kuwe na ufanisi wa utekelezaji wa azma hiyo, ni budi kuwepo na *data base* zenye taarifa sahihi zitakazoweza kutoa takwimu na uchambuzi katika maeneo yote. Kwa hivi sasa serikali inazo *data base* za Wazanzibari Wakaazi, wafanyakazi wa serikali, walipa kodi na wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Pia serikali inaendelea na utaratibu wa kuwa na *data base* ya vizazi na vifo na ya umiliki wa ardhi.

10. Mhe. Spika, marekebisho ya sheria hii pia yataiwezesha serikali kuwa na *data base* ya wataalamu wa kigeni waliopo nchini. Wawekezaji wa kigeni, wakimbizi na wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum. Hao watu tunao wamekuwa miongoni mwetu lakini hawatambuliki, wamekuwa kama nao ni Wazanzibari wa kawaida. Kwa hivyo, utaratibu huu utaweza kuweka *data base* ya kuwatambua wataalamu wote na wengine wote wanaojaribu kuwekeza na wanaoingia nchini mwetu.

Mwisho Mhe. Spika, taarifa hizi muhimu ni muhimu sana kwa mipango ya kiuchumi, usalama na mipango ya maendeleo ya nchi yetu. Aidha, *data base* zote hizi zikikamilika, zitaondoa haja ya kufanya sensa kila baada ya miaka 10, kwani taarifa zote zitaweza kupatikana kwa urahisi na hivyo kuokoa fedha nyingi zitakazotumika hivi sasa kwa utekelezaji wa zoezi hilo la sensa ya watu.

Mhe. Spika, sasa naomba nielezee muhtasari wa mswada wenyewe wa mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya usajili wa Mzanzibari Mkaazi nambari 7 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, ili serikali iweze kutoa vitambulisho kwa wageni, inapendekezwa kwamba sheria nambari 7 ya mwaka 2005 ifanyiwe marekebisho katika vifungu nambari 2, 6,7,10, 12 na 14.

Mswada wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi nambari 7 ya mwaka 2005, na mambo mengine yanayohusiana na hayo, una jumla ya vifungu 8 kama hivi ifuatavyo:-

Kifungu cha 1 cha mswada kinaelezea jina fupi la sheria, ambayo itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi, na pia inaelezea kuanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kifungu cha 2 cha mswada, kinaelezea kuwa sheria hii itasomeka kwa pamoja na sheria nambari 7 ya mwaka 2005, ambayo itajulikana kama sheria mama.

Kifungu cha 3 cha mswada huu Mhe. Spika, kinaelezea kuhusu marekebisho ya kifungu cha pili cha sheria mama, ambacho kinahusiana na kuongeza tafsiri ya maneno mapya ambayo ni taarifa za ki-*biometric*, shughuli za kibiashara, mkaazi asiyekuwa Mzanzibari, Afisa Msajili na mkaazi wa muda.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 cha mswada kinarekebisha kifungu cha sita cha sheria mama, kwa kuongeza kifungu kipya cha 6(a). Kifungu hiki kinatoa utaratibu wa kujisajili katika ofisi ya usajili wa Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 cha mswada, kinarekebisha kifungu cha 7(2) cha sheria mama kwa kufuta maneno ‘kidole gumba cha kushoto’ na kuweka badala yake maneno mapya ‘vidole au taarifa nyengine za ki-*biometric* mara tu baada ya neno lake’

Mhe. Spika, kifungu cha 6 cha mswada kinarekebisha kifungu nambari 10(2) cha sheria mama, kwa kufuta maneno ‘kidole gumba cha kushoto’ na kuingiza badala yake maneno yafuatayo:

‘Vidole au taarifa nyengine za ki-*biometric’* mara tu baada ya neno ‘alama’.

Mhe. Spika, kifungu cha 7 cha mswada, kinarekebisha kifungu nambari 12 cha sheria mama kwa kufuta maneno ‘Mzanzibari Mkaazi’ na kuingiza maneno mapya ‘anayestahiki kusajiliwa chini ya sheria hii’
Marekebisho ya mwisho ni ya kifungu cha 8 cha mswada, kinarekebisha kifungu nambari 14(1) (a) cha sheria mama kwa kuongeza nambari 6(a) mara tu baada ya neno ‘kifungu’.

Hayo ndio marekebisho manane ambayo tunayapendekeza Mhe. Spika, katika mswada wetu huu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo niliyoyatoa hapo juu kuhusu marekebisho ya sheria nambari 7 ya mwaka 2005, ambayo itatoa uwezo wa kutoa vitambulisho kwa wageni wakaazi wa Zanzibar. Sasa naomba kuwasilisha mapendekezo yafuatayo.

1. Kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kukubali na kuridhia marekebisho ya sheria hii, ili kuipa uwezo Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, kutoa vitambulisho kwa wageni.
2. Kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kukubali kuipa uwezo kisheria Ofisi ya Usajili na Kazi za Utambulisho, kuweka kumbukumbu binafsi za wageni. na
3. Kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kukubali kuipa uwezo kisheria, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, kuchukua alama za vidole wakati wa kumfanyia usajili muombaji.

Kwa kuhitimisha Mhe. Spika, utaratibu unaopendekezwa wa kutoa vitambulisho kwa wageni, ni muhimu sana kama nilivyosema kwa kuwatambua wageni wanaoishi nchini. Pia itasaidia katika mipango ya serikali.

Naomba kusisitiza kwamba vitambulisho vitakavyotolewa kwa wageni havitakuwa na mamlaka kama kibali cha kuingilia nchini au ruhusa ya kuishi. Naomba kusisitiza tena hapa kwamba vitambulisho vitakavyotolewa kwa wageni havitakuwa na mamlaka, kama kibali cha kuingilia nchini au ruhusa ya kuishi, bali kitakuwa ni kwa ajili ya utambuzi tu. Vitambulisho vya wageni vitatolewa na Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho kwa wageni

watakaopata ruhusa ya kuishi nchini kutoka Idara ya Uhamiaji. Pia kitambulisho kitakachotolewa kitaendana na muda uliowekwa na Idara ya Uhamiaji wa kuishi nchini mgeni huyo.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe, wamepata fursa ya kuupitia mswada huu na marekebisho yake. Nawaomba waujadili na hatimaye kuupitisha. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuja kusoma hotuba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pili nachukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati.

Mhe. Spika, aidha napenda kuipongeza serikali kupitia Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na watendaji wake kwa kuandaa na hatimae kuweza kutuwasilishia mswada huu mbele ya Kamati kwa lengo la kutoa mapendekezo, maoni na ushauri kwa ajili ya kuuboresha mswada huu kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza letu tukufu leo hii. Lakini pia shukrani zetu ziwaendee wadau walioshiriki katika kujadili na kushauriana na kamati kwa kutoa maoni na ushauri wao mbali mbali, ambao ulisaidia sana Kamati katika kuboresha mswada uliopo mbele yetu, kwani jitihada zao zimeleta faraja kubwa kwa kamati.

Mhe. Spika, pamoja na yote pia napenda nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati kumpongeza ndugu yetu Ibrahim Makungu kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Bububu na kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia jimbo hilo. Hatuna zaidi ya kumwambia isipokuwa karibu Barazani, tupo pamoja nae kushirikiana kusimamia na kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, napenda sasa niwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu, kwa mashirikiano na michango yao muhimu waliyoitoa wakati wa kujadili na kuuchambua mswada huu siku ya tarehe 5/10/2012 na naomba niwataje Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Mhe Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| Mhe Mwanajuma Faki Mdachi | Makamo Mwenyekiti |
| Mhe Ali Salum Haji | Mjumbe |
| Mhe Mgeni Hassan Juma | Mjumbe |
| Mhe Mohammed Haji Khalid | Mjumbe |
| Mhe Ussi Jecha Simai | Mjumbe |
| Mhe Salma Mohammed Ali | Mjumbe |
| Ndg Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| Ndg Ramadhan Kh Masoud | Katibu. |

Mhe. Spika, baada ya kuwataja Wajumbe wa Kamati, naomba pia kutoa pongezi za dhati kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, kupitia kanuni zake kwa kuziwezesha Kamati za Kudumu kukutana na wadau mbali mbali kuhusiana na Miswada inayotaka kuletwa mbele ya Baraza hili, hatua hii ni muhimu kwani inasaidia kuboresha miswada na kuleta ufanisi zaidi kwa serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia kuondoa manung'uniko kutoka kwa wananchi kwani na wao pia wameshirikishwa kwa niaba ya wenzao.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye mswada huu. Mhe. Spika madhumuni ya mswada huu ni kuweka utaratibu bora wa utambuzi wa wakaazi wote wa Zanzibar na wasiokuwa Wazanzibari kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa huduma mbali mbali zinazotolewa na taasisi za umma hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Sheria hii ni marekebisho ya Sheria ya Mzanzibari Mkaazi ya mwaka 2012, Kamati yangu inaipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wananchi wa Zanzibar, kwa kuona kuwa hivi sasa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la vitendo vya uhalifu na ukiukwaji mkubwa wa maadili ya Kizanzibari ikiwemo wizi wa kutumia nguvu, uporaji, pamoja na ukahaba na uvaaji wa nguo kinyume na maadili ya Mzanzibari. Kamati yangu inaamini kuwa marekebisho ya sheria hii yatasaidia ulinzi na usalama katika nchi yetu kwa kuwatambua wakaazi wote walioko hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati yangu imeupitia mswada huu na imeridhika kuwa ni mswada wa wananchi unaowalenga moja kwa moja. Mhe. Spika, kuna baadhi ya vyombo vya habari na baadhi ya watu kwa utashi wao, wamejaribu kuikejeli sheria hii eti inalenga kuwabagua watu kutoka Tanzania Bara, jambo ambalo si sahihi hata kidogo.

Mhe. Spika, sheria hii inalenga kuwapatia vitambulisho wakaazi wote waliopo Zanzibar wakiwemo wageni wote sio kutoka Bara peke yake, lakini hata kutoka nje ya nchi yetu kama vile Italy, Marekani, Ufaransa, Uingereza, Kenya, Uganda, Ghana na kadhalika. Hata hivyo, sheria hii ina nia nzuri, kwani tayari imeshawapatia Wazanzibari vitambulisho vya ukaazi seuze waliokuwa si Wazanzibari. Kwa hivyo, naomba kwa wale wenye fikra potofu au kupotoshwa kuachana na fikra hizo wajue kuwa lengo la serikali ni kuwatambua wakaazi wote waliokuwepo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, ni hivi karibuni tu nchi yetu ilikuwa na zoezi la uandikishaji wa sensa na madhumuni ya sensa hiyo, ilikuwa ni kuwatambua watu waliokuwepo nchini kwetu, ili serikali yetu kuweza kupanga mipango ya maendeleo kwa wananchi wake, ili kuweza kutoa huduma bora zinazostahiki. Kwa hivyo, sheria hii nadhani haina tofauti sana na malengo hayo kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pia kumekuwa na malalamiko ya ajira hasa katika maeneo ya sekta za hoteli za kitalii, kupewa ajira watu kutoka Ulaya na nchi nyengine, wakati ajira hizo wazawa wana uwezo nazo na ujuzi nazo jambo ambalo ni kinyume na sheria zetu hapa Zanzibar. Sasa sheria hii itakuwa ndio muarubaini wa tatizo hilo. Pia kuna baadhi ya biashara ambazo zimetungiwa sheria kuwa zinaruhusiwa kufanywa na wenyeji tu na sio raia wa Kigeni, ndio maana sheria hiyo ikamtambua mkaazi yeyote aliyepo Zanzibar na shughuli anayoifanya.

Mhe. Spika, pia kutokana na uingiaji wa wageni kiholela hapa Zanzibar kuna baadhi ya watu wanaingia Zanzibar bila ya kutambulikana na wakati mwengine hupata matatizo. Aidha, ajali au kifo na inakuwa hakuna njia nyengine yoyote ya kuweza kuwatambua, lakini sheria hii itaweza kusaidia sana kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Spika, sheria hii itaweza kuondoa malalamiko yanayotolewa wakati wa uchaguzi, kwani kuna watu wasiokuwa Wazanzibari ambao huwa wanashiriki kinyume cha sheria kupiga kura ya kumchagua Rais wa Zanzibar, uwakilishi pamoja na madiwani ambao wakati mwengine wanakuwa wao sio Wazanzibari.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako, kwa wale Wajumbe ambao waliokuwa na hii hotuba yangu, tuiruke kidogo katika ukurasa wa 5 na niendelee katika ukurasa wa 6, baadae nitakuja kukamilisha.

Mhe. Spika, **K**amati inapendekeza kifungu cha 6A (3) (a) kijumuishe pia wafanyakazi ambao hawana mkataba wa maandishi kama ambavyo unatambuliwa kisheria.

Mhe. Spika, kwa sababu katika sheria hii nilisema kwamba itawatambua tu wale ambao wana mikataba ya maandishi. Lakini katika sheria zetu tulizotunga Mhe. Spika, kuna baadhi ya mikataba ambayo haiko katika maandishi, lakini sheria imemkubali. Kwa hivyo, mapendekezo yetu katika kifungu cha 6A (3) hilo naomba lisomeke hivyo.

Mhe. Spika, lakini pia katika kifungu cha 6A (3) (c) kuwepo na orodha ya masharti na vigezo, kwa wafanyakazi wasiokuwa Wazanzibari kwa lengo la kudhibiti matatizo ambayo yanajitokeza kwa wafanyakazi hao katika mazingira tofauti.

Vile vile kuwepo adhabu kwa muajiri yeyote atakayekwenda kinyume na kifungu cha 6A (4), pamoja na marekebisho madogo madogo yaliyojitokeza katika herufi ambayo Kamati yangu imeyaona.
Mhe. Spika, mbali na malengo yaliyokusudiwa na sheria hii, Kamati pia imeona ni vizuri ikashauri wizara kufanya mambo yafuatayo kwa lengo la kuboresha zaidi nia na dhamira ya serikali kwa wananchi kuupitia mswada huu.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapendekeza sheria iwatambue wakaazi wasiokuwa Wazanzibari, ambao ni wanafunzi kutoka nchi za nje ambao wanasoma hapa Zanzibar kwa lengo la usalama wao na usalama wa nchi kwa ujumla. Pia kuwepo na vitambulisho maalum kwa wanafunzi ambao hawajatimiza umri wa miaka 18, hii ni kwa lengo la kuwatambua na kwa usalama wakati wa pirika zao za kutafuta elimu, kwani huwalazimu kuwepo nje ya nyumba zao nyakati za usiku.

Mhe. Spika, vile vile tunapendekeza kuwepo na utambulisho kwa wafanyabiashara kwa masheha, katika maeneo ambayo wanayofanyia biashara kwa madhumuni ya kutambulika uwepo wao. Lakini pia Kamati yangu inapendekeza kuwa vitambulisho hivyo viwe na rangi tofauti, ili kuweza kumtambua yule aliyenacho ni mtu wa aina gani wakati kitakapokuwa kinahitajika kutumika, kwa madhumuni yoyote yale kulingana na kitambulisho hicho na sababu za kupewa kwake.

Mhe. Spika, naomba anayefuatilia hotuba yangu arejee tena ukurasa wa 8.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia inaishauri serikali pamoja kuwa mswada huu unawalenga wale wakaazi waliopo Zanzibar tu, lakini ni vyema kuweka kifungu cha sheria kitakachowezesha kumpa uwezo Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho, kuandaa utaratibu maalum wa kuwapatia vitambulisho wale Wazanzibari wanaoishi nchi za nje yaani (*DIASPORA*), ili na wao wajihisi kuwa wanathaminiwa na serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili wazidishe mapenzi katika nchi yetu na kuondoa fikra mbovu kwa nchi yao au serikali yao. Lakini vile vile kujenga matumaini kuwa na wao wanakubalika. Mhe. Spika, hii itakuwa ni chachu na jambo hili litasaidia katika maendeleo ya nchi yetu, kwani tunawahitaji sana katika mchango wao wa mawazo.

Mhe. Spika, **K**amati yangu inaamini kuwa ombi letu hili kwa serikali litakuwa sio jambo gumu kutekelezwa, kwani hivi sasa tayari serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha idara maalum katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inachoshughulikia na kuratibu masuala ya Wazanzibari wanaoishi nchi za nje yaani (*DIASPORA*) na pamoja na upya wake, lakini wameanza kazi kwa vizuri na kuanza kuwasiliana na Wazanzibari walioko nchi za nje, ili kushiriki katika maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo, ni lazima ndugu zetu hawa kuwapa utambulisho maalum, ili kuwatambua wapi walipo na shughuli zao wanazozifanya na kuweza kuwasiliana nao kwa jambo lolote tunalohisi wanaweza wakatoa mchango wao wa mawazo, fikra, busara au hata msaada wa mambo mbali mbali, naamini serikali yetu itaona umuhimu wa ndugu zetu hawa kuwaangalia.

Mhe. Spika, tumeshuhudia baadhi ya ndugu zetu kama wakija hapa Zanzibar na kushirikiana na familia zao, marafiki zao na hata serikali yetu kwa kiasi fulani jamii yetu kwa njia moja au nyengine wanachangia maendeleo ya nchi yetu. Kuwatambua Wazanzibari waishio nchi za nje, ikiwa utawekwa utaratibu maalum nchi yetu itafaidika, kwani kuna baadhi ya nchi kama India au Srilanka na nchi nyengine (*DIASPORA*) hawa huchangia pato la taifa kwa kuweka utaratibu maalum hasa wa kutuma fedha katika nchi zao.

Mhe. Spika, baada ya hayo nataka nitoe maoni machache katika kusisitiza hili. Mhe. Spika, tunaelewa kwamba sheria hii inawatambua zaidi Wazanzibari Wakaazi, lakini kwa kuwa tumeanzisha Idara ya Kuwasimamia Wazanzibari waishio huko nchi za nje, ambao inasimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu, kuweza kuwatambua wote hawa, ni lazima kuwepo na utambulisho maalum. Mhe. Spika, wenzetu hawa kwa kushirikiana nao basi wanaweza wakatusaidia mambo mengi. Nafikiri jana nilizungumza.

Vile vile kuna wengine ambao wao wako tayari kushirikiana na serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuboresha elimu ya kompyuta hapa Zanzibar. Ndio maana tukasema kwamba sio lazima sheria hii iwatambue moja kwa moja, lakini serikali tunajaribu kushauri tu, kuangalia uwezekano. Kwa sababu ile idara iliyokuwepo pale Ikulu haina uwezo wa kutoa vitambulisho, lakini kwa kushirikiana na Idara ya Vitambulisho, ndio maana tukasema itakapofikia hali hiyo, basi Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho, aweze kuwa na mamlaka hiyo ili aweze kufanya kazi hiyo bila ya matatizo yoyote. Ninaamini wataweza kuwasaidia sana ile Idara ambayo inashughulikia (*DIASPORA*) hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini pamoja na hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, ahsante kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii kufika hapa kuendeleza kazi zetu za kawaida katika Baraza hili tukufu.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia mswada huu ambao hivi sasa upo mbele yetu unaohusu Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri nchi kuwa na utaratibu wa kuwatambua wakaazi wake halisi. Wakati Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha hoja yake aliwagawa wazanzibari katika vikundi tofauti.

Kwa hivyo, kuna wale ambao waliokuwepo kabla ya Januari 1964 ambao tulikuwa wazanzibari wakati huo, wale waliozaliwa baada ya hapo na angalau mmoja kati ya wazazi wao ni wazanzibari na wale ambao ni wazanzibari wa kuandikishwa kulingana na alivyosema yeye iwe ni mtanzania ambaye ameishi Zanzibar kwa miaka kumi mfululizo, nadhani kifungu hichi kimerekebishwa na wala sina hakika.

Lakini tuchukulie kama alivyokisema yeye iwe ameishi kwa miaka kumi mfululizo, hii ina maana kwamba mtu huyo kama atakaa miaka tisa na nusu hatimaye akaondoka, basi akija iwe anaanza upya kuutafuta uzanzibari, kwa sababu ile miaka kumi itakuwa haikutimia.

Mhe. Spika, kwanza niache huku na nije huku kwa mzanzibari kama alivyoelezwa, kuna mzanzibari ambapo yupo mzanzibari mkaazi na mzanzibari huyu iwe hapungui umri wa miaka 18 kwa ajili ya kupata kitambulisho, yaani umri wake uwe ni miaka 18 kwenda juu na haya ndiyo masharti ya kupata Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Kwa hivyo, kwanza mtu awe ni mzanzibari, awe ni mzanzibari mkaazi mwenye makaazi ya kudumu na awe na umri wa miaka 18 kwenda juu. Mhe. Spika, haya ndio masharti, lakini masharti haya baadhi ya wakati yanakiukwa ya kupata hichi kitambulisho.

Mhe. Spika, mimi ni mzanzibari wa asili lakini pengine kwa kutojua kwangu umuhimu wa baadhi ya mambo kwamba mwanangu nimemzaa hapa na ametimia huu umri uliotajwa wa kimasharti, lakini mara nyingi pamoja na kwamba amefikia umri wa miaka 18 inakuwa kupata kitambulisho hichi inakuwa ni vigumu. Kwa hivyo, hili kwenye marekebisho haya lazima ichukuliwe hatua.

Mhe. Spika, mtu mwenye umri kama wangu ni mzanzibari wa tangu siku hizo, lakini anataka Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi anatakiwa cheti cha kuzaliwa, hivi ni kweli mtu mwenye umri wa Mohammed Haji Khalid hajafika miaka 18 na wako watu wamezaliwa Mwambe na hata Kengeja hawajafika, maana yake hawajaondoka lakini kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa tu mtu mwenye umri kama huu, basi anakosa kitambulisho eti kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa. Hivi ni kweli mtu mwenye umri wangu unamwambia alete cheti na humpi kwa sababu una wasi wasi kwamba hajatimia miaka 18.
Kwa kweli hii ni moja katika kasoro ambayo Mhe. Spika lazima tuizingatie na tena tutilie maanani kwamba kitambulisho hichi ni muhimu kwamba lazima mzanzibari mkaazi awe nacho, na pale ambapo amekikosa kuna adhabu. Hivi je, tunakusudia mara nyengine mtu au rai ama mzanzibari wetu aadhibiwe kwa kosa ambalo si lake.

Kwa hivyo, matatizo haya lazima Mhe. Spika tuyapatie ufumbuzi, ili kila mzanzibari mkaazi ambaye yupo kwa kuzingatia masharti haya matatu yaliyotajwa, basi apatiwe kitambulisho cha mzanzibari mkaazi. Kwa mfano, wengine wanaishi Zanzibar na wakati mwengine wanaishi upande wa pili wa muungano, yaani hapa anayo makaazi ya kudumu na kule pia yupo. Mhe. Spika, kwenye ufafanuzi imetajwa kwamba hawa wenye makaazi pande zote mbili anayo haki ya kupata Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, kuna hawa wazanzibari ambao si wakaazi lakini ni wazanzibari wanaokaa nchi za nje tumewataja kwenye ripoti yetu, kulingana na sheria hii wao hawana kitambulisho cha aina yoyote ni wazanzibari lakini si wakaazi wa Zanzibar.

Sasa hawa wao si wageni, maana yake kile tunachowapa wageni wao hawapati na wala hawana chengine chochote watakachopewa je, hawa tuwahesabu vipi nao ni wazanzibari na wengine pengine hata kubadilisha uraia wao hawakubadilisha na hata kama iwe wamebadilisha. Je, pale wanapoamua kukaa Zanzibar ambapo ni kwao kwa muda wa mwaka mmoja au miwili, lakini sheria hii wao haijawataja kwamba wao watapewa kitambulisho cha aina yoyote.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kutujibu atufafanulie hawa wazanzibari hawa wao wana haki gani ya kitambulisho ndani ya nchi yao. Kwa hivyo, tutampa mtu ambaye anayetoka Italy kwa sababu amekuja kukaa Zanzibar kitambulisho cha aina yake, lakini huyu yeye ikawa bado hana hichi kitambulisho.

Mhe. Spika, kama lengo la kuwapa hawa wageni vitambulisho kwa ajili ya kuwatambua, ingawaje Mhe. Waziri amesema kwamba itaondoa ile kufanya sensa. Kwa kweli sensa hivi sasa sote ni watanzania, sasa itakujawezekana kuwa Zanzibar kwa sababu tunavyo vitambulisho vya kuwatambua wageni na sisi tunavyo vitambulisho vyetu na sensa inayokuja ya miaka ya mbele kwa wale watakaokuwa hai ni hivi, ni kweli hawatohesabiwa kwa sababu tumewadhibiti watu wetu katika takwimu hizo.

Kwa hivyo, itawezekana kujivua katika sensa kwenye hali hiyo kwa wakati huo, kwa sababu tu katika *data base* zetu tumewadhibiti wageni, watu walioko ndani ambao ni wakaazi wa kawaida na wengineo.

Sasa ina maana hivi vitambulisho vinataka kuondoa baadhi ya mambo ambayo yapo kiasili, kwa sababu sensa ipo zamani sana na wala sidhani kama itakuja kuwa sahihi ikiwa mfumo huu ukiwepo upande mmoja ukafanya sensa na mwengine haukufanya kwa sababu ya udhibiti huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo la msingi katika sheria hii mabadiliko yanayofanywa ni kuweza kuwapa vitambulisho wageni ambao wanaishi Zanzibar, ili tuwatambue. Lakini ningeomba sana pia isiwasahau wazanzibari wakaazi waliomo ndani ya Zanzibar kukoseshwa vitambulisho hivi kwa sababu mbali mbali. Vitambulisho hivi vinaonesha vina dhamiri mbili tofauti, moja ni dhamiri ya kisiasa na nyengine ya kujua watu ambao wanaoishi Zanzibar na uhalali wao uwepo.

Kwa kweli kisiasa inakuja pale tunapoingia katika mambo ya uchaguzi mkuu wa nchi, hata uwe na umri wa Nabii Nuhu na umezaliwa Zanzibar kama huna kitambulisho basi hutakuwa mpiga kura, kwa hiyo hapa imekuja hali ya kisiasa.

Upande mwengine kutambulika kuwa ni mzanzibari pale kwenye shughuli zao tofauti unapotakiwa uoneshe kitambulisho kuhakikisha kuwa wewe ni kweli mzanzibari na pia ni mzanzibari ambaye unakaa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuwa dhana kubwa ni kwamba mtu awe mzanzibari mkaazi, basi mimi niko Kengeja ni sehemu ya Zanzibar, je anaweza kuamua kuchukua uzanzibari wangu hapa Chukwani, kwa sababu lile sharti la kuwa mzanzibari tayari ninalo ni mkaazi wa Zanzibar na hapa haijaonesha ni mkaazi wa jimbo fulani, kwa sababu sheria inakutaka uwe mkaazi wa Zanzibar.

Kwa hivyo, je nikiamua kuchukua hapa Chukwani sitaambiwa kwamba wewe si mkaazi, kwa nini niambiwe si mkaazi na sheria inasema ni mkaazi wa Zanzibar wa kudumu.

Mhe. Spika, nimeona nivunje huu ukimya wa Baraza na nianze kutoa maoni yangu machache na baada ya kupata ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri, mimi naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema pamoja na wenzangu wote tuliohudhuria ndani ya Baraza lako tukufu.

Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipatia nafasi hii, ili na mimi kutoa maoni yangu katika marekebisho ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Nikiendelea na pongezi pamoja na shukurani zangu za dhati kwa Waziri husika Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuletea marekebisho ya vitambulisho vya mzanzibari mkaazi kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, baada ya pongezi zangu hizo niseme thamani ya mwananchi kupata kitambulisho cha mzanzibari mkaazi ni thamani kubwa, kwa sababu hata nchi za wenzetu wanajuana kwa vitambulisho. Lakini niseme tu kwamba mtu anapokuwa na kitambulisho ni jambo zuri sana, kwa sababu kitambulisho kina maana kubwa tena nzuri kwa mwananchi wa Zanzibar. Kwa nini niseme hivyo, nasema hivyo kwa sababu za msingi.

Kwa kweli hivi sasa kama huna kitambulisho cha mzanzibari mkaazi basi kwenda kuajiriwa ni matatizo, na kama utakwenda kutafuta tiketi ya kusafiria ni matatizo. Vile vile kama huna kitambulisho cha mzanzibari mkaazi kutaka kumchukulia ndugu yako dhamana au mtu mwengine yeyote ni matatizo.

Kutokana na hali hiyo, nasema kwamba kitambulisho cha mzanzibari mkaazi ni jambo muhimu kwa wazanzibari wote, na kila mzanzibari anayo haki ya kupata kitambulisho cha mzanzibari mkaazi, kwa sababu hili jambo tumepitisha kisheria, basi si haki kumnyima mzanzibari yeyote kitambulisho cha mzanzibari mkaazi na kufanya hivyo ni kumuonea.

Mhe. Spika, watu wengi wamekosa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi kwa sababu vigezo vyake vilivyowekwa ni vigumu sana. Kwa mfano, tukiangalia kwenye historia yetu si wazanzibari wengi hasa vijijini wenye vyeti vya kuzaliwa, lakini hiki kimekuwa ni kikwazo kikubwa sana na hili litatupeleka pabaya, kwa sababu gani litatupelekea pabaya.

Kwa mfano, tunasikia kwenye vyombo vya habari kama watu wanachukua vyeti *fake* kwa ajili ya kupata kitambulisho cha mzanzibari mkaazi, kwa sababu anaona kina umuhimu, lakini anapita njia nyengine kutokana na hali hiyo anayosumbuka. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukisema kwamba tukipitisha sheria kama mzanzibari hizi ni haki zake za kimsingi, basi lazima wazanzibari wote wapate haki zao za kimsingi na moja ndio hii hapa.
Mhe. Spika, kuna hasara nyingi sana ambapo mtu amekosa kitambulisho cha mzanzibari mkaazi na hasara moja ni kutoweza kumchagua Rais wako wa Zanzibar na kutoweza kuwachagua Waheshimiwa Wawakilishi sisi ambao tunaozungumza, ambapo ni haki yake.

Mhe. Spika, mtu ni mzanzibri wa kuzaliwa kabisa, yaani amezaliwa. Kwa mfano, kama mimi natoka Kojani, basi *Wallahi* Kojani hawajatoka kwenda Wete pale, lakini haki ya Mungu hawana vitambulisho vya mzanzibari mkaazi, kwa sababu Sheha amepewa mamlaka ya kutoa barua tu kwa ajili ya kupata kitambulisho, kama hamtaki yeye basi hampi kabisa na hili ni tatizo.

Sasa kama tunafanya marekebisho haya Mhe. Waziri husika lazima ujitwike kwamba kweli unafanya marekebisho, hata tukikumbuka ahadi za Rais wetu Mhe. Ali Mohammed Shein alizozitoa kule Bwawani wakati akiwa Rais Mteule, basi alitoa marekebisho haya.

Kwa hivyo, kama tumejikita kwamba kweli atafanya marekebisho yote na watu walikuwa wanapata tabu sana, basi Mhe. Waziri tujikite kweli na wala tusifanye mambo ya kudanganyana, na hapa ni sehemu ya kutunga sheria na watu wote wapate haki zao kwa mujibu wa sheria bila ya hivyo nchi yetu tunaipeleka pabaya.

Mhe. Spika, sisi tumekubaliana tunayo Serikali ya Umoja wa Kitaifa *Alhamdulillah* tunamshukuru Mwenyezi Mungu, mambo yetu yanakwenda vizuri na kila siku tuyaboreshe yaende vizuri na isiwe leo tunalifanya hili na kupinga yale mambo mazuri na mabaya yote tuyaache.

Mhe. Spika, mimi niseme heshima ya mzanzibari kikatiba ni kubwa sana. Kwa mfano, ukitaka kuangalia Katiba hii ya Zanzibar kwenye ukurasa wa 4 ibara ya 9(1) Mhe. Spika naomba ninukuu.

Katiba ya Zanzibar ibara ya 9(1) inaeleza hivi:-

9(1) “Zanzibar itakuwa ni nchi ya demokrasia na haki za kijamii, ambayo ni nchi yetu pamoja na sisi wenyewe.

(2) Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba:

(a) Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe, ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe;

(b) Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la Serikali”.

Mhe. Spika, sasa kama lengo la serikali ndio hilo usalama na leo unamnyima mtu kitambulisho cha mzanzibari kwa fikra zako tu au mambo ya kisiasa, kwamba chama chako kifaidike na mwananchi yule akose haki zake za kimsingi na hili ni tatizo.

Vile vile na mimi nasema kwenye vitambulisho hivi vimekwenda sana kisiasa na kuliko kumjali mzanzibari mwenyewe, kwa nini tunafanya chaguzi na chaguzi zote zilizopita na tunashukuru uchaguzi huu wa mwaka 2010. Lakini zilizopita zote zina matatizo na wala tusielekee huko kwa sababu nchi yetu tutaitia matatizo makubwa na Mwenyezi Mungu atuepushe kuelekea huko na tunao wajibu ni sisi viongozi.

Mhe. Spika, sisi viongozi mimi ninayezungumza hapa, wenzangu wote pamoja na wengine walioko nje tunao wajibu na hata mbele ya Mwenyezi Mungu tunao wajibu mkubwa sana, leo dhamana yoyote uliyopewa Mwenyezi Mungu atakuuliza wale uliokuwa ukiwaongoza ulikuwa ukiwaongoza vipi.

Kwa kweli Mhe. Spika, ni sisi tuliokamata Katiba hii kwa mkono wa kushoto na kukamata msahafu wa Mwenyezi Mungu na tunaapa, lakini nasema wananchi wetu hatuwatendei haki na tunaivunja Katiba. Sasa kama tunaivunja katiba basi na sheria yoyote hatuwezi kuifuata, kwa sababu Katiba ni sheria mama na sheria inayokiuka Katiba ni batili, kwa maana hiyo hii Katiba yenyewe hatuifuati, je tutaweza kufuata sheria nyengine.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, nikiangalia ndani ya Katiba hii kwenye ukurasa wa 7 kuna kinga na haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Katiba ya Zanzibar ibara ya 11(1) inaeleza hivi:-

> 11. (1) Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa.
> (2) Kila mtu anastahiki heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.
>
> 12. (1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria".

Mhe. Spika, Katiba yetu inasema hivi, hebu tuiangalie Katiba nzima hii ni wapi inaposema kwamba watu watumie nguvu au mabavu, lakini inahimiza usawa na mtu kupata haki yake mbele ya sheria na wengine wanabaguliwa kabisa na wala hawapati haki zao za kimsingi.

Mhe. Spika, mimi ninaomba kwa sababu hivi sasa ndio marekebisho ya Sheria hii ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, basi kwanza tuwatambue wale Wazanzibari wote wapate haki zao ndipo tuwatambue wageni kwa kuwasajili.

Kwa hivyo, tukifanya hivyo hapo tutakuwa na nchi yetu nzuri na kila mtu atakuwa amepata haki yake ya kisheria na tunakwenda vizuri ndani ya nchi yetu na siku hadi siku tutafanya shughuli za maendeleo kwa vizuri, lakini kinyume na hivyo mambo mabaya yatajirudia siku hadi siku.

Kwa kweli mtu yeyote ambaye unamnyima haki yake na ikawa ni haki ni yake basi iko siku hatakubali hata kama ukiwa na uwezo gani atakuja juu kudai haki yake. Sasa tuliangalie sana hilo na tukiliangalia hilo Mwenyezi Mungu atatufikisha hapala pazuri.

Mhe. Spika, kwa kutambua hilo ningeomba Mhe. Waziri husika hapa nilimwambia mimi mwenyewe binafsi hapa kama kuna watu waliopiga kura mwaka 2000, 2005 waliitwa pale kilimo na vitambulisho vyao vikatobolewa, na akatuahidi kwamba atakwenda kuwaona, lakini mpaka leo hii bado hajakwenda kuwaona na kutujua ni watu wangapi na wanastahili kupata vitambulisho na hili ni tatizo.

Vile vile sheria inaeleza mtu yeyote aliyetimia umri wa miaka 18 anayo haki ya kupata kitambulisho cha mzanzibari mkaazi, basi kuna haja ya kupita maskuli, watoto wetu wanaosoma kupatiwa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi kwa sababu ni haki yao wote waliotimia umri, pamoja na wale wote ambao hawajapatiwa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi basi wapatiwe haki zao kwa mujibu wa sheria.

Kwa kweli kumnyima mtu sio kumtendea haki ni kinyume na taratibu zetu za sheria na Katiba yetu hii ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la mwaka 2010.

Mhe. Spika, mimi nasema kama kweli tuko wawazi basi ningependelea au ningependekeza ombi langu hili kuwa huko kwenye Serikali za Mitaa, ambao ni masheha basi kungekuwa na Baraza ambalo lina uwiano wa kuwashirikisha watu wote. Kwa kweli mimi nasema sana mambo haya ya vitambulisho yanakwenda sana kisiasa.

Kwa hivyo, kama ni hivyo basi wangeshirikishwa watu wote, yaani vyama vyote vingeshiriki kama vile CUF, Chameda na vyengine vyote wakashiriki, lakini isiwe kwa sababu za utashi wake na ukienda kutaka fomu ya kwenda kuchukulia kitambulisho hakupi, lakini kuna watu wengine wanapata vitambulisho ambao hawastahiki kupata kabisa na hili ni tatizo.

Mhe. Spika, watu wageni wanaingia katika njia za panya na wao pia wanavyo vitambulisho. Kwa mfano, unaweza kumkuta Mmasai anacho kitambulisho na Mzanzibari halisi ambaye mzaliwa hasa hapati kitambulisho.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi mzuri, ili wananchi wetu watufahamu, na ni haki yao kupata vitambulisho na sio ufafanuzi tu. Sasa tuende huko kama kila mtu apate kitambulisho, kwa sababu ni haki ya kila mtu na kila mtu apate hii haki, kwani ukimkosesha kitambulisho utakuwa umemkosesha haki zake nyingi sana za msingi kama nilivyoziainisha hapa.

Mhe. Spika, niliyozungumza yanatosha, lakini mwisho kabisa nasema tujenge tabia ya kuaminiana, ili tujenge taifa lililo bora, kama hatujafikia hivyo basi itakuwa hatufiki katika kujenga nchi yetu na shughuli za maendeleo kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Ussi Jecha Simai:** Mhe. Spika, ahsante sana awali ya yote kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuchukua nafasi hii. Vile vile niwapongeze wale wote ambao jana Mhe. Rais wa Zanzibar amewateua kushika nafasi mbali mbali za uongozi katika serikali yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo moja kwa moja nianze kutoa maelezo kidogo tu kwamba mswada uliopo mbele yetu ni mswada ambao ni muhimu sana, na kwa kiasi kikubwa utapunguza manung'uniko na maswali mengi ambayo yalikuwa yakiulizwa miongoni mwetu.

Kwanza mswada huu una lengo la kuwapatia wakaazi wote ambao wapo Zanzibar vitambulisho vya ukaazi, ambapo kwa mujibu wa mswada huu vitambulisho hivi vitakuwa tofauti kabisa.

Kwa maana hiyo, kila mtu atapata kitambulisho kwa mujibu wa sifa zake za ukaazi wa Zanzibar. Kwa mfano, vitambulisho tulivyonavyo hivi sasa vinatoa fursa nyingi kwa wazanzibari ambao hasa wanakuwa na sifa za kupiga kura pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, mswada huu una lenga moja kwa moja kupunguza masuala ya udanganyifu miongoni mwa watu, ambao hawana sifa za kuwa Wazanzibari kutaka vitambulisho kwa ajili ya shughuli mbali mbali ambazo zinafanywa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, moja kwa moja nikiingia katika Mswada huu katika vifungu mimi ningelipendekeza kwamba katika Mswada huu au katika sheria hii, sheria ingeliwatambua Wazanzibari ambao wako nje ya nchi, wangetafutiwa vitambulisho ili tuweze kuwatambua na tuwajue wako wapi na wanafanya nini. Mimi nadhani hao wangeliweza kutusaidia kwa njia moja au nyengine katika shughuli zetu mbali mbali za maendeleo katika nchi.

Mhe. Spika vile vile katika kifungu cha 6A (3) (a) tujumuishe pia wafanyakazi ambao hawana mikataba. Kwa sababu tunasema kwamba mfanyakazi awe na mkataba lakini kuna wafanyakazi ambao hawana mikataba, nao pia sheria hii ingeliwatambua ili tukawajua wapo hapa kwa ajili gani, wanafanya nini na wanajishughulisha na jambo gani.

Mhe. Spika, kifungu cha 6(3) (c) kingelionesha orodha ya masharti na vigezo kwa wafanyakazi wasiokuwa Wazanzibari kwa lengo la kudhibiti matatizo ambayo yanaweza kujitokeza kwa wafanyakazi hao katika mazingira tofauti.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia ahsante sana.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Nakushukuru Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia machache kwenye Mswada huu muhimu uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, nchi zote duniani kwa namna moja au nyengine serikali zao huwa zinafanya namna ya kuhakikisha ulinzi, usalama wa raia na mali zao. Jukumu hili ni la serikali kupitia viongozi wao. Wizara hii inahusika na suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kachaguliwa Mzanzibari mwenzetu kupewa dhamana hii. Dhamana hii ina umuhimu mkubwa na ina uzito wa pekee. Kwa bahati mbaya sana imetungiwa sheria ulazima wa Mzanzibari kuwa na kitambulisho hichi na kutokuwa nacho ni kosa la jinai.

Mhe. Spika, maajabu yaliyotokea miongoni mwa waliotunga sheria hiyo ndio hao hao wanaosimamia kuwanyima Wazanzibari wengi wao kuwatia kwenye hiyo hatia. Lakini si tu kuwatia hatiani wana wanyima haki kadhaa za msingi pasi na sababu. Kama sababu sipo ni zile binafsi ambazo wamezificha wenyewe ndani ya vifua vyao.

Mhe. Spika, nasema hili  mimi siamini na wala sitoamini kwamba Sheha  kwa mamlaka yake aliyopewa na madaraka anaweza kumnyima mtu barua ya kwamba huyu ni mwananchi anaishi kwenye Shehia yangu ni Mzanzibari, wengine wamezaliwa anafahamu hilo, wazazi wake anawafahamu sheha, lakini kwa sababu alizoagizwa hampi ile barua kwa makusudi. Suala kubwa ambalo tunawaona vijana wetu kuhangaika wakati unapofika uchaguzi mkuu. Sheha bila ya aibu wala haya na hata hisani huwa anaziweka upande. Kijana anayesoma skuli na kijana wake baba yake wanacheza bao pamoja na Sheha anasema hamtambui. Na yule anayekubali kwamba ana mtambua basi anasema fomu hana.

Mimi naamini kwamba tunapokaa hapa na tukazungumza na wahusika kwa mambo haya, maji yao ni mazuri, matamu ya kutoondoa hapa tuondoke na sisi tuende tukawadanganye wale vijana kule. Lakini nia zao zinawasuta ndani ya nafsi kwamba wanayoyajibu sio ya kweli.

Mhe. Spika, wasiostahiki kupewa vitambulisho hivi ndio wanaopewa, anapewa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, anapewa cheti cha kuzaliwa, anapewa paspoti, anahalalishwa kupewa mirathi ya nchi hii kwa utashi tu basi. Wahusika wanayasikia na wanajijua. Kufanya hivi ni dhambi kubwa na ni kosa kubwa.

Jamani baada ya yote dhamana tulizopewa na wenzetu na tukazilia kiapo kuzisimamia na kuzitetea zitakwenda tusuta siku ikifika. Wala hutopongezwa na mtu siku hiyo ni weye na lile ulilolitenda hapa. Sasa sisi tunakwambia unachokitenda ni dhambi na Mwenyezi Mungu hakusamehe kwa sababu unawafanyia watu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sheria tunaendelea kuzitunga, kubadilisha kufuatana na wakati, hii ni kazi yetu na ndio wajibu. Hazitobaki kuwa ni sheria kama hazitumiki vile tulivyokubaliana zitumike. Wala mtu asijidanganye kwa sababu tumeshaipitisha akaona tumempa cheti, akifanya sivyo ni yeye mwenyewe anafanya sivyo. Mimi nitapiga kura kuipitisha lakini hivi ambavyo inavyotafsirika humu. Anayekwenda kuitumia kivyake ni yeye mwenyewe. Kwa kusaidiana kwa vile bado tupo hapa duniani ni vyema kila mmoja atende wajibu wake na tuwatendee haki tuliokubali kuwatendea haki hiyo.
Mhe. Spika, Zanzibar sasa hivi pameingiwa na wimbi kubwa la uhalifu. Uhalifu uliokuwepo Zanzibar sasa hivi ni wa kutisha. Wenzetu wanaokaa maeneo ambayo yanalindwa si ajabu hawana habari na haya. Wananchi wetu huko mitaani hali mbaya tena mbaya sana. Makundi ya watu wanavamia majumba na mapanga na masilaha ya jadi hivi sasa kupora mali zao na kuhatarisha na maisha yao.

Mhe. Spika, nimeshuhudia juzi, nimeshuhudia na jana tena mchana na juzi usiku. Hawa ni wale ambao wamepewa vitambulisho na vyeti vya kuzaliwa hapa Unguja bure kwa maslahi ya hao waliowapa. Faida yako wewe ama kundi dogo ni hasara ya waliobaki wote. Sasa na atizame mtu dhima hii, unafurahi wewe kidogo unawaudhi wote waliobaki, sijui utasema nini?

Mhe. Spika, vyombo vyetu vya ulinzi havitoshi kuwalinda wananchi wote, mji umetanuka, watu wako mbali na maeneo ambayo ni karibu na vituo vya polisi. Lakini pia tunatizama upande mmoja, tunawaingiza watu wasiostahiki ndani ya nchi hii kuwapa uhalali kama kwamba ni raia wa kuzaliwa ama wa kuandikishwa, wapo. Hivi kwa nini hali hii iliyofikia sasa ya uhalifu huu serikali imenyamaza kimya, hakuna hatua yoyote. Hivi kwa sababu wakubwa

mnalindwa, hamjali maisha ya wananchi wenu. Hiyo kuwa wakubwa si kwa kuwepo hawa wananchi, kama hawapo?

Mhe. Spika, maisha yao yapo hatarini hivi sasa, mali zao ziko hatarini, wakubwa nyie mnaolindwa mna raha ya kukaa huko mlipo. Sasa kama mlikuwa taarifa hiyo hamna nakwambieni hali ya wananchi wa Zanzibar ni mbaya mno na imekuwa mbaya kwa kuwaleta watu na kuwathibitisha kwamba ni Wazanzibari ili hali mnajua sio Wazanzibari. Nilisema mara moja mnatoa mirathi ya nchi hii dhulma mnayofanya.

Mhe. Spika, mimi binafsi sasa labda serikali ione haja ya Wazanzibari wamiliki silaha za kujihami maisha yao na mali zao, wakati umefika. Kama serikali imeona imefikia mahali kutoa haki ya Wazanzibari kuwapa wageni wasiostahiki, sasa kwa hawa raia wenye stahiki na nchi yao lazima na wao muwape haki ya kujilinda wenyewe kwa kuwaruhusu wamiliki silaha kwa utaratibu utakaokubalika kwa mujibu wa sheria. Maana wanasema "isiyo mkame hujikamua yenyewe."

Mhe. Spika, sasa msiwadhulumu watu, kuwalinda hamtaki na kuwapa haki ya kujilindanda hamtaki, mnachukua haki zao mnawapa watu wasiostahiki. Mtakwenda jibu na mtakuwa na hali mbaya siku ya Kiyama. Huu si utaratibu hata kidogo mnaoufanya. Sisemi kwa jazba lakini nasema kwa hamasa kubwa kwamba nakuoneeni huruma mnayoyatenda mabaya kiasi hichi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sheria ni nzuri naomba sana tuiheshimu na tuilinde, tutaipitisha kwa makofi makubwa kwa sababu inastahiki na ni nzuri lakini ombi langu na nasaha zangu hatuipitishi sheria hii wanaokwenda kuitumia vibaya wakadhani tumewahalalishia siye, *hasha lillah*. Sisi tunatenda wajibu wetu kwa wananchi wetu katika mazingira hayo ninayoyazungumza.

Ombi maalum kupitia nafasi hii Mhe. Spika, nakuomba uniruhusu kuiomba serikali kwamba Zanzibar imeingiwa na wimbi la uhalifu. Naiomba serikali kwa nguvu zote wasiostahiki kuishi Zanzibar watafutwe. Wapo na wanajulikanwa, warejeshwe au wakae kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi hii.

Mhe. Spika, jana usiku kavamiwa mama mmoja na watu saba na kila mmoja anapanga, watatu wamerukia ukuta wameingia ndani wametoa dirisha. Ndani ya nyumba kuna kijana mmoja tu wa kiume, sikio wakalichana awape ufunguo wafungue mlango mkubwa. Wanne waliobakia wamekaa mlangoni nje, kijana anapiga mayowe hakuna mtu anayethubutu kutoka, kila anayechungulia kutokana na njemba zilizokuwepo uwanjani hakuna mtu anayeweza kufika.

Polisi iko wapi, KVZ iko wapi, KMKM iko wapi, JKU iko wapi, na wote hawa niliowataja kuna siku kila unapotupa jicho wapo. Sasa wasikuwepo kwa harusi tu na msiba pia wawepo. Maisha ya watu ni muhimu, magari makubwa na viti mnavyovikalia mnavikalia kwa jasho la hawa wanyonge, mtakwenda kujibu siku ya siku. Mhe. Spika, hili nalisema kwa uchungu mkubwa ni matungu. Mali mtu kahangaika kapata alichojaaliwa kinakuja kunyanyuliwa nusu saa kubwa, serikali ipo, walinzi tulionao leo karibu ya robo ya Wazanzibari. Kwa nini uhalifu uwe kiasi chote hichi, serikali inasifa kubwa ya Mapinduzi, tunapinduliwa na watu hawa walioletwa juzi hatutambuani, hatuna raha ndani ya nchi yetu wenyewe.

Mhe. Spika, vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, vyende kwa Wazanzibari wanaostahiki kupewa na hatutaki lugha za ubabaishaji. Mtu anakwambia twende kesho nakubwa kwa huyo sheha mwenye matatizo. Tukiondoka hapa hadithi imekwisha. Anasimama na sheha kule Wete anaitwa roho mbaya, roho mbaya ya kuzaliwa na anavyoishi mpaka leo yuko hivyo hivyo habadiliki. Lakini kapata wapi kiburi kile, kapewa na wahusika.

Waziri anayehusika na wizara hii ananisikia, usilazimishe hali ikafikia kuwa mbaya hivi. Watu kuchukiana bure, mtu anamjua huyu amenidhulumu kapewa haki sio yake, mwanangu kanyimwa, watoto wanapoteza masomo, kaitwa na kaka ake angalau akasaidie maisha ya wazee wao hapati kwenda. Kamaliza shule hana kitambulisho chengine isipokuwa hichi, unamnyima kwani tunakusudia nini?

Mhe. Spika, mimi hamshukuru Mwenyezi Mungu, namshukuru zaidi na zaidi na kunifikisha leo nikawa hai na nikaweza kuyasema maneno haya. Kesho wenzangu wala hawatokuja kulaumu kwamba sikuyasema, hapa duniani *Hansard* ipo na *Hansard* kuu siku ya siku iko. Nawasaidia wenzangu wanaoyafanya mabaya haya.

Nataka nimalizie kwa kuiomba serikali. Wazanzibari wanaangamia, wimbi la uhalifu na ujambazi ni kubwa mno linatishia amani. Mhe. Spika nawaomba wakubwa wa nchi hii, nawaombeni tuwatizame kwa jicho la huruma wananchi wetu wamevamiwa, hali ni mbaya. Hawezi tena mtu kutoka akenda harusini saa 2 lakini hata saa 8 ya mchana gari inaibiwa viyoo nje uwanjani. Sio sifa ya Zanzibar hii. Zanzibar wanayoifahamu wenzetu miaka 20 au 30 iliyopita wakisikia haya leo wanalia machozi. Yote haya ni dhima imebebwa na mtu ama kikundi cha watu kwa faida yao.

Mhe. Spika, *message sent and delivered*. Nakushukuru.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, na mimi namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Mswada huu mfupi wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam 7 ya mwaka 2005 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo kwa sababu huu Mswada ni mdogo na nimeufahamu vizuri, mimi naomba kwa ruhusa yako nichangie Mswada huu kwa kupewa maelekezo kwa mle namuona sijapafahamu vizuri.

Mhe. Spika, Mswada huu unaohusiana na Usajili wa Mzanzibari Mkaazi tumepewa sheria mama hapa ndogo na imeeleza kuwa naomba kunukuu kwa kiingereza Mhe. Spika.

> *"Zanzibaries means a citizen of Tanzania resident in Zanzibar as defined in the Zanzibar Act No. 5 of 1985"*

Kama kiingereza changu ni kizuri nimefahamu hii inanieleza kuwa Mzanzibari maana yake ni Raia wa Tanzania anayekaa Zanzibar kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Mzanzibari Nam. 5 ya mwaka 1985.

Mhe. Spika, hapa kwanza ningeliomba nipewe ufafanuni Uzanzibari ni wa miaka mingi, karne na karne, Utanzania umeanza mwaka 1964 hivi juzi ni miaka 48 tu. leo ni sababu zipi kama tafsiri yangu ni sahihi zilizofanya kuwa Mzanzibari asiwe yoyote mwengine isipokuwa ni Mtanzania anayeishi Zanzibar. Wakati Tanzania inaikuta Zanzibari hii kwa vile ni kisiwa ina watu kutoka nchi chungumzima na nyengine si Tanganyika kabla ya Muungano.

(a) Nataka maelezo na sababu yakutosha kwa nini tuachiwe huko nyuma haki yetu tuje tupewe baada ya Muungano wa 1964.

(b) Ukenda katika Katiba ya Zanzibar hii tunayoitumia hivi sasa ukurasa wa 2 kifungu Nam. 6 Sehemu ya Kwanza kimeeleza kuwa "kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake atakuwa kama alivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Hapa ikitizama katika maneno ya pembeni. Mzanzibari kifungu Nam. 5 cha sheria Nam. 2 mwaka 2002. Huku ni mwaka 2002 na huku kwenye hii sheria ni mwaka 1985. Kwa hivyo ni ipi inayofuatwa ni hii huku katika hii karatasi tuliyopewa sasa hivi asubuhi au ni hii iliyokuwemo katika Katiba ambayo haina ufafanuzi vizuri, ufafanuzi wake hasa ni sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi ambayo hapa haipo Mzanzibari ni ipi, ili wananchi waweze kufahamu.

(c) Jengine Mheshimiwa tulikuwa na Katiba ya zamani ya mwaka 84 ambayo inaendelea kufanyiwa marekebisho mpaka hii leo. Zamani ilikuwa inaeleza kuwa "Zanzibar ni sehemu ya Jamuhuri ya Muungano" Sasa Mwenyezi Mungu katujaalia tumekwenda na Katiba ile mpaka tumerekebisha. Tukifungua ukurasa wa kwanza Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka bahari ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamuhuri ya Watu wa Zanzibar.

Sasa ikiwa Zanzibar ni nchi ni lazima inakuwa na wananchi, kwa vile wananchi wa Tanganyika wanaitwa Watanganyika, Kenya wanaitwa Wakenya, Uganda wanaitwa Wauganda kwa nini wananchi wa Zanzibar wasiwe Wazanzibari na Wazanzibari hao wakapewa vitambulisho vinavyoandikwa kitambulisho cha Zanzibar kama ilivyo hivi sasa, huu ukaazi unatoka wapi.

Kwa hili Mhe. Spika, kwa vile Zanzibar ni nchi na watu wanaoishi Zanzibar ni Wazanzibari na vile kitambulisho hakikuandikwa kuwa ni cha Zanzibari Mkaazi kimeandikwa kitambulisho cha Mzanzibari, ningeomba popote palipoongezwa ukaazi kwa kuainisha Mzanzibari kufutwe na hiki kiwe ni kitambulisho cha Mzanzibari anayeishi katika Zanzibar na Zanzibar ikiwa ni nchi yao.

Ili tunakwenda safari Mhe. Spika, na keshokutwa tunakuwa na mabadiliko tunakuwa na vitambulisho vya kitaifa na umetoa maelezo marefu umuhimu wake na umetoa maelezo marefu kwa hichi cha Zanzibar nacho. Kwa hivyo tunataka Zanzibar na Mzanzibari na kipande chake badala ya Zanzibar na kipande cha Mzanzibari Mkaazi. Mkaazi apewe yule mtu aliyekuwepo Zanzibar ambaye sio Mzanzibari kaja hapa kwa kukaa tu. Ikiwa ni mfanyabiashara, ikiwa ni vyovyote katika kazi alizonazo. Yule mwananchi wa Zanzibar kitambulisho chake kiwe ni *very clean* kitambulicho cha Zanzibar na kisiitwe kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, tunajua umuhimu wa kitambulisho na asubuhi tulikuwa na swali hapa na majibu yake yalikuja kuwa hata kusafiri ni lazima mtu awe na kitambulisho. Mengine yalikuja baadaye lakini hasa tunajua ni kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Naamini tutakapopata kitambulisho cha kitaifa cha Tanzania hakutokuwa na shida ni mtu akishakutimiza umri wa miaka 18 atapewa na sote tutapewa. Lakini masikitiko yangu makubwa ni kuona kuwa kuna shida ya Mzanzibari kupewa haki yake.

Mhe. Spika, waraka huu tuliopewa tumeelezwa kuwa kutakuwa na Mkurugenzi wa vitambulisho. Naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

*Duties of the Director of Registration subject to the provisions of this Act and directives of the Minister, the Director shall register every Zanzibari resident in Zanzibar who has attained the age of 18 years and above*

Hivyo ndivyo ilivyoelezwa. Sasa basi kitu kilichoelezwa hapa ni kuwa *and Direct of the Minister* yaani na maelekezo ya Waziri zaidi yah ii kazi yake ya kuwapa hawa wananchi vitambulisho vyao kuanzia miaka 18 na kuendelea lakini kunatiwa na maelekezo ya Waziri. Je, masheha hawa tulionao ugumu wote wa kutokubali kutoa vitambulisho kwa Wazanzibari walioanzia umri wa miaka 18 na kuendelea mpaka wengine hivi sasa wemeshapiga kura mara chungu mzima lakini hawana vitambulisho. Ni hayo maelekezo ya Mhe. Waziri yanayomfanya sheha awe mkaidi ambalo ni suala ambalo siku zote tunalitafuta. Kama kuna taarifa nyenginezo nataka nijue kwa vile hii ni haki ya Wazanzibari. Ni sababu zipi zilizowafanya Wazanzibari mpaka leo hawapewi vitambulisho vyao vya Uzanzibari wakakosa haki zao za kupiga kura, wamekoseshwa hati za kusafiria pengine na mambo mengine yatakayotokea ambayo kitambulisho ni lazima kama vile masomo na kadhalika, kwa sababu ya sheha tu kwa kusema *yes or no* kwa mtu anapokwenda kuomba.

Sasa kama Mhe. Waziri ana maelekezo labda kusema isipokuwa hivi hivi, kwa hivyo naomba tuambiwe kwa uwazi ili tujue ni wapi penye matatizo, kwa sababu hamu yangu ni kuona kila mzanzibari akawa na kipande hicho cha mzanzibari kabla ya kuja kipande cha uraia cha kitaifa ili wazanzibari tujuane.

Jengine Mhe. Spika, ambalo napenda kulieleza ni kuwa mzanzibari ana haki yake na moja katika haki yake au wajibu wake ni kuwa ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki mzanzibari. Hii ina maana ukimnyima kitambulisho ushamnyima haki zake hizo, na pia atapaswa kutekeleza wajibu na majukumu na dhamana za mzanzibari kama ilivyo kwenye katiba hii na kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Kitambulisho sisi ndio silaha yetu ya kuonekana mimi ndie mimi sie. Kwa hivyo yote hii nahimiza Mhe. Spika, kuwa suala la vitambulisho vya mzanzibari vitolewe haraka kama inavyowezekana.

La mwisho Mhe. Spika, ninaloomba kuchangia ni kuwa; hapa pana mambo kidogo naomba maelezo. Hapa Mhe. Spika, nikiangalia kifungu cha 3 (c) ukurasa wa pili wa huu mswada tunaoujadili imeandikwa shughuli ya biashara maana yake ni shughuli yoyote iliyokusudia kuzalisha faida bila ya kujali kama ina leseni au haina leseni. Hapa nilitaka nijue ni shughuli gani ya biashara ambayo haina leseni. Hilo ni moja.

Halafu chini kuna kifungu hicho hicho cha tatu kinasema mkaazi asiyekuwa mzanzibari maana yake ni mtu yoyote mbali ya mkaazi wa muda au mzanzibari mkaazi ambaye ameingia na anaishi Zanzibar kisheria ameingia kutoka wapi. Mkaazi wa muda ni yupi na huyo ambaye ameingia na anaishi Zanzibar kisheria na anaingia kutoka wapi, maana akitoka Tanzania Bara huyo ni mzanzibari kutokana na maelezo kama niliyoyaeleza juu nataka maelekezo, lakini huyu kaingia kutoka wapi mpaka akaja hapa akakaa na kadhalika.

Halafu jengine Mhe. Spika, ninaloomba kupata maelekezo ni kuwa hapa huu ukurasa 219 kifungu nambari 6 (a) sehemu ya kwanza naomba kusoma kimeeleza Mhe. Spika, kuwa kila mzanzibari, asiyekuwa mzanzibari kila mkaazi asiyekuwa mzanzibari mbali ya mkaazi wa muda anayeishi Zanzibar anatakiwa kusajili katika Ofisi ya Usajili wa mzanzibari mkaazi ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe aliyopata kibali cha ukaazi kutoka mamlaka ya uhamiaji wa Jamhuri ya Muungano. Je kuna ulazima kuwa lazima upate mamlaka ya uhamiaji kutoka Jamhuri ya Muungano ndio uweze kuishi hapa sisi hatuna chombo kilichokuwa kinahusika na mambo haya. Na nasema hivi kwa sababu itakuwa watu wanaingia tu, Jamhuri ya Muungano wakitaka watu waingie tu na hali kama ilivyo hivi sasa kama alivyoeleza Mhe. Asaa. Kwa hivyo hapa kwanza Uhamiaji wa Jamhuri ya Muungano ile mamlaka yake ya kuona anaeleta watu tu hapa naomba nipate maelekezo yake.

Na la pili kwa nini akae mpaka katika muda huo ulioelezwa yaani muda wa ndani ya miezi mitatu, miezi yote hiyo itakuwa pana shughuli gani zinafanywa mpaka ndio apewe shughuli nyengine zilizokusudiwa.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kama nilivyosema ninaloomba sana ni ufafanuzi. Ahsante.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusiana na mswada uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, niendelee kungana na wenzangu kumpongeza Mhe. Rais kwa kututeulia hawa Waheshimiwa watatu, kwa kweli uteuzi wake umesibu sana, wote watatu hawa kila ninavyowaangalia unawaona watu wapole, ukiwaangalia kwa wasifu wa nje ni watu wakarimu sana lakini kwa wasifu wa ndani kila ninapowaangalia Mwenyezi Mungu amewabariki vipaji vitatu kwa pamoja. Wana ubongo wa hekima, ulimi wa fasaha na moyo unaoweza kuhifadhi siri za Baraza na serikali yetu kama vile kaburi linavyohifadhi maiti. Jamani dogo hilo! Kwa kweli katika hili napenda nimpongeze Rais na niwapongeze hawa, ninaamini Mhe. Rais na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunatarajia utumishi ulio makini na mahiri kutoka kwa hawa. Mhe. Rais usiwe na wasiwasi watakusaidia wewe na hili Baraza kwa ujumla.

Baada ya dibaji hiyo Mheshimiwa naomba sasa moja kwa moja niende katika mswada uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu wa marekebisho ya sheria ya usajili wa mzanzibari mkaazi namba 7 ya mwaka 2005 na mambo mengine kwa kweli Mhe. Spika, imefanya haraka kuletwa hapa Barazani. Mheshimiwa huwezi kumtukana mamba kabla hujavuka mto kabisa kabisa Mheshimiwa. Leo hii tunazungumzia kutaka kuwapa wageni wasiokuwa wazanzibari vitambulisho, wakati Mhe. Spika, kuna kundi la wazanzibari hawajapata vitambulisho hili ni tatizo. Sasa mimi nadhani Waziri angeondoka nao huu mswada huu wakaenda nao huko serikalini wakaangalia utaratibu vipi tuwape wageni kwanza wakati hawa wenyeji hawana. Zaidi ya asilimia 30 ya wazanzibari ambao wameshafikisha umri hawana vitambulisho, leo tunataka kumuenzi mgeni wakati mwenyeji ana tatizo. Mimi naona jamani kwa kweli msitupotezee muda serikali, hamujawa tayari katika hili. Huwezi kumkarimu mgeni wakati mwenyeji ana matatizo, utamkarimu vipi mgeni wewe inaingia akilini kweli.

Sasa mimi nadhani serikali isitubabaishe, kama ina nia ya kuwatambua wageni basi kwanza iwatambue hawa wenyeji halafu ndio iwatambue wageni kabisa kabisa Mhe. Spika, ni tatizo. Ofisi ya Vitambulisho ina tatizo, mimi nitasema na nitaendelea kusema Ofisi ya Vitambulisho ni wabaguzi. Mhe. Spika, bado ni mapema mimi nashauri mswada urudishwe huu huu mswada tusiupitishe Barazani kwa sababu Ofisi ya Vitambulisho inatubagua. Hivi sasa Mhe. Spika, mimi Jimboni kwangu pale zaidi ya watu elfu mbili hawana vitambulisho na wameshafikia umri. Hapa nilipo nina wananchi wa Jimbo la Kwamtipura katika shehia ya sheha Machano, sheha Mbonga kuna watu 117 wenye vyeti vya kuzaliwa kwa sheha Mbonga Kwamtipura tu hapo wana vyeti vya kuzaliwa lakini wakienda kwa sheha hawapewi barua kupata vitambulisho. Waliozaliwa Kwamtipura, Muembetanga, Matemwe hapa hapa wamezaliwa 117 Mheshimiwa hawana vitambulisho. Kuna watu 46 kwa hapo sheha Mbonga wao hawana vyeti vile vile wanadai vitambulisho hawajapata huu ni mwaka zaidi wa sita wanadai tu wao hawapati.

Sasa leo mnatuletea mswada, maana yake sikutoa mfano wa Vitongoji jimbo la Wawi nimetoa hapa karibu na Ofisi hii ya Baraza la Wawakilishi Kwamtipura na majina haya hapa 117 hawa wana vyeti vya kuzaliwa hawapati vitambulisho, na 46 hawana vyeti wanadai vitambulisho hawajapata leo tunazungumzia kuwapa wageni. Kweli katika akili ya kawaida tutakuelewa vipi sisi. Tumpe mgeni mwenyeji, mimi siungi mkono mswada huu.

Nadhani Mhe. Spika, katika hili yafanyike mambo yafuatayo. Aidha wale wote wanostahiki tuwape vitambulisho hivi ambavyo vimeshatoka zamani, na wale waliopewa ambao hawastahiki kupewa kuna jopo la wananchi ambao hawastahiki kupewa vitambulisho wamepewa wanyan'ganywe kwanza halafu waje wapewe hivyo

tutakavyovipitisha vya wageni. Lakini haiwezekani Mmasai hapa awe na kitambulisho Mtumbatu na Mpemba hapati inasikitisha ni ubaguzi, na huu mswada bado wakati wake, na ikiwa mnafanya ukaidi serikali basi mimi naomba jambo mtusikilize. Hawa watu 117 na wale 2000 na wengine kadhaa wa kadhaa ambao hawana vitambulisho wazanzibari waliozaliwa hapa basi naomba tuufute uzanzibari wao na tuwatafutie nchi ya kukaa, la mwanzo hilo.

Kwa sababu inasikitisha, tuufute uzanzibari wa watu hawa ambao hatutaki kuwapa vitambulisho tuufute, halafu tuwatafutie nchi wakakae. Lakini siku zote hapa tuje tukipiga kelele vitambulisho vitambulisho, kama mta-*refer* hansard ya Baraza lililopita Mhe. Mshimba alisema kwamba mpaka Wamasai, Wanyaruwanda wamepewa vitambulisho huku Wamatemwe, Wapemba, Wamakunduchi wazanzibari halisi wazawa hatupewi. Na ukija hapa Waziri anakubabaisha hivi aa tutoke tutakwenda hivi siku ya pili mambo yamefifia.

Mhe. Spika, mswada huu bado wakati wake na uletwe baada ya kuwanyang'anya wale wageni vitambulisho na waliokuwa hawastahiki wapewe. Mhe. Spika, sifa za kupata vitambulisho tulizoelezwa ni tatu. Awe mzanzibari, awe mkaazi, awe mwenye umri usiopungua miaka 18. Sasa leo unakwenda pale kudai kitambulisho baba yako aliyekuzaa ana tangu kitambulisho alicho-*sign* Mhe. Said Washoto, sisi tunavyo vile alivyo-*sign* Mhe. Said Washoto tunavyo, na watoto wetu tumewazaa hapa hapa wanatoka migongoni mwa Afro Shirazi, waasisi wa nchi hii watoto wao wananyimwa. Leo mtoto anakwenda na kipande cha baba yake alichopewa tangu 1965 na Mhe. Said Washoto anaambiwa yeye si mzanzibari. Kazaliwa hapa hapa baba yake anacho kitambulisho alichopewa na Said Washoto, yeye anaambiwa si mzanzibari. Hii ni *biasness* anakuja Oletiman kutoka wapi kule akija unamuona anapewa kitambulisho cha mzanzibari mkaazi, ni mmasai kutoka wapi yeye anapewa wewe unashindwa. Aibu ni kufanywa watumwa katika nchi yetu. Twende kwenye katiba ya nchi Mhe. Spika, twende katika ibara ya 6 kifungu kidogo cha pili cha katiba.

Naomba kwa heshima na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Spika, uniruhusu kukinukuu. Kifungu hiki kinasema kwamba hii sehemu ya pili ya katiba hii mzanzibari kifungu cha tano cha sheria namba 2 ya mwaka 2002. Kila mzanzibari kwa misingi ya katiba hii ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki mzanzibari, na akapaswa kutekeleza wajibu, majukumu, dhamana za mzanzibari kama ilivyo kwenye katiba hii kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Yaani mzanzibari ana haki ya kufaidi fursa hii ni haki yake ya kikatiba, leo Mheshimiwa kutokana na kunyimwa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi tena mna-*violate* katiba unamnyima mtu kwa ku-*violate* katiba ya nchi unatunyima fursa. Watoto wetu wanataka kwenda kusoma wanataka kupata mkopo wa elimu ya juu hawapewi kwa sababu hawana vitambulisho vya mzanzibari mkaazi. Watoto wetu Mheshimiwa hivi sasa hawapati ajira kwa sababu hawa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi, anakuja kuajiriwa mmasai, mnyamwezi na mmakonde hapa, *shame!* Aibu tunafanywa watumwa katika nchi yetu wenyewe.

Mhe. Spika, lazima tuseme msi-*create* mazingira ya kutufanya watumwa we *are not slaves* kwa mujibu wa Mwalim Nyerere Rais wa Jamhuri ya Muungano alisema kwamba kuna utumwa wa aina mbili. Kuna utumwa wa bwana na mtwana *slave and lord*. Huu wa kwanza, wa pili kuna utumwa wa khofu, *this is a slave of fear* kwa mujibu wa yeye *slave of fear is the most worst slavery in the world*. Utumwa wa khofu ni utumwa mbaya sana katika ulimwengu hii kwa mujibu alisema Lenin kasema na Mwalim Nyerere.

Sasa mimi ninawaambia wazanzibari wote naomba mnisikilize hapa leo, haki haiwezi kupatikana katika kisahani cha chai kama inavyopatikana halua au tende, haki lazima idaiwe. Hamuwezi kufanywa watumwa wazanzibari katika nchi yenu kwa kunyimwa vitambulisho vya mzanzibari na hatimaye kukosa ajira, na kukosa fursa zote za nchi hii wakapewa wageni. Tumedai tumepiga makelele, Ofisi ya Vitambulisho mimi nimefuatilia sana tangu 1999 ninazungushwa hivi nikizungushwa hivi, lazima tuende kwa Rais sasa. Kwa hivyo ninawaomba wote wazanzibari ambao hawana vitambulisho, ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokotea zizini kusaidiwa. Na zizi pekee katika nchi hii ni Ikulu ya Zanzibar. Jitayarisheni mimi nitaongoza maandamano kuelekea kwa Rais kudai vitambulisho, kwa sababu Waziri hataki kutupa vitambulisho hivi.

Baada ya maelezo hayo siungi mkono hoja.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa kupata fursa hii kuweza kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, nianze kwanza kabisa kuishukuru serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa umahiri wake, kwa usikivu wake na kwa utendaji wake katika kuwatendea haki wananchi wa nchi hii. Lakini pia Mhe. Spika, niwashukuru ndugu zangu wa Idara ya Vitambulisho kupitia Mkurugenzi wetu ambaye yuko juu hapo, kwa uadilifu

wake na umahiri wake, na ukweli katika majukumu yake ya kazi ya kila siku, ninamuomba Mwenyezi Mungu amsaidie katika ufanisi wa kazi zake.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya kusimamia viongozi wa kitaifa, na kama ilivyo kawaida kwa mujibu wa kanuni zako, mswada kabla ya kuja Barazani basi unatakiwa upitiwe na Kamati katika kuona hali halisi ya ule mswada ulivyo, kupata ushauri kwa watendaji lakini kwa mara ya kwanza Mhe. Spika, kamati yangu au kamati yetu, imeweza kuwashirikisha wadau wote wa vyama vyote kutoa maoni yao katika suala zima la mswada huu wa vitambulisho vya mkaazi vya mzanzibari.

Mhe. Spika, nathubutu kusema kwamba tulikuwa tuna viongozi wa CUF, tulikuwa tuna viongozi wa TADEA, tuna viongozi wa CCM, tuna viongozi wa NRA, katika kuona kwamba haki katika nchi hii inatendeka na kuondosha zile dhana za wasiwasi katika suala zima la mswada huu. Nawashukuru sana viongozi wa vyama vyote, nawashukuru sana wadau wote, tumeweza kutoa mawazo yetu, hatimae leo mswada huu uko mbele ya Baraza lako tukufu na tunauchangia.

Mhe. Spika, mimi huwa napata mashaka sana, napata mashaka na baadhi ya viongozi wenzangu tunapoanza kuleta dhana ya kubaguana, dhana ambayo kwa kweli hatutowatendea haki watu wengine kuanza kuwazungumza Wamakonde, kuanza kuwazungumza Wanyamwezi kuanza kuwazungumza Wamasai. Mswada unamzungumza mzanzibari Mhe. Spika, hana kabila, mzanzibari si muhindi, mzanzibari si mwarabu, mzanzibari si mmakonde. Mzanzibari ni yule mtu ambaye ana haki na fursa ambayo inamtambulisha kwamba yeye ni mzanzibari.

Mhe. Spika, mimi ni mmakonde, mmakonde ambaye kwetu ninakuelewa, kwetu ninakufahamu na wazazi wangu wapo, ni mmakonde wa kijiji cha Mhesi, Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma. Sasa na mimi kama sina haki kama mmakonde basi Mhe. Spika, nasema tena kwamba hatuwatendei haki watu kuwachagua kwa makabila yao. Tutizame sheria inasemaje katika suala zima la uzanzibari.

Mhe. Spika, mimi niishukuru sana serikali, sisi ndio tunaopiga kelele kwamba watu hawatendewi haki, kama serikali imekaa ikaona kwamba kweli kuna tatizo ikaamua serikali kupitia wizara yake kuleta mswada kuondosha tatizo, tatizo liko wapi Mhe. Spika. Tunayozungumza ni mapungufu, tupange sheria nzuri ambayo itaondosha matatizo yetu, itaondosha dhana zetu. Mhe. Spika, bado kuna wenzetu hawajaiamini serikali na hawataki kufuata sheria. Mhe. Spika, kuna kesi iko mahkamani ya uchaguzi wa Bububu, lakini kama utaangalia CD aibu kwa viongozi wako wa serikali Waziri mzima anasimama anamdai mtu kitambulisho cha kupiga kura wakati Tume ipo, haya ni matatizo. Kama kuna vyombo na taasisi za serikali zimepewa mamlaka zina sheria zake, kama kuna tatizo Mhe. Spika, kama kuna mwananchi hakupewa kitambulisho fursa zipo. Sehemu za kwenda kwa ajili ya sheria zipo aende akatoe *evidence* yake, mimi sikupewa kwa sababu moja, mbili, tatu sheria itafuata mkondo wake. Na kama mtu amepewa kitambulisho pasipo utaratibu sheria zipo na kuna watu wako mahkamani sasa hivi, wale ambao wamepata vitambulisho hawakufuata utaratibu kwa udanganyifu, sasa tatizo liko wapi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi naomba niendelee kidogo niseme kwamba naishukuru sana kwa mara nyengine serikali sikivu, serikali inayojali wananchi wake, serikali isiyojali mivutano wala migongano kwa wananchi wake, serikali inayohitaji amani na utulivu katika nchi hii. Mhe. Spika, moja ya mapungufu ambayo tuliyaona ndio yale yaliyozungumzwa katika mswada huu kwamba kweli kuna wageni wanaingia pasi na kufuata utaratibu, wengine wanaingia katika vituo vya kawaida, lakini wengine wanaingia katika njia za panya. Ndio maana tukaandaa mswada huu kumtambua kila mwananchi wa nchi hii awe mgeni, awe mzaliwa awe wa aina yoyote na tumuelewe anafika hapa kama ni mgeni kwa shughuli gani na maeneo gani, ili kuondosha yale matatizo ambayo tunayazungumzia hapa na matatizo ya watu ambao wanakuja hawafanyi kazi za uhalali, hao watu ambao tuna mashaka nao katika shughuli za ujambazi kila mtu tunamtaka ajulikane juu chini katika hali halisi, na ndio maana tukaleta mswada huu. Kama serikali haina nia njema Mheshimiwa kama tunataka tulete majambazi tusingeleta, lakini tumeleta ili tusaidiane kuwatambua hao watu na fursa zao.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na masikitiko sana kwa wenzangu ambao wanaendekeza jazba zaidi mbele kuliko kufuata sheria, ambao hawana ustahmilivu katika nafsi zao, lakini nina imani kwamba tutafikia pahala tutafahamu nini tutakihitaji na nini tunakitaka ili Zanzibar yetu iwe huru, iwe haki.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, nami naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii kuweza kufika hapa. Pili nikushukuru Mhe. Spika, nami kunipa nafasi alau niweze kutoa mchango kuhusu mswada huu muhimu, unaohusiana na marekebisho ya sheria ya Usajili ya Mzanzibari Mkaazi, sheria namba 7 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kutambua kwamba leo tarehe 16/10 ni siku ya chakula duniani. Kwa kuwa ni siku ya chakula duniani na kwa kuwa Mhe. Rais amefanya uteuzi wa Naibu Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, ambayo hiyo ndio vyakula uteuzi huo umesibu, kwa kuwa umekuja katika siku ya kuadhimisha siku ya chakula duniani. Naomba nimpongeze Rais kwa uteuzi, lakini pia niwapongeze wale wote walioteuliwa kushika nafasi hizo mbali mbali za kutumikia nchi yetu. Kwa upande wetu Wawakilishi tunaahidi kwamba tutawapa kila aina ya ushirikiano ili watimize wajibu wao kama vile ulivyokusudiwa.

Sasa baada ya dibaji hiyo naomba niingie kwenye hoja ambayo ni marekebisho ya sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi ya namba 7 ya mwaka 2005, ambapo katika suala hili Mhe. Spika, tunakuwa tunazungumzia juu ya suala la kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, hakuna shaka kama Zanzibar kama nchi ambayo imetambuliwa Zanzibar kama nchi kwenye Katiba yetu ya Zanzibar katika kifungu kile cha mwanzoni kimeitaja Zanzibar kama nchi. Na kwa kuwa ni nchi basi kuna wananchi, wapo wazanzibari katika nchi ya Zanzibar. Kwa hivyo, kama Wazanzibari tuna kila sababu ya kutambuliwa na kujitambulisha na kitu kinachoweza kututambua na kujitambulisha ni hiki kitambulisho ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar. Kitambulisho kina umuhimu sana kwa sababu hiki ndicho kinachoweza kumtambulisha nani Mzanzibari na nani ambaye si Mzanzibari, haidhuru kama nchini kutakuwa kuna watu wengi wanaingia na kutoka.

Kitambulisho Mhe. Spika, tulivyoanza kukitoa mwanzo kilionekana zaidi kilikuwa kina sura ya kisiasa, lakini katika maisha ya sasa kitambulisho kinaonekana kwamba ni kila kitu. Kitambulisho kimechukua umuhimu wa lile lengo lake lililokusudiwa kwamba kila kitu ni kitambulisho na katika hili Mhe. Spika, tunapaswa kama serikali, tunapaswa kama Baraza la Wawakilishi na tunapaswa kama wananchi tuone umuhimu wa vitambulisho kwa watu wetu na tunapaswa tuondokane na zile fikra na dhamira tulizokuwanazo awali wakati kitambulisho hiki kinaanzishwa. Sasa kama ukiwa huna kitambulisho huwezi ukapata huduma yoyote ya kijamii, tulishuhudia Naibu waziri asubuhi akijibu swali namna ambavyo watu wanapata matatizo ya kukata hata tiketi za meli kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Katika hilo Mhe. Spika, tuna *categories* mbili Zanzibar, wapo wazanzibari ambao ni Wazanzibari kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa maumbile, lakini vile vile wapo wananchi ambao si Wazanzibari ambao ni wakaazi wa ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika makundi yote mawili na hasa hili kundi moja la *indigenous* Wazanzibari wenyewe nikisema Wazanzibari wenyewe wanafahamika ni wepi ni wale tunaowaongoza katika majmbo yetu. Kwa muda mrefu kumekuwa kuna malalamiko na Mhe. Spika, ni Baraza lako hili mara nyingi linapokuja suala hili tunakuwa tunashuhudia namna wawakilishi wa wananachi wanavyoleta vilio kuiambia serikali. Ni dhahiri kwamba kuna Wazanzibari wengi ambao ni Wazanzibari kwa namna moja au nyengine wananyimwa kupata fursa yao hii ambayo mimi nasema ni ya msingi kuliko kitu chengine chochote. Mara nyingi tumefika hadi kutoa hapa majina ya watu pamoja na *list* zao kwamba hawa ni Wazanzibari wanaokaa pahali fulani na fulani hawamo. Mimi sipingi kwamba yeyote apewe kitambulisho mimi nakubali kwamba yeyote ajae apewe kitambulisho, yeyote ajae mpeni kitambulisho tu, lakini sitokubali hata siku moja kuona mtu ni mzaliwa wa ardhi hii kuwa yeye akanyimwa kitambulisho akapewa mtu mwengine yoyote hilo halikubaliki.

Narudia Mhe. Spika, mimi niko radhi mtu yeyote anayekuja Zanzibar apewe kitambulisho yeyote, akitoka Bara, Kenya, Uganda apewe tu, lakini sitoridhika kwanza kupewa yeye akanyimwa mtu ambaye kitovu chake kimezikwa ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba, hilo halikubaliki.

Leo kama Wawakilishi wa wananchi hatuwezi kulitetea hilo ambao waliotufanya kutuleta katika ukumbi huu ndio hao miongoni mwao wanaoleta kilio uhalali wetu utakuwa uko wapi. Kwa sababu miongoni mwao waliomo katika majimbo yetu ndio hawa ambao wanasababu.

Mhe. Salehe Nassor Juma yeye anatoka katika Jimbo la Vitongoji lakini sasa hivi kazungumzia matatizo yaliyomo ndani ya jimbo moja katika mji huu wa Unguja. Sasa sidhani kama tutakuwa tunafanya haki, nadhani tufanye haki kwa kutetea wengine lakini hawa waliopo hapa ndio wa msingi lazima tuwatetee wao kwanza kabla ya kuwatetea wengine.

Sasa Mhe. Spika, tunarudia kusema kwamba kuna wananchi wengi wazaliwa wa visiwa vya Unguja na Pemba Wazanzibari kwa ufupi bado wana matatizo, wananyimwa haki yao hii ya vitambulisho. Na serikali ambayo mara nyingi humwambia Mhe. Waziri kwamba kuna tatizo, sasa nilidhani kwa serikali iliyo makini na sikivu hili ni jambo dogo sana katika kitu kidogo kushughulikiwa na serikali hili ni moja. Tangu kipindi ambacho tulikuwa tunapiga kelele na hadi leo kwa vyovyote mimi nilidhani kwa udogo wa jambo hili ni kitu cha siku mbili au wiki moja, mwezi mmoja au kitu cha mwaka mmoja kulimaliza tatizo hili, lakini inaonekana kwa makusudi serikali haitaki kulitekeleza suala hili au haitaki kulipatia ufumbuzi tatizo hili. Kama hivyo ndivyo, nini azma ya serikali?

Mhe. Spika, ikiwa serikali wananchi wao wanapiga kelele mwananchi wa Nungwi, Mtumbatu wa wapi, mtu wa Kiwani hamtaki kuwapatia vitambulisho mnachotegemea ni nini? Mimi nasema hili ni tatizo na kwa vyovyote Mhe. Spika, mimi leo nilidhani kwamba kuletwa kwa mswada huu itakuwa ni sehemu ya kujibu kilio, nilidhani sana kwamba matatizo yaliyoko makubwa ni namna ya kupatikana kitambulisho hicho hilo ndio tatizo letu, kwamba sheria imeweka masharti magumu kutekelezeka katika kuwapatia watu vitambulisho.

Hivi sasa Mhe. Spika, katika nchi yetu kuna zoezi la utoaji wa vitambulisho vya taifa, lakini utoaji wa vitambulisho vya taifa umekuwa vina utaratibu mzuri mno, Mtanzania yeyote pahala popote alipo anapata kitambulisho cha taifa, na masharti yake ni rahisi mno na yenye kutekelezeka kwa urahisi. Unapokwenda na cheti cha kuzaliwa unapata kitambulisho cha taifa, unapokwenda na *passport* unapata kitambulisho cha taifa, unapokwenda na cheti cha skuli unapata kitambulisho hicho, maana yake sheria imesema mtu yeyote aliyefikia umri wa miaka 18 kinachoweza ku-*justify* hiyo maana yake ni cheti cha kuzaliwa na vitu vyengine. Kwa hivyo, kitambulisho cha taifa kimeweka masharti mazuri, masharti rahisi na masharti rafiki yanayomuwezesha kila Mtanzania popote alipo apate kitambulisho bila ya bughudha yoyote, vyereje leo kitambulisho cha Zanzibar kiwekewe masharti yote haya kuna nini ndani yake?

Narudia kwamba kitambulisho cha taifa unapokuwa na cheti cha skuli unapata kitambulisho, unapokuwa na leseni ya udereva unapata, unapokuwa na cheti cha kuzaliwa unapata kitambulisho, unapokuwa na *passport* unapata na kitu chengine chochote ambacho kinaweza kukutambulisha tu kwamba wewe ni nani basi hicho kinatosha kupata kitambulisho. Hili ndilo kero, hiki ndicho kitu ambacho kinaweza kikavuruga amani ya nchi yetu. Sasa ikiwa Wawakilishi tunahubiri amani mimi nadhani tufanye kila kitu ambacho kitaweza kuepusha wananchi kutoa manung'uniko kwa serikali yao, wananchi kutoa manung'uniko kokote kule yaliko, na kwa vyovyote mimi leo nilidhani kwamba sheria hii itakuja na jibu.

Juzi tulikuwa katika mahojiano Waziri katika Ofisi ya Pili alinambia kwamba serikali inakuja na jibu, sasa mimi nilitegemea kuwa pamoja na kwamba sheria hii inataka wale watu ambao wapo Zanzibari lakini si Wazanzibari kupewa vitambulisho mimi hilo naunga mkono narudia kwa mara nyengine, lakini na wale Wazanzibari wa kuzaliwa kwa lile tatizo lililojitokeza kwenye sheria hii mama nalo litapatiwa ufumbuzi. Kadiri nilivyoangalia kwamba sheria hii haikuja na ufumbuzi wa lile tatizo tunalolizungumzia la kama pana pahala pana ufumbuzi naomba baadae Mhe. Waziri atakapokuja kwa namna ya kurahisisha kwa sababu hilo ndilo tatizo, kurahisisha watu kupata vitambulisho bila ya matatizo naomba anambie ni kifungu gani ambacho kimekuja katika marekebisho ya mswada huu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kadiri ninavyoona kwamba mswada huu umeelekea upande mmoja wa kuwapa haki watu waliopo Zanzibar ambao si Wazanzibari lakini haukuelekea kabisa kabisa katika kutatua tatizo. Narudia tena kama hivyo ndivyo basi naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze na hivyo mimi sikubaliani naye. Hili ni jambo zito na kwa kuwa ni jambo zito kwa kweli mimi sitoweza kuunga mkono Mswada wa Sheria ambao haukuleta majibu na ambao hauwezi kuwapa haki wananchi.

Mhe. Spika, siku ambayo serikali watakuja na mswada mzuri, mswada utakaompa kila haki Mzanzibari popote alipo mimi hilo kwa kweli nakubalianana lo, nakubaliana nalo kwa msingi kwamba sisi Wazanzibari jamani tufikeni pahala tujenge utamaduni wa kutibu chanzo cha matatizo. Maana yake leo Wazanzibari tumekuwa mabingwa wa kulalamikia matokeo, hili ndilo tatizo letu, mara nyingi sana tunakuwa tunalalamikia matokeo lakini

tunapozungumzia chanzo cha matatizo jamani ondosheni hili, ondosheni hili wakati huo kila mmoja hufunga masikio, lakini matokeo yanapokuja kila mmoja sasa huja kulaani na vitu vyengine kitu ambacho kwa kweli ni *very wrong* kwa watu ambao wana akili, watu ambao ni wastaarabu hukimbilia kwenye kutibu chanzo cha matatizo.

Mimi sitaki kuzungumzia uchaguzi wa Bububu kwa sababu uchaguzi wa Bububu kila mmoja anaujua na nini kilichotokea, lakini nataka kuzungumzia hili tatizo ambalo nina hofu huenda baadae likaleta sintofahamu katika nchi yetu, tatizo la Wazanzibari kukoseshwa vitambulisho vya ukaazi nadhani kama hatukulipatia jibu basi huenda siku moja nchi yetu ikapata matatizo kutokana na tatizo hili.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ni mpaka pale waziri atakapokuja kunieleza kwamba ni wapi na wapi mswada huu umejibu matatizo ya msingi ya wananchi ndipo hapo nitaunga mkono mswada huu. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Panya Ali Abdallah:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amtujaalia uhai wake mchana huu tukaweza kuweko hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, ambaye umenipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia machache katika mswada huu. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea marekebisho haya ya mswada wa sheria hii ambao utaifanya iweze kuwa bora na kila Mzanzibari aweze kupata haki yake.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu naomba niende katika madhumuni na sababu ya usajili wa Wazanzibari Wakaazi chini ya sheria mama ulikuwa na dhamira ya kuweka utaratibu bora wa utambuzi wa Mzanzibari.

Mhe. Spika, mimi kwanza nichukue fursa hii kuishukuru sana serikali kwa kazi ngumu ambayo imeifanya lakini leo inaonekana kazi hiyo kuwa nzuri kwa sababu ya kuweza kuhamasisha Wazanzibari juu ya umuhimu wa kitambulisho cha Mzanzibari na leo hii kinapigiwa kelele kwa kuonekana umuhimu wake kweli kitambulisho kina umuhimu mkubwa. Mhe. Spika, naipongeza serikali kwa juhudi yake hiyo.

Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kina umuhimu mkubwa maana ya kusema maneno hayo kitambulisho hiki asili yake mwanzo kilipoanza kutayarishwa serikali ilianza kwa juhudi kubwa za kutuhamasisha wananchi wake juu ya umuhimu wa kitambulisho hiki, lakini pamoja na lawama ambazo zinatupiwa serikali mimi nasema na sisi wenyewe pia wakati mwengine tujilaumu. Kwa nini nasema hayo Mhe. Spika, vitambulisho wa Mzanzibari Mkaazi vilivyotoka mwanzo sisi wengine ambao tulikimbilia kuvichukua tulichukua bure bila ya malipo yoyote na havikuwa na utatatnishi wowote. Lakini sisi wenyewe wananchi tuna tabia serikali inapotoa tamko au agizo lake tuna tabia ya kubeza au kudharau kuona hakuna manufaa yoyote.

Mhe. Spika, tuliibeza kauli hiyo na kuna hata viongozi hasa walithubutu kubeza hiyo kauli na vitambulisho vilionekana vikigaragara siku za mwanzo kama vile havina kazi yoyote, hiyo ilikuwa si tabia nzuri. Kwa kuwa kitambulisho ni muhimu kwetu mimi nasema bado kama viongozi tusichukue jazba, bado elimu kubwa inahitajika kwa wananchi wetu tuweze kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Tukichukua lawama tu bado kuna wananchi tunavyofahamu sisi na wanavyofahamu wao ni tofauti, nasema hilo kwa mfano ambao umepita hivi karibuni.

Hivi karibuni tulikuwa na uandikishwaji wa sensa ambapo wananchi wetu tunajua walikumbana na wimbi kubwa la kuwa wanakataa uandikishwaji ule na ni jambo muhimu tu, lakini tulilibeza na kudharau na sisi viongozi tunapaswa tuchukue juhudi ya kuelimisha wananchi wetu ili wajue umuhimu wa jambo lile. Sasa basi, itakapotokea kitambulisho hicho cha Mtanzania ndio sasa hivi serikali inachukua juhudi vile vile ya kuhamasisha tena kwamba jamani pamoja na kwamba tuwe na kitambulisho cha Mzanzibari lakini kwa Wazanzibari bado tunatakiwa tuwe na kitambulisho cha Mtanzania ambacho hicho ndio Utaifa wetu. Bado wananchi wataendelea kubeza kwa kuwa wanaona hawajui umuhimu wake, mtu hatoibuka mpaka siku ile ambapo ana shida ya kuona tayari kile kitambulisho kinahitajika na yeye ana shida ya kutatua tatizo lake kwa kupitia kitambulisho kile ndipo mtu analeta lawama hiyo haitasaidia.

Hivi sasa mimi ushauri wangu bado ni mapema vitambulisho bado vipo na kama sifa unazo huna sababu ya kunyimwa kitambulisho. Mhe. Spika, mimi naomba kama viongozi tuchukue juhudi za makusudi tuweze kuwaelimisha wananchi wetu wakati ndio huu vitambulisho vipo na hakuna sababu ya mtu kunyimwa haki yake. Hivyo bado elimu hiyo tuitoe kwa wananchi wetu na vitambulisho vyengine vimeshakuwa tayari vya Mtanzania

basi ni lazima tuhamasishe wananchi wetu ili waweze kuvipata vitambulisho vile viwe kwa manufaa ya kutatulia matatizo yetu ambayo tunakumbana nayo kila siku.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano mdogo tu wa kwangu mwenyewe ambapo juu ya umuhimu wa kuwa na kitambulisho. Mhe. Spika, zamani wazee wetu walikuwa wana kitambulisho kile kilichokuwa kinaitwa pasi ya uraia ambayo ilikuwa pasi hiyo huwezi kupita katika kituo cha polisi kama huna. Mhe. Spika, mimi nilikuwa naishi kijijini lakini kwa bahati ilikuwa bibi yangu kila inapokaribia sikukuu ananileta mjini nije kula sikukuu mjini. Kwa bahati siku hiyo zamani gari zilikuwa tabu kidogo, tukakaa mpaka saa sita tunasubiri gari ikawa haijatokea kwa bahati bibi yangu akanambia basi mimi nakwenda Mfenesini kutafuta mahitaji baadae tutarudi nyumbani, mimi nikaona haijawahi kutokea kula sikukuu shamba.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri likatokea gari moja la mizigo nikalisimamisha kwa jazba ile ya utoto ya kuona mimi nina hamu ya kwenda mjini hata nikiwa bibi yangu sijamwambia, nikapanda lile gari na kwa bahati kile kitambulisho chake kilikuwemo katika mkoba wangu mimi ambao ameniwekea nguo zangu, nikaenda tukafika mpaka mjini. Sasa kwa bahati anakuja bibi yangu anaambiwa mjukuu wako kasha panda gari kasha kwenda mjini na yeye alikuwa ananipeleka kwa sababu anaona labda sikuelewi vizuri nisije nikapotea, sasa akasema ishakuwa kazi kwa sababu anakutaka mjini anifatilie lakini hawezi kuja kwa sababu ile pasi ya uraia ninayo mimi imo ndani ya mkoba.

Sasa huo ni umuhimu wa kitambulisho na kuwa serikali inapotoa agizo lazima wananchi tuweze kulifuata ni muhimu. Pasi ya uraia ilikuwa huendi pahala au huwezi kuvuka kituo kama huna pasi ile. Sasa na kitambulisho cha Mzanzibari na cha Mtanzania kina umuhimu mkubwa tunapobeza tunajikosesha sisi wenyewe. Kwa hivyo, wito wangu mimi kama kiongozi nitachukua jukumu hili kuhamasisha watu katika Mkoa wangu kuwa jamani kitambulisho kina umuhimu na tukitumie na kupitia chombo hiki ndio tayari nahimiza ambapo watu wetu wengi wana utamaduni sasa hivi wa kuangalia televisheni. Kwa hivyo, mimi natoa wito huu vitambulisho ni muhimu kila mwenye sifa anastahiki kupata kitambulisho hicho lakini na sisi viongozi ambao tumo humu tujitahidi kupunguza lawama ili twende katika elimu ya kuelimisha wananchi wetu waweze kujipatia vitambulisho hivi na waondokane na yale matatizo yatayowapata watakapokuwa hawana vitambulisho.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe aligusia hapa kuhusu masharti kwamba yamekuwa mazito, lakini mimi kwa upande wangu nasema na tutakapoyarahisisha sana pia kuna wasiwasi wa kuja mchele ukazidi chuwa. Kwa kila mmoja ataona ni njia rahisi tu mana ukiwa na kitu hiki tu tayari umeshaingia ni bora kuwa na masharti ambayo yatawachuja na kuwapata wale Wazanzibari wenye uhalisia mzuri wa Uzanzibari.

Mhe. Spika, mimi  baada ya kusema hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono mswada huu tuweze kuuchangia na kuupitisha kwa nia njema ya kutatua matatizo ya wananchi wetu. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika suala zima la mswada tulionao hivi sasa wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, katika mswada huu kitu kinachojitokeza mswada mzima ni suala la ufafanuzi hakuna jengine, ni ufafanuzi tu wa huu mswada uliokuwa wa zamani. Kwa hivyo, hapa tumetajiwa kitu ambacho kinamsaidia huyu msajili ambacho tunakiita *biometric information*. Hii *biometric information* ni taarifa ya ki *biometric*, hiki ni kifaa ambacho kinaweza kusaidia kutoa taarifa si kitu kibaya kuwa na chombo kama hicho cha kuweza kutoa taarifa. Chombo hiki mbali ya kutoa taarifa lakini vile vile kina utaratibu wa kiteknolojia na vile vile wa kuweza kutoa vipimo pamoja na uchunguzi. Sawa tunakubali chombo hiki kipo, lakini sasa wakati tunapewa kifaa hiki ambacho ni muhimu sana *biometric informationa* ambayo inatoa taarifa kwa mtu yoyote lakini sasa inategemea, wewe unapotia ile taarifa unamtilia nani taarifa ile? Ni mtu ambaye anahusika au kila yule anayehusika na asiyehusika, kifaa hicho hicho kimoja kinaweza kutoa taarifa mbili kwa mtu anayehusika kwa kutiliwa taarifa zile au kwa mtu ambaye atakuwa katika kifaa kile asiyehusika pia yote yanaweza kutendeka.

Mbali ya hayo Mhe. Spika, tumeelezwa katika ufafanuzi mwengine kwamba kuna tafsiri ya shughuli za kibiashara, yaani biashara hii ina mastaajabu makubwa sana sijapata kusikia ni mara yangu ya mwanzo kuisikia aina hii ya biashara. Biashara ambayo ndani yake inazalisha faida bila ya kujali kama ina leseni ama haina leseni biashara ile na

huku faida inatolewa lakini bila kujali kama ina leseni au haina na kama inafanywa na taasisi za kibiashara au vyenginevyo. Sasa mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri katika suala hili la biashara ambayo ndani yake inatia faida iliyokuwa haitakiwi leseni kuwemo ikiwa ni taasisi au vyenginevyo vyovyote akija hapa angalau atupe taarifa hiyo mimi sijaifahamu bado atueleze aina gani ya biashara ambayo haina leseni.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la ufafanuzi wa Mzanzibari Mkaazi, hapa tumeambiwa kwamba asiyekuwa Mzanzibari tunajua huyu kwa lugha nyengine atakuwa ni *Non Zanzibari Resident*, huyu si mkaazi. Halafu katika wale watu wengine ambao wanakuja kuna wakaazi wengine ambao wanakuja kuishi Zanzibar kwa muda mfupi hawa tutakuwa tunawaida *Temporary Resident* yaani wanaishi kwa muda mfupi halafu wanaondoka na yule ambaye ni Mzanzibari kamili atakuwa ni *Zanzibari Resident*, huyu ambaye anakubalika. Hayo yote Mhe. Spika, tumeyafahamu na tumeyaona, lakini makusudio hasa na kiini cha zogo la mswada huu bado ufafanuzi wake haujaletewa. Mimi ningelishauri katika mswada huu kwa kuwa mswada huu unaanza kupigiwa kelele tangu kipindi cha nyuma mswada huu uliingizwa mwaka 2005.

Mimi nataka niseme mwaka 2005 na mimi nimo ndani ya Baraza hili la Wawakilishi na mswada huu ulikuja wakati ule tuko baina ya *CUF* na CCM ndani ya Baraza hili sisi *CUF* tuka-*abstain* kwenye mswada huu, hatukutoka nje lakini tuli-*abstain.* Kwa sababu maelezo katika mswada huu hayakwenda sambamba na wananchi yanakwenda kinyume, yaani unawakwaza wananchi hauwapi haki sisi ndio tuka-*absatin* mswada huu kuonesha kuwa hatukuridhika tangu kipindi hicho ulipokuja hatukuwa radhi nao na ndio maana tuka-*abstain*, hatukunyanyua mikono tulibakia hivyo hivyo, lakini walio wengi ndio wakashinda na mmeshinda. Tunapoulizana huko wanapokuja wakubwa kutuuliza si mmeupitisha nyinyi wenyewe, ndio tumeupitisha lakini wengine hatukuupitisha hatukuwa radhi kwenye mswada huu kwa sababu ulikuwa unakwenda dhidi ya wananchi.

Lakini jengine Mhe. Spika, mimi nataka nizungumze kama kweli sisi Wazanzibari tunafuata nyayo za Rais wetu wa Zamani Marehemu Abeid Amani Karume kwa nini leo tunapinga mambo yake mazuri aliyokuwanayo miaka hiyo ya nyuma. Mhe. Karume kipindi hicho cha miaka ya zamani alitoa vitambulisho kwa Unguja vitambulisho vya aina mbili, alitoa kitambulisho cha raia wa Unguja rangi ya kijani na akatoa kitambulisho kingine cha Mkaazi wa Unguja rangi ya manjano. Mzee Karume kwani hakuwa na akili yeye wakati huo, hakujua hii faida yake? Mimi nilihisi kwamba Mzee Karume aliyoyafanya akatoa akabainisha kwa Wazanzibari kwamba hawa ni raia na hawa sio raia wanakuja kwa kuishi kwa muda halafu wanaondoka.

Halafu niseme kitu chengine Mhe. Spika, sisi hapa zamani tulikuwa naye *British Resident*, nini maana yake *British Resident*, maana yake ni mkaazi kwa sababu yeye ni mtu mgeni amekuja kuhamia katika nchi kwa muda halafu ataondoka atakwenda kwao, ndio maana yake resident. Lakini sisi watu wa Zanzibar si wakaazi, sisi ni raia wa Zanzibar. Kwa hivyo tunastahiki uraia, tuitwe raia wa Zanzibar na aliyekuwa si raia wa Zanzibar apewe huo ukaazi kama alivyofanya Marehemu Mzee Karume.

Kwa nini tunapinga mawazo yake. Hii imekuja mwaka 2005. Ilipokuja mwaka 2005 kipindi cha ukereketwa wa kisiasa baina ya pande hizi mbili zilikuwa ni nzito katika suala zima la uchaguzi.

Kwa hivyo hii ni *strategy* maalum kwamba hii wananchi wasipewe upande mmoja na hii kweli tunaona hali halisi watu wanapewa vitambulisho watu ambao si Wazanzibari, wanaingizwa katika hii mashine ya *information* wanatiwa watu ambao si Wazanzibari.

Sasa mimi ninasema sisi ingekuwa vyema ningemshauri Mhe. Waziri huu Mswada urudishwe tena upya na hapa tukubaliane kwamba badala ya kusema Zanzibar *Resident* tuwe na kitu kwa sababu kuna maneno mawili ya kiingereza; moja linasema ni *resident* na moja linasema ni *citizen*. *Citizen* ni raia, *resident* ni mkaazi, kwa nini haya mambo hatuyaweki kama ilivyo. Sisi ni *citizen* na sio *resident*, kwa nini mswada huu ukaletwa kwa jina la mkaazi ilikuwa inatoka wapi mwaka 2005, kwa nini tusimfuate Marehemu Karume aliyesema uraia wa Zanzibar na wakaazi wa Zanzibar kulikuwa kuna kosa gani.

Mhe. Spika, hili ni suala muhimu. Sasa tunaulizana, hii kwetu sisi kupewa hiki kitambulisho ni *right* yetu au ni *privilege*, namuuliza Mhe. Waziri. Wazanzibari kupewa hati ya vitambulisho kwa Mzanzibari yeyote kwa jina hilohilo munalotaka nyinyi la mkaazi ambayo sheria imepitisha, lakini jee *is it right or is it privilege*.

Atwambie akija hapa Mhe. Waziri kama vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni *privilege is not right*, sio haki yetu sisi kupata vitambulisho, ni *privilege* tu, kwa hivyo atapewa anayetaka. Kama ikiwa ni *right* yetu basi kwa nini watu wote wapewe vikwazo hivyo.

Mimi ninataka niseme kitu kimoja. Mtu yeyote katika nchi za *Europe by birth* unapewa *passport* bila ya kujali wewe umefika miaka 18 au hujafika, madhali yule amezaliwa pale na ameshazaliwa ni Muingereza, Mmarekani au mtu yeyote wa nchi za nje basi akizaliwa ana *right* ya kupewa. *That's not a privilege*, ni *right* ya kila mtu anayezaliwa katika nchi ile. Kwa nini sisi watu wa Zanzibar haiwi hii ni *right* yetu, kwa nini hii iwe ni *privilege*.

Sasa hii mimi ninachokiona kwa ufupi ni kwamba ni kitu kibaya sana kumnyima kwa sababu sisi katika sheria ya mwaka 2005, tayari tulitunga sheria kama utakapokuwa huna kitambulisho cha Mzanzibari Ukaazi, maana yake kuna *imprisonment* kufungwa mwaka mmoja au faini ya shilingi laki moja, imo humu au kifungo. Hii haijachukuliwa hatua tu lakini siku yoyote askari wakati watakaposimama barabarani, wakasimamisha magari wakasema aliye na kitambulisho na aliyekuwa hana kitambulisho ateremke kwenye gari watu wengi watakamatwa na watakwenda mbele ya sheria na wao watapata adhabu.

Sasa kwa nini ifike hadi yote hiyo kwamba sisi tukamatane kwa sababu sheria hii inatukwaza sisi Wazanzibari lazima tutiwe adabu, kifungu cha mwaka mmoja au faini ya laki moja. Tumeweka hii ni ya nini. Is it right au ni *privilege* hii kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri sisi tuna hamu na wewe sana uje utueleze na wala usiifiche utueleze kwa nini ikawa hivyo. Sasa kwa umuhimu wa vitambulisho hicho hicho cha Uzanzibari Ukaazi, leo sisi Wazanzibari tunapata shida, sisi kama ni Wawakilishi wa jamii ya wananchi, sisi tunapata matatizo kwa wenzetu wanatwambia sisi tuna shida chungu nzima, tumekwenda kuomba vitambulisho, tumekwenda kuomba kwa Sheha kuomba barua tukapate vitambulisho hatupati tunanyimwa, mara tunaambiwa hivi na vile.

Kwa hivyo umuhimu wa hiki kitambulisho kweli kila mtu anahitaji siku hizi watu wanakwenda kibiashara, wanataka kuzunguka kutokana na hali ya kimaisha watu inabidi waende nje wakatafute maisha, kama hana kitambulisho cha kusafiria hawezi kuondoka katika nchi hii. Ina maana huyu tumemfunga hatuki nje, hapati kutoka nje, ukenda Dar es Salaam unaambiwa utoe kitambulisho, ukeja Zanzibar unaambiwa utoe kitambulisho, ina maana yake hawa watu wetu wasizunguke wala wasitafute maisha, *is it right* ni haki hiyo kumuweka ndani usimtoe nje. Hii ni ufungwa itakuwa huu.
Lakini la pili vile vile Mhe. Spika, hawa vijana wetu wanataka kazi, kama hana kitambulisho kazi hawezi kupata, hii ni haki. Jengine kwamba yeye ana mzigo wake *custom* anataka kwenda kuutoa kama hana kitambulisho cha Mzanzibari Ukaazi hawezi kuutoa mzigo ule *custom*.

Jengine kama si hilo vile vile kama yeye anataka kwenda benki kutoa pesa au kitu chochote kama hana kitambulisho cha Uzanzibari Ukaazi hawezi kutoa pesa zile au hawezi kuweka pesa zile.

Mwanafunzi ambaye anayetaka kusoma nje ni lazima awe na kitambulisho cha Uzanzibari Ukaazi, kama hana kitambulisho hicho, mwanafunzi huyo atashindwa kwenda kusoma nje. Lakini siasa mimi ninasema katika masuala haya, haya masuala tunayazungumza kwa mara ya pili au mara ya tatu katika Baraza hili, haya ni mambo muhimu sana na tuna wajibu wa kuyasikiliza na tukayachukuliwa hatua na sio tumezungumza katika Baraza halafu tukayaachilia yakatiwa makabrasha katika makabati ikawa *the end of the story*, hadithi imemalizika. Ninasema isiwe hivyo.

Lakini jengine ninalotaka kusema, haya masuala wamekabidhiwa watu, tunahitaji kuwa waadilifu na hili ni suala muhimu Mhe. Spika, nchi yetu hii uadilifu haupo. Hapana uadilifu, hapana uaminifu. Matatizo haya yanatukuta na ndio maana watu wadogo wadogo wakakosa haki zao kwa sababu watu tuliowapa dhamana si watu waadilifu. Kwa maana gani nikasema si waadilifu, isingekuwa imejitokeza mara nyingi watu kupewa Uzanzibari Ukaazi watu ambao waliokuwa hawastahiki kupewa Uzanzibari Ukaazi, ule ni uadilifu au si uadilifu wa kazi.

Vyombo tumepewa tunatumia katika *wrong way*, hatuitumii Kiuzanzibari, tuna *feed information* kwa watu ambao hawastahiki kutiliwa taarifa zile katika mashine zile. Mhe. Spika, utendaji umekuwa umekuwa unatuletea matatizo kinyume na utaratibu ambao tuliopanga hapa katika Baraza.

Kwa hivyo ile taarifa ambayo tutaipata ni muhimu ambayo itaweza kutusaidia katika kujua Wazanzibari wangapi waliopo hapa. Leo hii mashine zile haitupi Wazanzibari *actual number* ya Wazanzibari hatupi, kuna siri ndani yake imejificha hata katika uchaguzi uliokuwa umepita, tukitazama katika hili daftari la kudumu la wapiga kura kumeshajitokeza watu ambao si Wazanzibari ni wengi sana wamo mule. Ninataka twende *through* mwaka huu 2015 tuhakikishe kwamba daftari la kudumu la wapiga kura limekwenda sawa sawa kama inavyotakiwa. Muna watu wengi katika daftari la kudumu ambao si Wazanzibari na hii imejitokeza taarifa zake tunazijua na sote hapa sote wengine taarifa zake tunazijua.

Kwa nini tunafanya kitu kama hiki. Mimi ninasema pamoja na kuwa chombo tunacho cha kutaka kujua idadi ya watu lakini vile vile inatupa takwimu ya Wazanzibari katika chombo hiki. Leo chombo hiki hakina faida kwetu sisi na atwambie Mhe. Waziri takwimu aliyenayo katika chombo chake hiki cha *information*, atupe Wazanzibari ni kadhaa na wakaazi ni kadhaa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninasikitika kwamba vijana wengi wanatuelemea sisi Wawakilishi kwamba mimi nimekosa, mimi nina watu chungu nzima katika jimbo ambao wameshindwa vijana wabarobaro wazalia kindakindaki katika nchi yao, wanapewa watu wengine na wengine hawapewi, *is that fair*, ni haki hiyo.

Hili tunalolizungumza Mhe. Spika, tunamtaka Mhe. Waziri aandaeni *circumstances what so ever* Mhe. Waziri hili suala ni nyeti kabisa na tunataka achukue *serious step against* haya tunayoyazungumza, haya ni mambo muhimu, ni mambo ya wananchi na sisi tumeletwa hapa kwa ajili ya wananchi. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri vijana wamekuwa wakali sana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninahisi kwa hayo ambayo nilikuwa nimeyatoa yanatosha yaliopo katika mswada huu ni mambo ni marekebisho tu, lakini waziri hajatwambia mpaka hivi sasa atatusaidia kiasi gani katika matatizo haya.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa angalau atwambie mwaka huu itakuwa hivi na hivi atupe, lazima atakuwa na *outline* zake, atwambie yeye ndiye waziri tunayemtegemea hapa na sisi mambo yetu yote ni lazima tumwambie Waziri, wananchi wakipiga kelele ni lazima tumwambe waziri haya yatakuwa ni sehemu ya majukumu yake Mhe. Waziri.

Tunamuomba Mhe. Waziri akija hapa atueleze mambo haya kwa urefu tujue na suala langu nililompa ambalo ninamtaka Mhe. Waziri abadilike na yeye, *this is the world of changing* bwana! Hatuwezi kukaa na mambo yale kwa yale. Tunasema Wazanzibari tuwe raia wa Zanzibar, sisi wakaazi bwana, *resident* Mngereza yule ndiye aliyekuwa mkaazi (*British Resident*), *we are not resident*. Sisi *are born here*, tumezaliwa hapa, *this is our country*, ni nchi yetu hii, kwa nini tuwe wakaazi tusiwe raia.

Mimi nasema tuondoshe neno ukaazi, hebu tupeni tafsiri ya ukaazi, tupeni tafsiri ya uraia, nani raia, sisi si raia nchi hii. Tunasema hii nchi yetu Zanzibar ni nchi yetu, sisi ni raia wa Zanzibar, sisi si wakaazi mheshimiwa.

Kwa hivyo Mhe. Waziri akija hapa atupe *definition* nzuri tuelewe, jee atatupeleka kwenye uraia au atatubakisha kwenye ukaazi kwenye nchi hii, alilipata wapi jina hili akalileta hapa 2005 na hili ni neno la kigeni, *resident* ni neno la kigeni.

Ahsante Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, *thank very much*. (*Makofi*).

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru *Allah Subuhana Wataallah* kwa kumtakia rehema Mtume wetu (SAW).

Pili nikushukuru na wewe mchana huu kupata nafasi ya kutoa maoni yangu machache katika mswada wa sheria ulio mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza na mimi niungane na Kamati walipowasilisha maoni yao kwamba kuna wanafunzi kutoka nchi mbali mbali wanaokuja kuchukua elimu zao hapa Zanzibar, wanafunzi ambao miongoni mwao hawajafikia umri wa miaka 18 ambao hupatiwa vitambulisho hivi vya ukaazi.

Mhe. Spika, hili ni jambo moja la msingi sana kwa sababu mauti hayakuekewa rika wala hayajaekewa muda, ni wakati wowote mwanafunzi huyu anaweza akafika na wajibu wa kufa na akaleta tatizo wapi anatoka. Lakini iwapo serikali imemthamini kupatiwa hiki kitambulisho cha wageni basi itakuwa ni jambo moja rahisi mno kuweza mwili ule kufikishwa katika nchi yake anayotoka. Mimi nina sababu moja kubwa nimeiona ina umuhimu wake kwa wanafunzi wale ambao hawajafika umri lakini wapo nchini na wao kuweza kupatiwa vitambulisho hivi.

La pili ninataka kulizungumza katika kamati maoni yao ni suala zima la Wazanzibari walio nje ya Zanzibar ambao hawa nchi ina matumaini makubwa kuwa Wazanzibari hawa kuweza kusaidia nchi yetu. Karibuni hivi tulipitisha sheria ya Wazanzibari hawa wanaoshi nje ya nchi kuwajua wapo nchi gani na gani na kuwajua ni kiasi gani ili wanapotuma pesa zao kuingia hapa Zanzibar basi ziwe zinakwenda ule utaratibu wa sheria.

Sasa watu kama hawa tunapowaacha ikawa hawajulikani katika huu Uzanzibari wao, kwanza tutakuwa tunaipoteza ile haki yao na itaonekana kuwa hatuwajali wao lakini kile chao tunakijali. Kwa hivyo ningelimuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelekeze kuhusu Wazanzibari hawa walio nje ya nchi sheria hii au mpango gani wanaweza kuekea hawa ili na wao waone kwamba nchi yao imewajali.

Mhe. Spika, tokea asubuhi tulipoanza kujadili mswada huu Waheshimiwa wanatoa maoni yao mbali mbali na baadhi ya maoni haya yana masikitiko makubwa kutokana na baadhi ya Wazanzibari kutokupatiwa vitambulisho vyao vya ukaazi.

Vile vile Mhe. Spika, ninapata mashaka makubwa sana Mzanzibari kuitwa Mzanzibari Mkaazi. Huwa Kiswahili hiki kwa kweli kinanisumbua na kumbe sio peke yangu tupo watu wengi ambao tunasumbuka na suala hili, hufika tukajiuliza hasa huyu Mzanzibari hasa ni yupi, kama Wazanzibari wote ni wakaazi, wahusika Wazanzibari ni akina nani.

Kwa hivyo kwa hali yoyote wapo watu wamezaliwa hapa kwa muda mrefu ndio pao lakini bado anaitwa mkaazi. Mimi ningeliiomba sana serikali isiwe na kigugumizi suala zima la Mzanzibari. Ni vyema pale ambapo tumeona kwamba sheria imekosekana maandiko yake si vibaya hii ndio wajibu wa mwanadamu na mwanadamu yeyote linaweza likaandikwa lakini mbele ya safari likaonekana lina matatizo.

Kwa hivyo kufanya marekebisho ni wajibu wetu wala serikali isiwe na kigugumizi kwa hili, tusiitwe Wazanzibari Wakaazi, huu ni wajibu wetu. Kumbe ilikuwa huyu mgeni ndio wa kuitwa Mzanzibari Mkaazi na huyu Mzanzibari akawa ni Mzanzibari.

Sasa ukiangalia sheria inavyojieleza humu utaona kama inakanganya, haifahamiki. Ni vyema pakafanywa mabadiliko Mzanzibari akaitwa Mzanzibari na Mkaazi anayekuja kukaa hapa Zanzibar akaitwa Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, tukija katika Uzanzibari Ukaazi, sheria iliyopitishwa mwaka 2005 tumeona kwamba vilianzishwa vitambulisho, lakini vitambulisho hivi vimefanya matatizo makubwa. Mimi hapa mbele yangu Mhe. Spika, nina stakabadhi mbili ambazo nimezipata ghafla tu za wananchi walionyima hadi leo hawajapewa vitambulisho vyao vya ukaazi.
Hii stakabadhi moja iliandikwa tarehe 27 mwezi wa saba 2005 na hii nyengine alipewa huyu bwana tarehe 29 mwezi wa saba 2005. Stakabadhi hizi zilichukuliwa hapa hapa Mkoa wa Mjini/Magharibi lakini hadi leo watu hawajapata vitambulisho vyao. Wanaloambiwa nenda uje hadi leo.

Mhe. Spika, wananchi wetu tunawapeleka wapi. Kama stakabadhi zao bado wanazo na wanapokwenda kwa wahusika hawapati jawabu ni nenda uje. Tunawapeleka wapi wananchi wetu. Kitu unapokifanya sheria ni kwamba sheria ile ifuatwe na mtu umeshafika kumpa stakabadhi unamnyima humpi kitambulisho chake, malengo yako ni yepi, afungwe, apigwe faini.
Kwa hivyo hii Mhe. Spika, inaonesha wazi kwamba ndani ya chombo hiki kuna watu hawatendi haki. Sasa usioe leo upo duniani mzima unadunda ni dunia hii hii itakayokuacha na ikakufedhehesha. Hii ni haki na siku zote Waswahili wanasema haki haizami, haki itakuja juu tu.

Kwa hivyo tukiendelea kuwanyima basi jua na wewe ipo siku na wewe kuna jambo muhimu utanyimwa. Hiyo ni lazima tu, unapomtendea wema mwenzako na wewe utatendewa wema, ukimtendea maovu mwenzako na wewe utatendewa maovu. Hivyo Mhe. Spika, huu sio utaratibu mzuri.

Mimi ningelimuomba sana Mhe. Waziri hebu akague hivi vyombo vyake. Malumbano haya mpaka lini, tutafika wapi au tunasema midomoni tu lakini ndani ya nyoyo kuna na mengine. Kama itakuwa ni hivyo Mhe. Spika, itakuwa hakuna lolote la maana tunalokuja kusimama hapa tukilisema, tunasema kwa midomo lakini ndani ya nafsi zetu muna kutu. Hii hatufiki kabisa.

Mhe.Spika, suala hili la vitambulisho katika bajeti iliyopita hapa ya Mhe. Waziri aliliahidi Baraza hili kwamba tatizo hili baada ya Baraza atafuatana na Waheshimiwa Wawakilishi katika majimbo yale yote ambayo yana matatizo ili kuhakikisha tatizo hili amelionda.

Mwezi wa saba, wa nane, wa tisa na wa kumi; leo tupo tarehe 16 Oktoba, 2012. Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze ni jimbo gani na gani ambalo tayari amelifuatilia hili tatizo pamoja na Mwakilishi husika kuliondosha hili tatizo. Isibakie inasemwa tu, kusema sio kutenda Mhe. Spika, matendo ni lazima uyafanye. Kama tutabakia na kusema siku zote tutakuja hapa na kubishana na hatma yake nchi hayendi.

Kwa hivyo ni vyema tunapotoa ahadi tutekeleze. Kuna watu wanasema aah! haya mambo ya kisiasa. Waheshimiwa hakuna siasa mbele ya Mwenyezi Mungu, Mungu ameahidi kwamba kila unalosema linadhibitiwa, kila unalosema linaandikwa na pia unalolifanya utakwenda kuulizwa. Kwa hivyo tusihadaike na ulimwengu tukaliona jua linatoka mashariki na kutua magharibi, wananchi wetu tukawanyima haki zao ambazo haki hizi tumezitengeneza sisi wenyewe. Kwa hivyo ningelimuomba sana Mhe. Waziri aje anieleze kuhusu ahadi hii aliyeitoa hapa Barazani ameifutilia kiasi gani.

Lakini pia Mhe. Spika, niseme kwamba kuleta mswada huu wa kuwapatia haki wageni si vibaya, ni vizuri sana. Lakini kwanza Mhe. Spika, unajiangalia wewe. Leo nyumbani mwako umepata kilo moja, uhalali wako wa kula ni kilo mbili na nusu, lakini familia uliyonayo chakula hiki kilo moja wanakisha chote, lakini unasema aah! Nyinyi wanangu laleni na njaa msile kabisa, kungejea kwanza tuwape hawa wageni. Hapo hujatenda haki. Sadaka inaanza nyumbani.

Bado Wazanzibari wengi wana kilio vya kuhusu vitambulisho. Sadaka hii hawajaipata. Mhe. Spika, ni vyema Mhe. Waziri akafanya upembuzi wa kujulikana hawa Wazanzibari ambao hawana vitambulisho wakapewa mwanzo hatimaye tukaandaa karamu kwa ajili ya wageni. Lakini nyumbani kuna njaa bwana, halafu unakuja kumpa mtu mwengine, hii itakuwa hajatenda haki.

Mhe. Spika, mimi ninasema kwamba mswada huu si mbaya ni mzuri, tatizo lake kubwa ni hili la kutomjali Mzanzibari kwanza. Iwapo kama Mhe. Waziri atakuja hapa kunihakikishia kwamba Wazanzibari wote ambao wana haki ya kuwa na vitambulisho vya ukaazi, kuna mpango ameuandaa na mpango huo ukaniridhisha basi sina matatizo na mswada huu kwa ajili ya wageni. Lakini atakapokuja ikawa maneno yake ni yale yale, serikali ina matatizo, serikali ni hivi, tutashirikiana, hakuna la msingi kuhusu Wazanzibari hawa basi mimi sitounga mkono hoja hii.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nafasi hii ndogo ya kumalizia kwa siku hii ya leo kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake mzuri.

Aidha pia Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kutekeleza vyema ilani ya CCM, kwani yote haya yanatokana na ahadi ambazo zimo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuleta utawala bora Zanzibar. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mhe. Spika, mswada huu kwa kweli utapunguza matatizo mengi hasa kuwepo kwa wageni ambao wanaishi hapa Zanzibar bila ya kujulikana nini wanachokifanya.

Lakini Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 (a) (3) (c), “Kuwepo orodha ya masharti ya vigezo kwa wafanyakazi wasiokuwa Wazanzibari ili kudhibiti matatizo ambayo yanaweza kujitokeza kwa wafanyakazi hawa”. Mhe. Spika, leo hii asubuhi wakati nauliza swali Mhe. Waziri alishindwa hata kujua ni Wa-South Africa wangapi ambao wanafanya kazi ya utalii hapa Zanzibar.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sheria hii itaweza kuwatambua wale wageni wanaofanya kazi hapa Zanzibar. Mhe. Spika, pia katika kifungu cha 6 (a) (3) (a), kifungu hiki pia kimejumuisha wafanyakazi ambao hawana mikataba ya maandishi ili kuweza kuwatambua kile ambacho wanachokifanya.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sheria hii haina matatizo bali naona watu wanajitakia tu au hawataki kuifuata sheria hii hasa wale wanaoishi nje ya nchi na wanakuja hapa wakati ule wakati wa kupiga kura ili wapate kupiga kura. (*Makofi*).

Mhe. Spika, vitambulisho vipo na maelfu wa Wazanzibari wapo ambao hawajaenda kuvichukua wao wenyewe. Mimi ningeomba Mhe. Spika, wale ambao vitambulisho vyao vipo basi waende wakavichukue, isiwe lawama tu huko mitaani vitambulisho hatupati.

Mhe. Spika, kila nchi ina utaratibu wake wa kutoa vitambulisho vya kuzaliwa na pia vya wale wageni. Mhe. Spika, kwa kweli tatizo hili la vitambulisho ninaona tunajitakia wenyewe, kwa sababu kuna wengine ambao tunakuwa hatutaki kufuata zile taratibu.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano mimi ni Mzanzibari, Mtanzania, nimezaliwa Zanzibar katika Kisiwa cha Pemba, Kijiji cha Kengeja Msalani. Katika kutekeleza yote haya kuona kwamba hakuna ubaguzi wa Mtanzania, Mzanzibari kwa Mpemba, kwa Muunguja, Wamatemwe, Wamkoani, Wawambaa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo. Ni Mpemba mzaliwa, mimi mwenyewe wazazi wangu, babu zangu lakini leo mimi ni mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo na haya yote yanaonekana kuwa hakuna ubaguzi wa Chama cha Mapinduzi, kwa serikali hakuna ubaguzi. Sasa mimi ninashangaa wanasema wengine kwamba kuna ubaguzi wengine hawapewi vitambulisho, wengine wanapewa vitambulisho. Kwa hivyo hili kwa kweli sio kweli lakini ni utaratibu tu. (*Makofi*).

Mimi mama yangu ni mzaliwa wa Pemba. Hivi juzi tu kwa vile alikuwa hajui taratibu nilimfahamisha fanya taratibu hizi na hizi, na leo hii anacho kitambulisho cha Mzanzibari. Kwa sababu gani, kafuata taratibu. Kwa hivyo ningewaomba wananchi wenzangu Wazanzibari, Wapemba, Waunguja tufuate taratibu ili kuweza kupata vitambulisho cha Mzanzibari na tuondoe ubaguzi, sote ni wamoja ni ndugu, tumezaliwa Zanzibar, aliyezaliwa Bara leo kafika hapa kakaa miaka 10 ni Mzanzibari.

Kwa hivyo baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kwa asilimia mia moja naunga mkono mswada huu.

**Mhe. Spika:** Kuna dakika zisizozidi 10 jina linalofuata ni la Mhe. Fatma Mbarouk Said. Kama zinatosheleza basi zitumie hizo.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia mswada huu.

Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada mbele yetu ili sasa tuujadili kama Wawakilishi, tutoe maduduku na hatimaye tuipitishe kama sheria ya usajili mzanzibari mkaazi.

Mhe. Spika, wenzangu kwa kweli wamenifilisi waliopita kwamba serikali inakuwa na mitazamo yake na miongozo yake. Kwa hivyo serikali inapotoa miongozo hiyo ni lazima sisi kama ni wananchi basi tuifuate.

Mhe. Spika, mimi nichukue fursa hii kuwaomba Wawakilishi wenzangu tuchukue jukumu hili la kuwaelimisha wananchi wetu mbali mbali ambayo serikali inayatoa kwetu sisi viongozi ambao ni wawakilishi wa wananchi katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba vitambulisho vilitoka lakini kwa mtazamo ile ile ya kisiasa tulishindwa kuwahamasisha wananchi ili kujua umuhimu wa vitambulisho vile. Ni baadae tu ya kuambiwa kuwa huwezi kupiga kura ni lazima uwe na kitambulisho cha Mzanzibari, hapa sasa imekuwa kila mtu akachukua kwamba fursa hii kanyimwa na kumbe mwanzo vilivyotoka hatukuchukua umuhimu wa sisi kama Wawakilishi tukawaelimisha wananchi umuhimu wa kitambulisho hiki. (*Makofi*).

Mhe. Spika, juzi tu kama alivyosema mwenzangu na kwa kweli kanifilisi sana Mhe. Panya; juzi juzi tulikuwa na sensa pia lakini kwa kutokujua umuhimu wa sensa watu walifunga milango na kuchukua fursa mikononi mwao hata kuwafukuza kabisa katika maeneo yao.

Lakini hebu kama sisi Wawakilishi kwa nini hatuelimishi, tuwaelimishe watu umuhimu wa sensa, hata ndani ya majumba yetu kama hatukuwa na hesabu ya watoto wetu na nashukuru sana kila unapopata mtoto unakuja ukaulizwa ni mtoto wa ngapi, unasema sasa ni mtoto wa nane. Kwa nini kwenye sensa tunakuwa wagumu na kwa nini hatuwafahamishi wananchi na sisi tuliochukua nafasi ya kuja humu ndani ya Mabaraza kama haya.

Mimi nashangaa sana leo kusikia kwamba sisi humu tunasema kuwa hatupitishi. Hebu tuseme tunaelekea wapi juu ya hili kwamba tunaliona hili jambo ni muhimu na baadae tunaanza kugongana sisi wenyewe humu ndani, kila mtu anasema mimi sipitishi. Hivyo tutakuwa tumefanyia haki wale wananchi kule nje. Kweli tutakuwa tumewafanyia haki.

Leo tumo humu ndio kwenye hili Baraza, kesho nje, hebu tuchukueni juhudi ya lazima ya makusudi, kuna mambo mengi yanatendeka, serikali yetu ni hii. Hebu tuwaelimishe vijana wetu jambo dogo si dogo tunaona na sisi viongozi tumo humu kwa nini hatukatazi, mabarabara yanachomwa moto, tunakaa humu bajeti hiyo ipo wapi. Kweli sisi tunataka nchi yetu hii iendelee. Hebu jamani sisi ni Waislamu sote na sisi kama tumechaguliwa na wenzetu tuwaongeze basi tuwaongeze kihalali. Ni lazima tufuate utaratibu kama viongozi kesho tutakwenda kuulizwa kwa watu tuliowaongoza.

Kwa hivyo ni lazima sheria hii tuipitie, tuijadili vizuri na kisha tuipitishe Mhe. Spika. Mhe. Spika, kumbukumbu ni nyinyi na tukizisema leo tutarudisha madonda, sisi sote hapa ni wamoja. Mimi ni wa Mtambwe, Farida wa Mtambwe, Assaa wa Mtambwe, Asha Bakari wa Mtambwe, Omar Ali Shehe ni Mtambwe lakini anahusiana na huku, tunakwenda wapi (*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Spika, niseme kwamba sheria ni nzuri na leo hii ndio imekuja na sisi ndio wapitishani wa sheria hii, tuache yote tuliyokuwa nayo ili wenzetu huko nje watufahamu. Lakini tukianza Mwakilishi wa CUF anasema humu kwamba yeye hapitishi sheria hii, ina maana na huko nyuma nje anawasemesha hivyo hivyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninasema sheria hii tuipitishe kwa pamoja.

Ninashukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa michango, bado wapo wachangiaji ni wengi kidogo inaonekana kuna marejeo mengi ya michango hii. Kwa hivyo nategemea kwamba jioni tutamaliza halafu tupitishe mswada kwa kadri itakavyokuwa. Niombe basi Waheshimiwa Wajumbe mambo mawili.

Kwanza wale Waheshimiwa ambao bado hawajapata nafasi ya kuchangia na wameomba na nadhani wanatosha, tufike mapema ili shughuli hii tuimalize. Nao ni Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Hilo la kwanza tufike mapema ili tuweze kumaliza michango ya mswada huu ambao kimsingi ni mfupi sana.

Lakini la pili wananchi wetu wanatuuliza sana mbona tumepwaya mno humu ndani *quorum*, kuna mambo mazito muhimu lakini Wawakilishi wa wananchi wa kuyashughulikia hayo hawapo wa kutosha humu ndani. Si vizuri hatuwakilishi vyema.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote tuhakikishe kwamba tunafika tena kwa wakati ili tumalize kazi hii na wajibu huu. Mimi ninashukuru sana kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi tumekuwa tunatamka tutakwenda kuulizwa, wengi karibu wote, tutakwenda kuulizwa.

Basi tutimize wajibu ili tukaulizwe tujibu vizuri na moja kati ya wajibu wetu ni kufanya kazi ya kuwawakilisha wananchi wetu na wala sio kuwachanganya wananchi. Kwa hivyo niombe sana Waheshimiwa Wajumbe tufike kwa wakati tufanye kazi tunayojipangia kuipanga.

Baada ya machache hayo basi tuakhirishe kikao chetu hiki hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia jioni hii tukawa hapa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuleta marekebisho haya ya sheria ya usajili wa Mzanzibari nambari 7 ya mwaka 2005 kama yalivyoandikwa katika kurasa hizi. Nasema ni jambo zuri, kuonekana kitu chochote kina upungufu basi kufanyiwa marekebisho ni jambo la msingi.

Mhe. Spika, vile vile niipongeze nayo Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa marekebisho yao waliyoyafanya. Katika marekebisho haya na wao nadhani walikuwa makini katika kujadili marekebisho haya.

Mhe. Spika, mimi mswada huu wa marekebisho nimeusoma na nimeufahamu kwa makini sana, katika marekebisho haya ikiwa ni pamoja na kutaka kuwasajili wageni watakaoingia katika kisiwa chetu cha Zanzibar, ni jambo zuri na ni jambo la busara. Mimi hili silikatai na ninakubaliana nalo kabisa.

Lakini katika madhumuni na sababu yaliyoelezwa katika marekebisho haya ni mazuri nayo ukilinganisha na yalivyoandikwa. Lakini Mhe. Spika, tatizo lililopo ni Wazanzibari wetu tunaposema kwamba kuna watu wanakuwa na matatizo na kusajiliwa katika ofisi hizi za usaji. Wala hili Mhe. Spika, Mhe. Waziri asitukatalie, kwa sababu sisi ndio tulioko huko kwa wananchi na haya ni matatizo ambayo tunayaona mpaka maofisini.

Mhe. Spika, katika madhumuni yake Mhe. Waziri kasema usajili wa Mzanzibari Mkaazi chini ya sheria mama, ilikuwa na dhamira ya kuweka utaratibu bora na utambuzi wa Mzanzibari Mkaazi kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji wa huduma, tofauti zinazotolewa na taasisi za umma. Zoezi la usajili lilionesha kuwa na mafanikio, hata hivyo kunaonekana baadhi ya matatizo ya kiutendaji na malalamiko ya wananchi dhidi ya utaratibu wa usajili. Matatizo hayo kwa jumla wake yameanza kufanyiwa kazi ili kuboresha mfumo mzima wa usajili. Hili ni dhumuni moja alilolieleza yeye Mhe. Waziri katika madhumuni yake kwenye sheria hii, kwamba kakiri kuwa kulikuwa na matatizo. Lakini yameshafanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, mimi nakubali kutokana na kauli nyingi tunazozisikia kwa mawaziri, naona sio watu wa tabu hata kidogo, ni watu wapole na ni watu wataratibu. Lakini matatizo haya sana yanajitokeza katika wizara zao au watendaji wao ndio wanaokuwa na matatizo haya. Ndio maana pale tunapokaa tukazungumza kuwa kuna moja, mbili basi Waziri anastahiki atusikilize, ili matatizo haya aweze kuyafuatilia na kuyapatia ufumbuzi. Hilo ndio suluhisho. Lakini kama tutaonekana kuwa tunazungumza hivi kwa utashi wa kisiasa, au tunazungumza hivi kwa sababu ya chama fulani, hii itakuwa hajatutendea haki. Mhe. Spika, ni kweli vitambulisho vinatolewa, lakini katika njia ya usumbufu mkubwa.

Lakini katika madhumuni yake ya pili kasema kuwa ni nyenzo muhimu katika utambulisho wa maisha ya kila siku ya jamii. Sasa hivi vitambulisho hatuwapigii wananchi kelele tu kwa sababu ya kuwa aunge mkono chama fulani, lakini ni kwa sababu ya kuwa kitambulisho sasa hivi kimekuwa ni kitu muhimu kwa mtu yeyote. Ni kweli kwamba mwaka 2005 vitambulisho vilitolewa, wengine wakadharau, lakini kulikuwa na sababu mbali mbali. Wengine walidharau, wengine walikuwa hawapo. Lakini kuna wengi waliokuwa hawakufikia umri huo.

Mhe. Spika, katika kipindi kile cha nyuma sisi tulikwenda tukapewa kitambulisho bila ya matatizo yoyote, bila ya vikwazo vyovyote, hutakiwi cheti wala hutakiwi kitu chochote. Sasa leo inakuwaje vizazi vyetu visiweze navyo kupata fursa kama hii. Au kuna ulazima gani ya kuwa ni lazima aende na Sheha na wakati ana cheti cha kuzaliwa, kwani cheti cha kuzaliwa kina matatizo gani. Cheti cha kuzaliwa kina vielelezo vyote vya kujulikana kuwa huyu kazaliwa wapi, wazee wake ni wapi, leo tatizo ni nini. Hapo tulipopewa sisi ilikuwa kuna madhumuni gani na hivi sasa kutolewa bila usumbufu kuna matatizo gani.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpe ushahidi mmoja Mhe. Waziri ambapo ni mwezi huu wa tisa tu tulikuwa katika Wilaya ya Micheweni. Kwa sababu Mhe. Rais kachagua mawaziri wake waliokuwa makini na ukiwatizama ni watu wasikivu, lakini watendaji wao wanakuwa ni wakorofi ajabu ya Mungu.

Mhe. Spika, walijitokeza vijana wawili kutoka Tumbe wakaenda na fomu za kwa Sheha na vyeti vyao vya kuzaliwa, baada ya kufika Wilayani wakaingia katika ofisi moja wakamkuta msichana, pengine wakaeleza matatizo yao wakapeleka vile vielelezo vyao, lakini alishindwa kuwafahamisha ni namna gani ya kufanya. Alizichukua fomu zile za kwa Sheha akazichana na akazitia kwenye *dust bin*.

Mhe. Spika, tunayoyasema ni kweli, hatukuja hapa kusema uongo, tumekuja hapa kwa ajili ya kusimamia wananchi. Hilo lilitendeka, vijana wale wakawatafuta viongozi wao wakawalalamikia, baada ya kuwalalamikia sisi tulikwenda Wilayani na lengo letu tumuone yule Mkuu wa Wilaya, lakini kwa bahati nzuri siku hiyo hakuwepo, ikabidi tumkute Afisa Mipango, ambaye anaitwa Hamad Masoud tukamueleza suala lile, kwa bahati nzuri akakiri jambo lile kuwa huyu mwanamke kafanya makosa, kwa hivyo hili suala niachieni mimi. Hiyo ndio hali halisi ilivyo. Je, hapo panakuwa na utendaji wa haki. Kama walikosea kuingia ofisi sio yake, basi ilikuwa yeye awafahamishe, na kama fomu zilikuwa sizo awafahamishe, lakini hilo ndilo lililotokea. Tukienda pale Mheshimiwa huyu Hamad Masoud akaomba radhi mbele ya viongozi. Mhe. Subeit Khamis Faki alikuwepo, Mhe. Mbunge wa Micheweni alikuwepo karibuni wawili.

Mhe. Spika, lakini sio hilo tu, watendaji hao hao waliokuwa wamewekwa pale kufanya kazi za serikali wanalipwa, lakini inafika pahala wanakwenda kazini saa 5:00. Nakuambia hivyo Mhe. Spika, kwa sababu mimi baada ya masuala yale nilikuwepo pale Wilayani nikizunguka zunguka, nikawauliza vijana wale waliokuwepo pale, wakasema wao wamekuja pale toka asubuhi anasubiriwa mpiga picha, mpiga picha huyo hajulikani aliko. Kitu ambacho unaweza kujiuliza Mhe. Spika, huyu mpiga picha ameajiriwa hapa au ni mtu binafsi. Sasa utaona usumbufu umo katika suala hili la vitambulisho. Mhe. Waziri anastahiki akae kitako azungumze na watendaji wake waache ubinafsi wao, hili suala halikuwa dogo tena sio mambo ya kisiasa haya. Sasa hivi ukienda benki huruhusiwi kufungua *account* kama huna kitambulisho, tiketi sasa hivi huruhusiwi kusafiri kama huna kitambulisho. Sasa haya ni mambo muhimu ambayo vizazi vyetu vinatakiwa na wao wafuate utaratibu wa kutafuta vitambulisho.

Mhe. Waziri tunakuomba sisi hatupingani na kuwasajili wageni. Wageni wasajilini ni haki ya serikali kujua ni wageni wangapi waliopo, wanafanya kazi gani na wapo kwa madhumuni gani, hiyo ni haki ya serikali. Lakini sasa na sisi tuliopo raia ni lazima tutendewe haki, tusifanyiwe kama tuliokuwa hatujulikani hapa.

Mhe. Waziri nakuomba sana hayo ni matatizo yako na kama hukuzungumza na watendaji wako basi itakuwa siku zote tutakuwa hatuna imani na wewe, na ilhali kumbe ni watendaji wenu ndio wanaowaponza katika mawizara, hilo mkae mkilijua. Sisi hatuna masharti ya kuwa tusikubali mswada huu kwa kipengele cha kusajiliwa wageni, hilo hatuna tatizo nalo. Lakini tatizo tunalosema vikwazo vipo na huo ni ushahidi. Kama Mhe. Waziri utataka tuende katika Wilaya hiyo, basi niko tayari kwenda na kuthibitisha suala kama hilo.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, mimi siungi mkono hoja hii, mpaka Waziri atakapokuja kunijulisha ni utaratibu gani atakaoufanya kuhusu watendaji wake. Ahsante.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipata fursa jioni hii ya leo kuweza kuchangia mswada huu wa kubadilisha baadhi ya vifungu vya kuwezesha kunufaika wananchi waliokuwa ndani na wa nje kuweza kupata vitambulisho.

Mhe. Spika, kwa kweli tangu asubuhi nimesikia mijadala mingi sana, lakini la msingi hasa mswada huu Mhe. Spika, kuna baadhi ya vifungu Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake waliona iko haja ya kuvirekebisha na vyengine kuongeza ili kuleta ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa sasa hivi kuna mambo ya sayansi na teknolojia, kuna mambo ambayo sasa hivi yanabadilika. Kwa hivyo, kila wakati ukifika wa kubadilika basi na wao Mhe. Waziri hasa katika wizara zake anaona yapo mambo ambayo yanamlazimu kubadilika.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wake wa Vitambulisho na watendaji wake wakuu kwa kutuletea mswada huu. Mhe. Spika, habari hii mimi nilikuwa nikiizungumza siku nyingi sana na wakati ule nilikuwa ni mkali sana wa kueleza masuala ya vitambulisho na ilifika hadi Mhe. Spika, nikatoa vielelezo.

Lakini Mhe. Spika, mimi kijana wako ujue nimepevuka kwa njia moja. Siku hizi baada ya kutoa hoja katika Baraza, basi baadae nafuatilia hoja yangu. Singoji tena mtu nikapigana naye mpaka kwenye bajeti, sasa hivi hiyo nimeiondoa nina *system* mpya na mimi nimebadilika.

Mhe. Spika, baada ya kutoa hoja ile mimi nikaenda katika ofisi ya vitambulisho, ili kuweza kufuatilia zile hatua ni jinsi gani ambavyo tumezungumza kwenye Baraza hili na zimechukuliwa hatua za kiasi gani. Mhe. Spika, binadamu ni binadamu, makoseo yapo na yanakuwepo mapungufu ni lazima tukubaliane nayo hayo yanakuwepo. Lakini binadamu vile vile hukaa pahali na yeye akafikiri na kuwaza, akalitengeneza lile pungufu ambalo lililotokezea.

Mhe. Spika, kwa kweli masheha wetu waliteleza sana. Binadamu anakuwa na mbinu za kuweza mtu kudanganya jambo na likakubalika na ukaliona hili jambo ni kweli na wakati sio kweli. Mhe. Spika, samahani sana nitawatolea mfano hai na nimeona mimi mwenyewe, japo watu nikisema mfano wa nje, wengine wanafurahi na wengine wananuna, wache wanune, lakini si nimeona. Ukweli nitausema.

Mhe. Spika, nimekwenda katika nchi ya Austria ambako nilimuona mtu ambaye alidanganya kuwa yeye ni mtu mmoja katika *member* wa nchi za Europe, wakati anataka kazi. Akatoa vyeti vya uongo, akabadilisha uraia wake. Lakini tizama hatari iliyomkuta na sio yeye tu, hata na yule mwekezaji hatari ilimkuta kubwa sana. Mhe. Spika, wenzetu wanafuatilia sana. Lakini yule alifanikiwa kuingia nchi ile na aliweza kufanya kazi kwa muda wa wiki moja. Lakini wenzetu wana mtindo wa kila baada ya muda wanakuwa wanatizama zile *system* zao, vitambulisho vyao na ukaazi wa mtu, wanakuwa wanatizama bila ya wewe mwenyewe kufahamu. Kwa hivyo, yule mtu akagundulikana kuwa kumbe sio mtu wa nchi zile za Europe ni mtu wa Colombia huko chini kabisa. Mhe. Spika, mtu yule aliondoshwa kwa masaa 24 na hoteli ile aliyokuwa akifanya kazi imefungwa moja kwa moja mpaka leo hii yule jamaa wa hoteli analia kuwa kaingia hasara.

Mhe. Spika, na hawa ndugu zetu wa vitambulisho na wao halikadhalika kuna mambo ambayo wameyafanya wakishirikiana na uhamiaji, baada ya kusema baadhi ya wengine wamekimbia wenyewe, wengine wamewakamata wako mahakamani. Tatizo liko wapi, wanafanya kazi vizuri sana ndugu zetu hawa Wakurugenzi na watendaji wake, lakini binadamu Mhe. Spika, tusilaumu wakati hatujaenda kutafuta ile njia.

Tatizo sasa Mhe. Spika, liko hapa, kuna sheria ambayo iko wazi na hiyo ni sheria. Mhe. Spika, ukitaka kwenda nje unaulizwa wewe hapa, kwamba unakwenda kule sehemu gani na unafikia kwa nani, ndivyo ilivyo. Lakini mimi nashangaa sana kwa sisi leo Waafrika tunakataa hapa hapa ndani wenyewe tumeweka sheria ya hapa kwa hapa tunakataa ni kitu ambacho kinanisumbua sana Mhe. Spika. Ukitoka katika mji wa kwanza ukienda mji wa pili ni lazima utoke na barua ya Sheha kwenda katika mji wa pili, sioni kama ni tatizo. Kwa sababu kuna namna mbili pale, wewe ujulikane kuwa unatokea wapi, lakini hili tunalikwepa.

Mhe. Spika, mimi siku ile nilipotoa hoja hapa *Wallahi* nilipata watu wengi sana na wenyewe ni mashahidi hawa watu wa vitambulisho. Nilitoka na watu wengine kutoka Tumbatu na Magomeni. Nilikwenda Mhe. Spika, kuwatafutia utaratibu wa vitambulisho na wamepata, kumbe wamekosea utaratibu tu, hii kweli tuseme. Kuna fomu ambazo ni maalum za rufaa.Mimi Mtumbatu ni jamaa yangu, lakini kwa siku ile sikumuweka kama ni jamaa yangu, wala sikumuuliza wewe ni chama gani, una dini gani. Mimi nimeona kwa kuwa ni mmoja katika waliotoa hoja, nikaona nikamilishe ushahidi wangu, tatizo liko wapi. Nimekwenda kule nimechukua fomu ya rufaa wamejazishwa wale watu, wenye makoseo wamefahamishwa warudi kule kwa sheha arekebishe hili, na mimi nikafuatilia hatimaye kule kuna jopu maalum likiongozwa na Mwanasheria. Mwanasheria anakaa *pending* na watu wake wanaliangalia lile jopu. Mhe. Spika, mimi sioni tatizo hapa mpaka tunasema hawafai au kitafutwe kitambulisho, hatufai sisi kwa sababu hatufuatilii, huo ni ukweli tuseme Mhe. Spika. Tatizo la mswada huu sasa hivi ni kuwarahisisha na wale wenzetu walioko nje kuwaambia na wao ili wajulikane uraia wao.

Mhe. Spika, mimi nikienda nje natembea na uraia wangu wa Mzanzibari, situmii kitambulisho chako, kwa sababu na mimi najinasibu nina sehemu yangu na nchi yangu ya Zanzibar, ina watu na ina maeneo. Kwa hivyo, natembea nacho kile, nikiambiwa kitambulisho, *passport* sitoi, basi cha mwanzo natoa kile. Kwa sababu mule muna lugha

mbili, kuna Kiingereza na Kiswahili. Sasa mimi hiki ni kitu ambacho kinaniumiza kichwa sana, tangu asubuhi mimi kichwa kinaniwaka moto Mhe. Spika, kwani tatizo liko wapi.

Mhe. Spika, kumbe tatizo ni kwamba sisi wenyewe tunazubaa kuzifuata zile sheria. Mhe. Spika, tulisema hivi tufanye zoezi la kwenda kuhakiki. Mhe. Spika, mimi kule kwangu tumefanya uhakiki ipo mpaka leo havitambulikani, huu ukweli tuseme na wapo wanaendelea msifikirie wapo Unguja tu watakwenda mpaka Pemba. Mpaka leo Mhe. Spika, nakuhakikishia tayari watu wengine wale waliofikia muda mbona wanapewa tu na wakifika kule hawaulizwi, kwani tatizo liko wapi.

Mhe. Spika, mimi nakuambia tatizo letu sisi Waheshimiwa tunapiga kelele bila ya kufuatilia na hii ndio athari yetu inayotufika. Kwa sababu mtu kama jambo halitaki atakuwa halitaki tu, hata kama zuri vipi basi halitaki tu. Hata mimi baadae likitokezea jambo jengine kama silitaki nitalisema tu, lakini hili mimi silikatai, lakini kumbe mimi napinga sheria. Mimi sioni haja ya mtu kusema kwamba mswada huu mimi siuungi mkono hata siku moja, mimi nakataa sana Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nakubaliana na Mhe. Waziri tuwatengenezee mafao wale wa nje, kuwatambulisha na kuwapa vitambulisho, hiyo ndio hoja nzito ya kuweza kujadili sisi ili kumpa nguvu Mhe. Waziri kuwatambulisha wale.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba nilisema hapa kwenye Baraza hili kuwa ipo haja sasa *investors* ni lazima wapewe vitambulisho. Mhe. Waziri kaitikia na kakubali kuwa ni msikivu na ni mtu mzuri Phd, kalikubali suala hilo, ndio hili sasa kalileta hapa. Kwa sababu Mhe. Spika, ma-*investors* wetu walikuwa wana-*hang* na tunawapa matatizo, tunawasumbua mpaka inafika hadi tunawanyang'anya mpaka mali zao, lakini mambo yenyewe ni kwa kuwa hakuna vitambulisho vya kumtambulisha. Lakini sasa daktari akaona hili suala lina umuhimu wa *investors* kupata vitambulisho. Kwa kweli hili suala ni zuri sana mimi naliunga mkono. Lakini tatizo letu sio tufikie hapa kusema tu, ipite sheria tuifanyie kazi, hii kazi ifanyike mara moja kwa uadilifu kabisa.

Lakini tuende kwa watendaji. Mhe. Spika, juzi nimshukuru sana Dk. Shein amewapa semina nzuri ya jinsi gani sasa hivi tunataka tuelekee. Hizi semina jamani zimewasaidia sana Mawaziri, Manaibu, Makatibu na Wakurugenzi wetu. Mimi naamini watabadilika basi tusiendelee kuwashtumu tu, semina imewajenga ujengefu mzuri sana. Sasa kila siku tukiwa tunawashtumu tu tutakuwa hatuna kazi ya kufanya, lakini tuende pahala tuone panapo makoseo tupaseme na tuparekebishe na ndio wajibu wetu.

Mimi siku zote nakuambia Mhe. Spika, panapo makoseo sitopanyamazia kimya nitaeleza, baada ya kufuatilia nitawaeleza hapa wala simuogopi mtu. Mhe. Spika, ni kweli nikubaliane na Waheshimiwa Wawakilishi kuwa hatuwaelimishi wananchi wetu kuwaambia maana ya kitu. Suala la sensa ndio ni sawa sawa na hii mantiki yake. Sensa ilitupa shida sana, lakini kumbe sensa ina mantiki yake nzuri na inasaidia, ndio maana unaweza kujua wewe nchi yako kuna watu wangapi na utaweza kupanga mipango yako ya kuinua uchumi na ukajua kwa uhakika. Lakini tukiwaambia watu wasiende kujiandikisha ni hasara kubwa, halafu isitoshe kukiwa na uchaguzi wale wale wanazunguka aah! Tumeibiwa, mmeibiwa vipi wakati nyinyi wenyewe hamkwenda kujiandikisha mtajua vipi. Ukweli tuseme Mhe. Spika, kwa sababu kuna hatari yake ya kuwakataza watu bila ya kuwafahamisha athari zake na faida zake. Hili ndio jambo ambalo lilitukuta Mhe. Spika. Suala la kuwa na vitambulisho ni muhimu na suala la kujiandikisha kwenye sensa ni muhimu.

Lakini vile vile Mhe. Spika, niseme kwamba bado mimi napiga kelele kwamba sheria mmeilegeza, kwa sababu kuna watu Mhe. Spika, wamejiandikisha mara mbili na mpaka leo wengine hawajachukuliwa sheria wapo, hata kama wengi lakini bado sheria mimi nasema haijachukua ipasavyo mkondo wake.

Mhe. Spika, kuna mtu anaondoka hapa anaitwa Haji Juma, anakwenda Wete anaitwa Makame Mshimba, hebu ona wewe mwenyewe Mhe. Spika. Sio uongo, nakuambia watu wanakwenda na sayansi na teknolojia sasa hivi, huoni ile kompyuta ilivyojengwa mule ndani na zile picha. Wewe utadanganya jina, lakini kule inakataa, hivyo vitu vipo wazi nendeni Waheshimiwa Wajumbe mkaoneshwe kule jinsi inavyokwenda, ni vitu vya utandawazi sasa hivi. Kwa hivyo, hayo mambo yapo.

Vile vile nilisema Mhe. Spika, kama ni kweli wako Wakenya, Waafrika ya Kusini, lakini kutokana na utaratibu wenyewe ulikuwa vipi. Wale sasa hivi Mhe. Spika, nakuambia ukweli, wala sisemi kwa kubahatisha, mimi mambo yangu sisemi kwa kubahatisha hapa. Nasema kitu ambacho kipo kwa uhakika kabisa.

Mhe. Spika, sasa hivi asilimia imepungua sana, wengi wamepungua sio masihara wamekimbia kabisa. Hawa wanaopigiwa kelele hapa hakuna sasa hivi kabisa. Kwa hivyo, mimi nafurahi sana kwa sababu sasa hivi wenzetu wako nje Marekani na Uingereza, lakini wakiwa na uhakika wa kuwa na kitambulisho basi wale wenyewe watajisikia raha kumbe kwetu kule na wazee wetu wametujali na watakuwa na vyeti vile vya uhakika. Mimi nafikiria tumekwenda pahala pazuri sana.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 ukurasa wa 219, kuhusu muajiri mkaazi asiyekuwa Mzanzibari atatoa taarifa za mtu. Sasa hizi ndizo tunazopingana nazo sisi, tunaona shida na tunaona tabu. Ndio hapo mtu anapokuambia, mimi mtu wa hapa nimezaliwa hapa. Ndio kwani ukimuambia mimi nimetoka kwa Sheha Juma au ukachukua barua ukamuelekeza kwamba mimi ninatoka kwa Sheha Juma nimekuja kwa Sheha wewe Makame, kuna tatizo gani Mhe. Spika. Tatizo ni taarifa tu, tusiogope taarifa. Kama wewe una nia nzuri kwa nini unaogopa kutoa taarifa.

Mhe. Spika, suala la vyeti vya kuzaliwa nimuambie Mhe. Abubakar. Binadamu humshindi kwa mbinu, nalo hilo linatokea kule linakuja zake kwenye vitambulisho. Sheha anaingia hivi hivi kichwa kichwa, anaona mimi nimeshapewa cheti cha kuzaliwa kile na watu wa siku hizi mishahara yenyewe midogo wanayopewa wasiibe. Lakini nashukuru sana sasa hivi mishahara mizuri kwa kiasi cha uzuri na wataendelea kuongezwa zaidi mshahara ili watu wasiendelee kuiba.

Dk. Mwinyihaji umeilinda sera ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake ndio huu. Mhe. Spika, mimi nasema wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wanaunga mkono sana mswada huu ulioletwa na Waziri mwenyewe muhusika hawana tatizo nalo, wamekubaliana nao na mimi nasema naunga mkono, kama itawezekana niwekewe kwa asilimia 200. Lakini mimi nasema naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia kutokana na mswada huu. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 5 mwaka 2005 na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Vile vile nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi alioufanya jana na ninawatakia kila la kheri wale wote waliochaguliwa katika utekelezaji wa majukumu mapya. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nampongeza Waziri pamoja na watendaji wote ambao wameandaa mswada huu. *(Makofi)*

Kwa kweli serikali ina nia nzuri kabisa kwa kuandaa mswada huu, mswada ambao utasaidia kuweka utaratibu bora wa kumtambua mzanzibari, pia utasaidia upatikanaji wa huduma tofauti zinazotolewa. Mhe. Spika, mswada huu utasaidia pia kuwatambua wazanzibari wote wasiokuwa wakaazi wanaoishi hapa Zanzibar, pamoja na kuiwezesha serikali kupanga na kufuatilia kwa ubora zaidi na sio tu shughuli za kiuchumi na hata zile za kijamii. *(Makofi)*
Mhe. Spika, ili mswada huu uweze kutekelezeka, nashauri kanuni zifanywe haraka kutengenezwa kwa ajili ya kuleta manufaa katika nchi yetu pamoja na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakumbuka katika kipindi cha bajeti Mhe. Waziri alitueleza kwenye hotuba yake kwamba kuna wilaya ambazo hadi hivi sasa vitambulisho hawajaenda kuvichukua, na akatutajia takwimu hasa vitambulisho vyenyewe. Kwa hiyo, ninaposikia kuwa vitambulisho vinatolewa kwa ubaguzi kwa kweli nashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kumnukuu Mhe. Saleh Nassor Juma aliposema kwamba vitambulisho vinatolewa kwa ubaguzi kama vile wanapewa Wachaga, Wandengereko, Wangoni ndio ni haki yao, kwa sababu kuitwa Mngoni au Mndengereko wakati amezaliwa hapa ni Mzanzibari huyo.

Kwa mfano, ukinitizama mimi utaona huyu Marina kwa umbile lake utasema ni Mbara, lakini mimi ni Mzanzibari na mama yangu ni Mzanzibari, kwa sababu mama yangu amezaliwa mwaka 1932 hapa Zanzibar na mimi nimezaliwa mwaka 1964. Kwa hiyo, usinibague ukasema labda Mndengereko au Mchaga ukasema si Mzanzibari, kwa sababu Mzanzibari ni yule aliyezaliwa. Kwa maana hiyo, suala la ubaguzi hapa naomba tuliache. *(Makofi)*

Hivyo, naomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwahimiza wananchi wao kuvifuatilia vitambulisho vyao kwenye sehemu husika na sio kuwapotosha wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu. *(Makofi)*

**Farida Amour Mohammed:** Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kwa kuchangia machache kuhusu Mswada huu wa Marekebisho ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, mswada huu umefafanua mambo mengi, na katika ufafanuzi wake Mhe. Spika umeweka masharti maalum, masharti yake aliyoweka Mhe. Waziri hapa au sheria ilivyoweka masharti haya ni kuwa mtu awe na umri usiopungua miaka 18, awe mzanzibari, awe na makaazi ya kudumu.

Sasa kama hivi ndivyo Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba bado baadhi ya watendaji wake hasa masheha hawajawa tayari kutoa haki hii kwa wazanzibari. Vile vile baada ya Mhe. Waziri kutoa kauli thabiti hapa kwa nia safi ya kutoa vitambulisho na wao wanafuata maagizo mengine kinyume na unayoyatoa wewe hapa. *(Makofi)*
Kutokana na hali hiyo, naomba nimueleze Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kama wapo watu makundi kuanzia miaka 45 mpaka 80 na zaidi, ambao ni wazaliwa wa Pemba na wala hawajawahi kutembea hata kwenda Dar-es-Salaam hawakujui.

Kwa hivyo, watu hao wameambiwa hawa vyeti vya kuzaliwa, basi tumefuatilia na tumekwenda na tukaambiwa tukatafute *affidavit*, mimi binafsi nimefuatilia watu hao na wamekwenda mahakamani, lakini mpaka leo hii Mhe. Spika wameshindwa kupewa vitambulisho hivyo vya uzanzibari. Kwa mfano, wanapokwenda kwa Sheha au wilayani wanapigwa danedane.

Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Waziri kupitia kwako, kwamba yeye ndiye *mas-uli* wa suala hili, kama moto huu unaowaka katika Baraza la Wawakilishi kila siku zogo, malumbano ya muda mrefu kuanzia mwaka 2005 tulipewa vitambulisho hivi.

Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba mwaka 2005 baadhi ya Wajumbe au wananchi walizembea au walikataa kwenda kuchukua vitambulisho hivi lakini kwa sababu maalum.

Kwanza walikuwa hawana elimu hawajajua umuhimu wa kuchukua vitambulisho hivi, lakini baada ya kuelimishwa na serikali pamoja na sisi Wawakilishi wao kipindi hicho bado hatujawa Wawakilishi, basi tuwaelimishe watu hawa kujua umuhimu na kila mmoja akajua umuhimu wa kitambulisho hichi, kwamba kitambulisho hichi ni nusu ya maisha ya mwanadamu. Kwa hivyo, tayari watu hawa wameelimika na taratibu wamezifuata, lakini kuanzia mwaka 2005 Mhe. Spika mpaka leo 2012.

Je, kwa sababu watu hawa walikataa hapo nyuma kwa sababu ya kutoelimika, sasa wameshaelimika na tayari wameshajua umuhimu wa vitambulisho hivi, bado wanaendelea kupewa adhabu na mpaka lini watu hawa kushindwa kupewa vitambulisho vya uzanzibari Mhe. Spika.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba alisimamie hili kwa nguvu zake zote, sisi hapa hatutaki malumbano na tutaendelea kulalamika, kwa sababu tunachokilalamikia bado hakijafanikiwa.

Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Waziri kuwa atakapolisimamia hili sisi hatuna tatizo na mgeni yeyote kuja hapa na kupewa kitambulisho, kwa sababu hakuna nchi hata moja duniani wanayoishi wazaliwa peke yao, isipokuwa nchi zote wanaishi wageni na wanazo faida na hasara zao.

Jambo la msingi almuradi wageni wale wakifuata sheria za nchi kama sisi tunavyoishi kwenye nchi za watu hatuna matatizo seuze sisi watanzania ambao Unguja na Pemba na Dar-es-Salaam ni moja, kwa nini tukatae wageni. Lakini kwa sababu wazanzibari waliopo hapa Mhe. Spika wameshindwa kupewa haki hiyo mpaka leo lazima watu walalamike. *(Makofi)*

Kwa kumalizia Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kila anayesimama hapa sina lengo la kujibu wanazungumza habari ya sensa kuwa tumekataa sensa.

Kwa ushahidi ulio wazi Mhe. Spika, mimi binafsi na Wawakilishi wote tunaotoka Kisiwa cha Pemba tumepita nyumba kwa nyumba kwa ajili ya kuhamasisha watu wajiandikishe kwenye sensa, na matusi makubwa tuliyokuwa tukitukanwa, tulikuwa tukiambiwa nyinyi mnatuandikisha sisi kwenye sensa wakati kitambulisho cha uzanzibari tunashindwa kupewa hatutaki, basi tuliwalazimisha pamoja na kuwaelimisha na asilimia hiyo iliyopatikana tumeshiriki kikamilifu katika hilo. Kwa hivyo, nawaomba wenzangu wasituelewe kama sisi hatufuatilii, kwa kweli tunafuatilia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako kwamba ataona haya ninayoyasema ni kinyume, basi baada ya kumaliza kikao hichi cha Baraza tufuatane mimi na yeye nimpeleke ndani ya wilaya pamoja na shehia zangu, kwa ajili ya kwenda kumuonesha watu ambao tayari wameshatimiza masharti, lakini mpaka leo bado hawajapewa vitambulisho vya uzanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri atalisimamia hili kikamilifu basi Zanzibar yetu itakuwa haina matatizo wala tabu na tutaishi kama ndugu na wala hatutarejesha tena yale tuliyokuwa nayo nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, nakushukuru sana jioni hii ya leo kunipa na mimi fursa ya kuchangia mswada huu wa vitambulisho uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli Wajumbe wako tuliomo ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, sote humu hamna mwendawazimu naamini kwamba sote ni watu wenye akili timamu. Mhe. Spika, ukimuona mtu suala moja analirudia kila siku suala hilo hilo, basi ujue suala hilo lina matatizo. Kwa hivyo, sisi humu hatujaugua wazimu sote ni watu wazima wenye akili timamu.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi bajeti zaidi ya mara mbili zinazopita mimi binafsi nazungumza kuhusu suala hili la vitambulisho kwa Mhe. Waziri. Lakini Mhe. Spika, tunapokuja kusema tunasema kwa ushahidi kamili na wala hatusemi tu kama ni wendawazimu, isipokuwa tunasema kwa ushahidi kamili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lazima tuambizane kweli humu, kwa sababu hili Baraza ni la wananchi, ambapo wananchi wote wanatuangalia sisi ambao tumo humu na kila siku tunasema Mhe. Spika, kwamba kila mmoja atakwenda kuulizwa kutokana na lile analolifanya au alilokabidhiwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, sisi tunasema kama viongozi ni *mas-uli* tutakwenda kuulizwa kutokana na uongozi wetu tunaoongoza.

Mhe. Spika, kwa nini vitambulisho hivi tunaviingiza kwenye mambo ya siasa na kuwanyima watu haki zao na Mwenyezi Mungu atakwenda kutuadhibu kwa sababu hizi ni haki za watu.

Kwa kweli vitambulisho bado havitolewi katika wilaya zetu hasa Wilaya yetu ya Micheweni imezidi, ambayo ina matatizo makubwa sana na hawa masheha inakuwaje vitambulisho. Kwa mfano, mtu anacho cheti cha kuzaliwa pamoja na ushahidi kamili kwa nini anyimwe kitambulisho, jamani vitambulisho tusiviingize kwenye siasa, kwa sababu hivi sasa tumevifanya ni muhimu kwa kila kitu. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, tunapokuja kuzungumza wenzetu wanasema mimi jimbo langu mbona watu wamepewa, lakini langu mimi hawapewi haya tuende kama kuna ushahidi kama wangu mimi hawapewi, wako wewe wanapewa kwa sababu vimeingizwa kwenye siasa na wangu mimi hawapewi kwa hilo tatizo la siasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo la siasa kama mtu anajilinda basi hawezi kujilinda, kama mtu anajilinda basi angejilinda Firauna. Mhe. Spika, Firauna alitawala miji mia 600 katika ulimwengu na yeye akafika pahala na kusema mimi ndiye mungu mtukufu na wala hakuna mungu mwengine isipokuwa mimi.

Lakini tizama Mwenyezi Mungu alipotaka kuuondoa ufalme wake Firauna, basi alizaliwa Nabii Mussa katika mji wake na alimlea yeye nyumbani mwake, kwa ufalme wa Mwenyezi Mungu kwa sababu anataka kuondoa ufalme wake, basi alimlea Firauna Nabii Mussa na ilikuwa mtu yeyote anayezaliwa katika mji wake mtoto wa kiume

anauliwa, lakini yeye alimlea yeye mwenyewe Firauna, kwa sababu Mwenyezi Mungu anataka kuondoa ufalme wake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, jamani tusiwaadhibu watu na tumeleta sheria ili ziwanufaishe wananchi, na leo sheria tunazozitunga zinawaangamiza wananchi wetu, sheria za kukandamiza hazifai katika nchi na kwa nini tusiwaambie ukweli humu, kwa nini tukisema ukweli tuonekane sisi tunasema tu humu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu alipomjaalia akazaliwa Nabii Mussa, basi mama yake alisema mtoto wa kiume yeyote anayezaliwa katika mji huu anauliwa, mama yake alisema ni bora nimtie kwenye sanduku nikamtupe baharini, basi alichongewa sanduku na kuingizwa kwenye sanduku na baadaye kutupwa baharini.

Mhe. Spika, sanduku lile lilielea moja kwa moja mpaka kwa Firauna chini ya bahari, kuokotwa lile sanduku lina mtoto, alipokwenda Firauna akasema auliwe huyu. Lakini akatokea mtu akamwambia utamuua unajua anatoka nchi gani huyu, basi alimlea mwenyewe Firauna Nabii Mussa, ulipofika muda basi yeye ndiye aliyemuondoa.

Kwa hiyo, jamani tusione kwa sababu sisi tunafanya hivi siasa na kuwakandamiza watu kwa kuwa tunajinufaisha kisiasa. Kwa kweli Mwenyezi Mungu anasema kwamba ukifika muda itatokea sababu ndogo na utaondoka tu moja kwa moja.

Jambo jengine tukumbuke kwamba sisi tunakwenda kuulizwa tukifa, na ufalme wako ulimwenguni uliwatendea vipi haki wenzio. Kwa hivyo, sisi tunafanya kama ni mchezo huu tunawaadhibu watu. *(Makofi)*

Katika nchi hii kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba kuna watu wameandikishwa zaidi ya mara nne na sio mara mbili, na mimi nimeona juzi kwenye uchaguzi wa Bububu. Kwa hivyo, juzi uchaguzi wa Bububu mnasema mawaziri walikwenda kwenye uchaguzi Bububu, ee walikwenda mawaziri na watu walipigwa risasi, je kama wangekwenda watu kiholela, waseme vipi mawaziri na wao walikwenda kuangalia tu. *(Makofi)*

Lakini pamoja na mawaziri kwenda hawakuheshimiwa na watu walipigwa risasi, na sisi ambao sio mawaziri tunaambiwa tupigwe bakora na tulinusurika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Sasa leo mnasema wamekwenda mawaziri, ndio kwani wamekwenda kusimamia ile haki ya watu na wala hawakwenda kwa ajili ya kufanya uchafuzi, na wala mawaziri hawakuheshimiwa je kama wangekwenda watu tu kiholela, jamani nchi hii hasa tunaipeleka wapi. *(Makofi)*

Tumesema kwamba tunayo Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Maridhiano na tumekaa humu tunashauriana pamoja na kufanya kazi zetu bukheri, basi jimbo moja tu limetutoa imani, jamani tunaelekea wapi. Kwa kweli tufanye uadilifu pamoja na kutenda haki.

Mhe. Spika, hivi sasa vitambulisho ni haki ya kila mmoja, na leo mnatuletea mswada huu tuwape wageni vitambulisho wakati wenye nyumba bado hawajapa jamani. Kwa mfano, leo nyumbani unacho chakula na watoto wako nyumbani hujawapa na unawatafutia watu wengine unawapa, hivi tunakwenda wapi jamani na mimi mswada huu siukubali, kwa sababu watu bado hawajapewa vitambulisho na hawa wenyewe hawajapewa.

Sasa leo hawajapewa wenyewe mnasema tuwape wageni vipi tunawaandalia wageni wakati wenyeji bado hawajapewa. Kwa nini tunaona tabu gani kurekebisha sheria kwamba wananchi wa Zanzibar kila mwenye haki kwa utaratibu maalum, yaani mwenye haki yake akapewa, lakini watu wote wanaitwa wageni na mtu amezaliwa hapa, baba anacho kitambulisho na mama hana, au mtoto anacho kitambulisho na baba hana kitambulisho.

Kutokana na hali hii, tunaelekea wapi ndugu zangu na wazee wangu jamani tufanye uadilifu eee! Hii nchi ni yetu sote na wala si ya mtu mmoja, kwa nini tunafanya hivi ubaguzi, na mukiambiwa munasema hakuna ubaguzi. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk anasema jimboni kwake watu wanapewa vitambulisho na mimi kwangu hawapewi kwa nini, kuna watu wanavyo vyeti marundo na wala hawapewi, kwa nini tunafanya hivi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sikubaliani na mswada huu, kwa sababu kwanza labda kwa kuwa Mhe. Waziri kila siku ananiweka kwenye *line*, ananiambia hivi na ikifika muda hatekelezi. Kwa hivyo, labda tuondoke mguu kwa mguu, ili wale watu wangu ambao hawana vitambulisho basi wapewe vitambulisho ni haki yao na wao kwani si wazaliwa wa nchi hii, hivi kwa nini tunawabagua watu kwenye nchi hii, na hasa hivi vitambulisho vyetu tuliviita vya

mzazibari kwa nini, kwamba anayekuja kutoka nchi nyengine afike hapa siku mbili apewe, lakini wale wanaozaliwa hapa wasipewe. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, leo vitambulisho tunaviita vya mzanzibari mkaazi kwa shabaha maalum, na mimi nasema hii ni mbinu maalum, yaani hivyo kuitwa vya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni mbinu maalum kwa sababu wakija watu wanaokaa siku mbili ambao mna imani nao muwape, lakini wale ambao hawana imani nao wanaitwa wageni, eti wazaliwa na nchi hii ni wageni na wanaokuja jana ni wenyeji. *(Makofi)*

Hivi tunaelekea wapi na tunasema kwa hasira na wala hatusemi kwa hasara, isipokuwa tunasema kwa sababu inatuumiza ndani ya nafsi yetu, kwa kuwa hii nchi ni yetu pamoja. Kwa mfano, mimi niliwauliza kipindi kilichopita munipe tarehe iliyounganishwa Visiwa vya Unguja na Pemba na wala sikupewa tarehe, kwa sababu gani ni nchi moja tokea Mwenyezi Mungu alipotuumba ametuweka pamoja. Sasa kwa nini tufanye hivi na watu wasipewe vitambulisho wazanzibari wenyewe, lakini wageni wanaandaliwa wapewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nikae kitako na wala simo. *(Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari. *(Makofi)*

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunifikisha salama muda huu kuweza kuchangia mswada huu ambao ni mzuri na halafu unatupa nafasi sote wananchi wa Zanzibar kuweza kuwa na vitambulisho halisi vya mzanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nakataa kwamba hakuna mzanzibari ambaye anakosa kitambulisho, labda hafuati sheria ambazo zimepangwa na Serikali ya Zanzibar, kwa sababu Mzanzibari yeyote anayo haki ya kupata Kitambulisho cha Mzanzibari. Kwa mfano, ikiwa tunasikia hotuba za viongozi wetu basi tungejua kwamba hakuna Mzanzibari hivi sasa ambaye hapati Kitambulisho cha Mzanzibari, mwenye kufuata zile sheria zilizowekwa na Serikali ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hivyo, napenda kujuilisha kwamba Wazanzibari wote wanatakiwa wapate vitambulisho kwa kupitia masheha wao ambao wapo katika wilaya, majimbo pamoja na vijiji vyao. Lakini nashangaa sana wenzetu wengine ambao wanaokataa makwao.

Kwa mfano, mimi kwetu shamba Kaibona siendi kuchukua utambulisho wangu kutoka Kaibona, nasema lazima niwe mtu wa mjini Unguja, kwamba naishi kule Jimbo la Mji Mkongwe kumbe vile ninako kwetu na wala siendi. Kwa hivyo, vipi Sheha atanifahamu kwamba mimi nahusika kupata Kitambulisho cha Mzanzibari.

Sasa ikiwa mimi mshamba siendi kwetu Mzanzibari, je ndugu zetu wa Pemba wapo pale Mji Mkongwe na wala hawaendi Pemba kuchukua kwa masheha wa Pemba, sasa atapata wapi Kitambulisho cha Mzanzibari, kwa sababu tunasema mtu kwao.

Kwa hivyo, mtu kutoka Pemba aende kule Chokocho akachukue kwa Sheha Kitambulisho cha Mzanzibari, na sio aende Mji Mkongwe kusubiri Kitambulisho cha Mzanzibari. Kutokana na hali hiyo, siku zote watasema wananyanyaswa na wanasemwa, basi ni vyema wafuate sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nampenda sana kiongozi wetu Makamo wa Kwanza wa Rais anavyowaelimisha wenzetu, na jana nilisikia hotuba yake akifahamisha kwamba hakuna kitu kinachopangwa na serikali kisiwe na maana. Kwa hivyo, kitu chochote kinachopangwa na serikali ujue kwamba kina maana, ndio jana aliwasisitiza wenzetu kuwa Kitambulisho cha Mtanzania ni muhimu kwamba uwepo Tanzania upate Kitambulisho cha Mtanzania ndio utakuwa Mtanzania. *(Makofi)*

Sasa anaweza kutokea mtu ambaye akajipa madaraka kwamba na yeye anayo sauti kwenye serikali na kuwaambia ndugu zetu msichukue Kitambulisho cha Mtanzania, hivi utamlaumu nani. Vile vile Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad alisema, kwamba usiwe mjinga akili ya kuchangiwa ongeza na yako, siku zote mtakuwa nyuma kwa kuwa mnakuwa na akili za kuchangiwa. *(Makofi)*

Kwa mfano, mtu anatoka Qatar anakuja Zanzibar na kusema yeye ni Mzanzibari anaitetea Zanzibar, ataitetea vipi Zanzibar na yeye ni mtu wa Oman, hivi nani asiyemjua kwamba ametoka Oman na ataitetea nini Zanzibar, isipokuwa anawapotosha Wazanzibari. Kwa kweli Wazanzibari wote wanapata haki zao kupitia njia ya masheha na ukifika kwa sheha hutakosa Kitambulisho cha Mtanzania na wala kile cha Zanzibar na tarehe zinawekwa.

Mhe. Spika, naomba kuwakumbusha wenzangu tarehe ya Kitambulisho cha Mtanzania itawekwa na kama mtu hakwenda kuchukua tarehe ikiwekwa, kama mtu hakwenda kuchukua wakati tarehe itakapowekwa asije kulaumu Serikali ya Tanzania, atakwenda Oman ndiko kwao. *(Makofi)*

Wazanzibari pamoja na Watanzania asili yetu sote hapa tunajuana, kwamba Mzanzibari yeyote anasema Zan na Bar, yaani Bara na Zanzibar ndio nchi moja Mmakonde, Mnywamwezi, Mswahili ndio Mzanzibari na sio Mwarabu, Mwarabu aende Oman akachukue utambulisho na sio awapotoshe Wazanzibari wasipate vitambulisho.

Mhe. Spika, leo unajitambua wewe mtu ni mzanzibari unawatambulisha kwamba usichukue Kitambulisho cha Mzanzibari na matokeo yake unawapotosha wananchi, na ukiwapotosha unawahangaisha wananchi kupata vitambulisho vyao. Kwa hivyo, nawahakikishia wananchi kama utafuata njia zinazotakiwa kupitia kwa masheha basi hutakosa kitambulisho cha Mzanzibari pamoja na haki zao, kwa sababu haki yako umepangiwa lazima upate. *(Makofi)*

Kwa mfano, mimi mwenyewe hapa ninacho kitambulisho changu cha shamba, na mimi ni Mkaibona pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Koani, lakini asili imetoka Makunduchi na Kaibona vipi nitakataa nyumbani na nitapata wapi utambulisho. Mhe. Spika, mtu anaweza kuuliza kwa Sheha wangu kama hanifahamu, sababu zangu za kwenda kuchukua pale kwa sababu ninayo asili ya kwamba nipate kitambulisho.

Kwa hivyo, wananchi wote wanajuilisha kwamba kuanzia leo waende sehemu zao, kwa sababu mtu kwao na wala usikatae kutoka Chokocho na kusema kwamba hukujui na wewe ni mtu wa Mji Mkongwe kule vile unakataa asili yako. *(Makofi)*

Sasa wewe unasema kwamba watu wanapigwa katika Jimbo la Bububu, unatoka Micheweni uende Bububu inakuhusu nini na pale pametakiwa kila mtu aende mwenye asili ya Bububu, ndio utakwenda pale na usiwahangaishe watu, lakini wewe umekwenda kuwachafua watu kwa makusudi. *(Makofi)*

Kwa mfano, wewe umetoka Micheweni mpaka Bububu umekwenda kufanya nini na sheha anakujua. Kwa hiyo, tumia nafasi yako ya kwamba wewe ni Mzanzibari tumia haki yako sehemu yako, na hivyo itakuwa siku zote unapoteza haki zako na kusema kwamba unaonewa ama unadhalilishwa na wala huwezi kudhalilishwa kama utatumia haki yako unayotakiwa ya Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na wala sipendi kutumia muda wako mwingi, isipokuwa hutaka niwaambie ukweli. Vile vile nimesikia hotuba yako jana ya kuwafahamisha Wazanzibari wasipoteze haki zao pamoja na Utanzania wao.

Kwa hivyo, ni vyema watu wachukue ya kuchangiwa pamoja na yao wenyewe na waachane na watu ambao wanajipa madaraka ya lazima ambayo hayawahusu, kwa sababu hata Mwenyezi Mungu mwenyewe anampa riziki yake, pia kila mtu amempa uwezo wake, na Mwenyezi Mungu ametoa nafasi kwa kila mtu amempangia haki yake hadi kufa kwake.

Kwa maana hiyo, wewe usijipe madaraka ya kwamba unayo haki ya kuweza kuwatawala watu wakati Mwenyezi Mungu hajakupangia, unajihangaisha na wala hutambuliki.

Mhe. Spika, nasema kwamba Vitambulisho vya Zanzibar ni haki yetu, vijana, wazee, wanawake na wanaume wafuate sheria, ili wapate haki zao, masheha wako wazi. Kwa hivyo, sheha yeyote ambaye atakwenda mwananchi na hamtekelezei basi iko haja ya kushtakiwa kwamba anadhalilisha nchi yetu, kwa sababu masheha wote wamefunzwa na wamesomeshwa vipi kuwapatia wananchi haki zao. *(Makofi)*
Mhe. Spika, zaidi ya yote ni kwamba nawataka wananchi wa Zanzibar watumie haki zao, waache jazba, Zanzibar ni yao na wala hawana pa kwenda kwengine, na popote watakapokwenda watarudi Zanzibar, na Zanzibar inataka kuongozwa na Wazanzibari na Watanzania tunaongozwa na Tanzania. *(Makofi)*

Baada ya hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Salim Abdalla Hamad, ulitaka kutoa taarifa.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru sana Kanuni yetu ukurasa wa 44 kifungu cha 59(3) naomba kunukuu kidogo:-

Kanuni za Baraza kifungu cha 59(3) kinaeleza hivi:-

> "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo aliyesema atoe uthibitisho kwa usemi wake unaohusika".

Sasa Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako, kwamba amezungumza uzuri kwa hamasa na maneno mazuri. Lakini kwenye mazungumzo yake amesema kuna baadhi ya viongozi wa serikali kama nilivyomsikia mimi kama nimemsikia sawa sawa, wanawaambia Wajumbe wao wasiende kuchukua vitambulisho. Kwa hivyo, kama ndivyo nilivyosikia basi naomba nijue ni kiongozi gani huyo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri bila ya kwenda kwenye Kanuni masuala haya tuyaache, kwa sababu kwa wananchi kumevurugika huko na wavurugaji ni kati ya wananchi sisi wenyewe. Kwa hivyo, tusiende huko kwenye na mswada wetu huu. *(Makofi)*

Naomba sana nimkaribishe Mhe. Hija Hassan Hija na baadaye Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, kwa dhati ya nafsi yangu naomba nikushukuru na naomba nianzie hapo kidogo ambapo umetupatia mawaidha. Nakushukuru kwa sababu nilikuwa na mawazo kwamba niwaambie Wajumbe wenzangu kuwa wasichokozeke, muhimu tujenge hoja na wananchi watapima na Mwenyezi Mungu yeye ndiye atakayehukumu. *(Makofi)*
Kwa hivyo, hatuna haja ya kuweka *point of order*, ili tujenge hoja kwa ajili ya kuweka nidhamu ndani ya Baraza, na bila ya shaka Wazanzibari si wajinga na wanatuelewa tunafanya nini.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyotujaalia uzima, pia nikupongeze Mhe. Spika kwa jinsi unavyoendesha Baraza hili.

Vile vile nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar kwa uteuzi wake aliofanya jana kwa kuteuwa Manaibu Waziri wawili na Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum.

Mhe. Spika, kwa hakika mimi ni miongoni mwa watu waliofurahi katika uteuzi huu, kwa sababu uteuzi wake umesibu. Pia uteuzi huu umetupunguzia sisi ambao tumeamua kusema kwa ajili ya wananchi kupumua. Kulikuwa kuna watu wamegeuka fisi, waliopata habari kwamba Mhe. Rais huenda akateuwa Manaibu Waziri walikuwa wanajipendekeza. Mapandekezo yao ni kwa ajili ya kuwafitinisha wenzao kwamba huyu mbaya na huyu hafai. Bahati nzuri wale wote waliokuwa wakijipendekeza Mhe. Raisi hakuwaona na ameteuwa watu wengine wapya na makini ambao ndio watakuwa Manaibu Waziri.

Mimi naomba Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nimshukuru sana Mhe. Rais kwa uoni wake. Baraza hili halendi kwa fitna, mwaname, mwanamke mwenye hoja ajenge hoja wananchi wapime. Sio utumie tamaa yako ya maslahi ya uongozi na kufanya fitna kwa wengine. Kila mtu hapa ana jimbo na kila mtu amechaguliwa kwa niaba ya wananchi. Kwa hivyo wale wenye tamaa ya fisi kwamba mkono ukatike apate nyama nadhani wameumbuka na namshukuru sana Mhe. Rais.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa niende kwenye Mswada wenyewe na nianze kutoa mchango wangu kwenye sababu na madhumuni. Mimi nadhani niseme tena sio kwa jazba niseme kwa hoja. Kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais anaendelea kututania. Maandiko hayo unapoyatoa na kuwaeleza Wazanzibari na dunia inahitaji kuwa na

umakini mkubwa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anasema kwamba sababu na madhumuni ya Mswada huu kuwa, kwanza zoezi la usajili limeonesha kuwa la mafanikio.

Nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kiwani kusikitika sana kwamba Mhe. Waziri kwamba haya aliyaandika kwa nia safi *Wallahi Laadhimu* niseme kwamba ameteleza. Sheria hii iliyopo tangu siku ya mwanzo iliyoanza kutumika haina mafanikio. Kwa maana kwamba Wazanzibari waliowengi wamekosa kupata haki yao bila ya kuangalia utashi wa kisiasa. Kama kweli viongozi wapo hapa kwa ajili ya watu hii ni hoja ya msingi. Sababu hii ni kwamba Mswada uliopita unamafanikio nadhani Mhe. Waziri hili hakusema kweli na halina ukweli wowote.

Mhe. Spika, sababu nyengine anasema kwamba Wazanzibari wakaazi wasiostahiki kusajiliwa, kutafuta usajili kwa kutumia mbinu za udanganyifu. Hili naliunga mkono kwamba kweli kuna Wazanzibari wasio wakaazi wanatumia mbinu zao za udanganyifu kwa kupata vitambulisho. Mhe. Spika, mimi kama kawaida yangu nimeendelea kufanya utafiti na Mhe. Waziri hili namuunga mkono kwamba kweli kuna Wazanzibari waliokuwa sio kweli wanatumia Afisi yake kwa maana ya Masheha na kuwasajili Wazanzibari kupata haki hii ya watu kwa udanganyifu. Ninao ushahidi kwamba kuna watu wamedanganya vyeti vya kuzaliwa, kuna watu wamedanganya mpaka vyeti vya ndoa hatimaye ofisi yake imetoa haki hii kinyume na sheria.

Pointi hii Mhe. Spika, namuunga mkono kwamba amesema kweli. Kwamba kumbe anawajua kwamba kuna watu wanatumia fursa hii ya udanganyifu kunyima haki za Wazanzibari pasi na sheria, lakini ajiulize yeye kama Waziri amechukua hatua gani. Anawajua kwamba kuna watu wadanganyifu atwambie leo amechukua hatua gani ya kuwadhibiti wahalifu hawa ambao wamedanganya taifa kwa ajili ya kupata haki iliyokuwa si yao. Sio kusema tu, kusema ni jambo jengine na kuchukua hatua ni jambo jengine.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atwambie basi kwa kuwa amekiri kwamba kuna watu wanafanya udanganyifu kupata haki ambao si zao, atwambie yeye kafanya nini. Mimi ninayo ripoti mpaka ya Uhamiaji kwamba kuna watu wamefanya udanganyifu lakini yeye kama ni Mhe. Waziri amechukua hatua gani, si kusema tu, hii ni nchi ambayo inasheria. Kwa kuwa amekiri kwamba kuna watu wamefanya udanganyifu, yeye ni waziri tuliyemuamini kumpa Ofisi ya Rais amechukua hatua gani kuwadhibiti watu hao ambao wamefanya ufanganyifu.

Jengine Mhe. Spika, kwamba mtandao huu wa usajili kwenye udanganyifu unakuwa mkubwa. Kwa upande mwengine serikali kwa madhumuni, uchumi na mipango ya nchi na jamii, inahitaji kutambua Wazanzibari kwenye maeneo ya taaluma, takwimu na hali nyengine. Ni kweli kabisa Mhe. Waziri anatambua kwamba hawa wanaofanya udanganyifu ndio hawa hawa ambao wanachukua sekta za ajira zote hasa mahotelini.

Mhe. Spika, ninayo orodha kwamba wale wote ambao wamepatiwa ZAN ID ndio walioajiriwa katika sekta ya utalii, huku serikali wakitwambia kwamba Wazanzibari hawapati haki ya ajira kwa sababu hawana elimu. Ninao ushahidi kwamba kuna watu wamefoji mpaka vyeti vya skuli leo ni ma–PO kwenye Mahoteli yetu hapa Zanzibar. Kumbe serikali kwamba kuna watu wanaghushi vyeti na wanaajiriwa. Leo unatwambia nini kwamba Wazanzibari hawana sifa hawakusoma. Kumbe serikali inajua kwamba kuna watu wanaghushi vyeti lakini wanawaajiri. Mswada huu kwa sababu hii nakubaliana nao kwamba Mhe. Waziri anatambua kwamba kuna watu wanaghushi vyeti lakini wanapewa haki kinyume na sheria ambayo tumejipitishia.

Mhe. Spika, kwa msingi huo sababu zote mbili ambazo Mhe. Waziri amesema mimi nazikataa. Sababu ya mwanzo amesema sababu hizo mbili zimepelekea kufanywa marekebisho ya sheria mama. Dhumuni la msingi la sheria hii ni kuwatambua Wazanzibari wote wasiokuwa wakaazi wanaoishi Zanzibar. Sawa baada ya kuwatambua Wazanzibari ambao kuwa si wakaazi kisheria Mhe. Waziri atwambie sasa atafanya nini. Hivyo tangu sheria hii tulipoipitisha hujawajua Wazanzibari ambao kuwa si halali? Wewe na Waziri wa Sheria mmefanya nini, mtwambie.

Mimi ninayo taarifa kwamba mmepewa mpaka taarifa kwamba huyu na huyu anaghushi cheti lakini Wazi wa katiba yupo na wewe Waziri mwenyewe upo, twambieni nini hatua muliyoichukua, baada ya kumgundua kwamba huyu ameghushi cheti, huyu ameghushi mpaka stakabadhi ya ndoa kuna hatua gani ambayo mmeichukua. Mtu mkubwa wa kulalamikiwa Mhe. Spika, ni Waziri wa Sheria na Waziri wa Vitambulisho kwamba mmeshindwa kuchukua hatua kwa wale watu ambao wamefanya makosa ya kijinai kwa niaba ya Wazanzibari.

Mhe. Spika baada ya kutoa utangulizi huo mimi naomba nisema maneno mafupi sana. Kwamba Wazanzibari Mhe. Spika, viongozi tumesahau, kuna haja ya kutumia kiti chako utafute shehe mzuri kidogo atupe mawaidha viongozi

tumesahau. Viongozi sisi kama Wawakilishi na Wabunge na Mawaziri pengine tumesahau kwamba kuna siku viongozi hawa watakufa kama viongozi wengine na mbele ya Mwenyezi Mungu wataulizwa.

Mhe. Spika, nina wasi wasi kwamba watu wanafikiria kwamba wataulizwa nini umevaa. Ukiulizwa nini umevaa ni rahisi kusema tu kwamba nilivaa koti au kanzu ni rahisi tu. Ukiulizwa nini umekula utasema tu kwamba nimekula pilau au biriani, ni rahisi tu. Lakini wanasahau viongozi kwamba wataulizwa nini uliwafanyia wananchi wako.

Mhe. Spika, mimi nimejiuliza sana maswali mengi tangu juzi, kwa nini viongozi kuanzia Wawakilishi, mtu anapopewa uwakilishi miaka 20 lakini akistaafu kazi kubwa anakuwa ni kuuza mikate, anakuwa hana kitu. Tathmini yangu ni kwamba viongozi sisi kuanzia Wawakilishi kwenda juu tumekuwa ni wa mwanzo kufanya dhulma kwa wananchi wetu. Kwa nini uwe kiongozi miaka 20, 30 au 40 baadaye kazi yako uuze mikate ya boflo. Ni dhahiri kwamba watu wamekosa maadili, wanafanya dhambi na Mwenyezi Mungu anatuhukumu duniani na tusubiri mbele ya Mungu tukapate adhabu nyengine. Kwa mtindo huu wa kujitia usiasa na kujitia nyie CUF na CCM tukadhulumu wananchi wetu kwa kisingizio cha usiasa, *Wallahi Laadhimu* Mhe. Spika, hatufanikiwi.

Mimi nataka nikuombe Mhe. Spika, kuna haja sisi Wawakilishi kupata mawaidha kidogo ili tumjue Mungu wetu, tujue nini tunachokifanya. Mtu anajua kwamba hili ni kosa lakini kwa sababu ana wasi wasi wa ushindi wake basi anakubali kufanya dhulma kwa ajili ya kulinda maslahi yake. Mimi nimejaribu kufatilia Mhe. Mshimba amezungumza kwamba kuna watu wameingia hapa kwa Pemba wanaingilia Msuka kutoka Kenya, wanavaa kofia na kanzu, basi Zanzibar ukivaa kofia ni muislamu. Unguja hapa watu wanaingia kwa slogan ya Umasai, ukivaa rubega yako hapo basi wewe Mmasai. Kumbe watu wanaingia kwa ajili ya kupata vitambulisho vya Uzanzibari.

Mhe. Spika, mpaka mwaka huo watu wamepatiwa haki hiyo bila ya utaratibu, leo Mhe. Waziri anatwambia kwamba eti Mswada huu lengo lake ni kuwadhibiti watu hao wakati tayari ametoa haki hii tangu miaka ya nyuma zaidi ya miaka mitatu. Sasa basi ange twambia ni watu wangapi amewakamata na kuwadhibiti na kuwapeleka Mahakamani.

Mhe. Spika, Uhamiaji walitoa barua Wizara ya Elimu na wakaomba wapatiwe uhakiki wa watu fulani kwa ajili ya uhalisia wao wa vyetu vya kuzaliwa na vyeti vya masomo. Ripoti ya Wizara ya Elimu na Baraza la Mitihani wamesema kwamba watu hao vyeti vyao wamefoji na hawapo tayari kuwa wawe wanafanya kazi serikalini. Leo serikali inajua na imewaajiri, imeaacha ndugu zetu Wazanzibari wazalendo wanakosa kazi eti kwa kuwa hawana elimu. Kama kweli Mhe. Waziri uko makini basi chukua hatua. Na mimi nasema kwamba Ofisi yako ya ZAN ID inajua *A to Z*. Wale watu ambao kuwa wanapewa vitambusho hivi wameanzia nambari maalum maana yake nini? Maana yake kwamba huu ni mradi maalum wa watu maalum.

Mhe. Spika, kama kweli serikali ina nia hiyo basi atwambie Mhe. Waziri kwamba watu hao ambao wanajulikana wanafanya nini. Nataka niseme kwamba kibaya zaidi wanaingilia mpaka Afisi ya Katiba na Sheria ili waonekane wema, wanajaribu kufoji mpaka vyeti vya ndoa. Ninao ushahidi hapa wa cheti cha ndoa na Mhe. Waziri anajua kwamba mtu amefoji cheti cha ndoa kwa kujiita yeye ni Mariyam kumbe ni Meri. Ili apate hati ya kuishi hapa amekubali kujiita yeye ni Maria na ameolewa kimizengwe zengwe na Afisi ya Waziri wa Sheria wamempa cheti cha ndoa ni hatari kubwa sana. Sasa mimi sishangai Mhe. Spika, kusikia kwamba mbwa anazaa paka, kwa sababu ikiwa ndio mtindo huu, mbwa atazaa paka na ng'ombe atazaa mtu.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba serikali hii ni kama lengo kuwafanyia haki Wazanzibari tunakubali. Na kama tatizo ni uchaguzi basi tufute uchaguzi, tuwaachie watu watawale lakini Wazanzibari wapate haki yao. Tusiwanyime haki Wazanzibari kwa sababu tu kuna uchaguzi, hili haliwezekani. Mhe. Waziri tumesema, nakumbuka mwaka jana hapa kwamba atapita jimbo kwa jimbo ili Wawakilishi tufuatane tumpatie orodha ya wale wananchi waliokuwa hawajapata haki yao. Atwambie Mhe. Waziri ni nani aliyemwambia, Mwakilishi gani alimwambia kwamba tufuatane twende jimboni kwako tukawapatie hao watu. Hii ina maana kwamba Mhe. Waziri yeye mwenyewe anakusudia kuwanyima haki Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba hii sio hoja ya kisiasa, lazima tuangalie haki za watu. Kama mzimu unaotula ni uchaguzi basi uchaguzi ufutwe, tumwambie Waziri wewe utakuwa Waziri miaka mia hapa lakini watu wapewe haki yao. Na kama hoja ni uchaguzi basi tuwaachie watu watawale mpaka watosheke baadaye watu wapate haki yao. Lakini isiwe sababu za uchaguzi ndio tukawadhulumu watu.

Mhe. Spika, leo kuna wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani wapo Bagamoyo, wamekosa tiketi ya kuja Zanzibar kwa sababu hawana ZAN ID. Sasa unamnyima mtu kupata haki yake kwa sababu tu unategemea wewe kuwa mwakilishi, uwakilishi wenyewe ndio huo wa kuuza mikate. Mimi nasema kwamba tusijivune kwa uwakilishi, tusijivune kwa uwaziri. Kuna wangapi walikuwa Mawaziri hapa leo wanaomba huko mitaani, kuna wangapi walikuwa wawakilishi miaka 40, leo wanafanya biashara ya kuuza boflo mitaani, huu ni mtihani tu. Mimi nakwambieni Mhe. Spika, kwa nia safi kabisa kwa mtindo huu kila mtu atatoka hana kitu *muflis*. Hatuwezi kuwadhulumu watu halafu tukacheka tu, lazima haki itolewe. Mimi nasema Waziri wa Katiba na Sheria ikiwa tatizo ni uchaguzi basi futeni uchaguzi, kaeni huko weee mimi nitawambia watu wa Kiwani Mhe. Abubakar Khamis, Waziri wa Sheria maisha, Dokta Mwinyihaji Waziri wa Nchi maisha, sisi tuko radhi, lakini mtupatie haki yetu tuende tunapotaka.

Mhe. Spika, mimi nasema kama kweli Mhe. Waziri una nia safi mimi nitakupa orodha huu na utwambie ni lini utawapeleka Mahakamani hawa watu ambao wamefoji vyeti. Mimi najua kuna watu Kengeja Mhe. Nassor anamjua yeye ni mtu wa Kengeja, mtu alikuwa Msumbiji yeye ni Mzanzibari halisi lakini limekuwa ni gangwe kwa kuwapokea watu wa Msumbiji kuja Kengeja kwa mashirikiano na Sheha. Serikali inajua je, imechukua hatua gani.
Mhe. Spika, nasema tena kama tatizo ni uchaguzi mimi kwa niaba ya watu wa Kiwani nipo radhi uchaguzi ufutwe, watu watawale mpaka watosheke lakini Wazanzibari wapate haki yao. Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi watu wanaangalia kwamba mimi nikiondoka hapa nitakwenda wapi. Lakini wewe madhali hufanyi haki wewe utauza mkate tu kwa masusu. Baada ya hapo Mhe. Spika, siungi mkono hoja hii mpaka nipate maelezo ya kutosha.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kusimama hapa jioni ya leo nikiwa mzima na afya njema. Lakini pia nichukue nafasi hii ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji wa Mswada huu.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii adhimu nimpongeze sana Mhe. Rais kwa uteuzi wake uliofanyika jana wa nafasi mbali mbali za utendaji wakiwemo Manaibu Waziri. Nawaombea Mwenyezi Mungu wale waliochagulia jana wawe na afya njema na uzima kuweza kuzitumikia nafasi hizo vyema na kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli marekebisho haya yamekuja katika wakati muafaka. Nasema hivyo kwa sababu kipindi kilichopita tulikuwa tunalalamika sana sisi Wawakilishi tuliokuwemo humu ndani na Wazanzibari kwa ujumla jinsi ya vitendo vya uhalifu na ujambazi vilivyotawala nchini kwetu. Lakini pia niipongeze sana serikali kwa kusikia kilio chetu sisi Wazanzibari na kuona kuna umuhimu mkubwa wa kuleta marekebisho haya ambayo yatakuwa yanamlenga Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mchango mwingi. Kwanza niseme kabla sijaendelea na mchango wangu naunga mkono asilimia mia moja kwa marekebisho haya na naomba wananchi tukubali na sisi tuliokuwepo hapa tuunge mkono ili tuweze kupitisha marekebisho haya. Mhe. Spika, pia kutokana na uingiaji wageni kiholela hapa Zanzibar kuna baadhi ya watu wanaingia Zanzibar bila ya vitambulisho wakati mwengine hupata matatizo ya ajali au kifo na inakuwa ni vigumu sana kupatikana *record* zao. Lakini naamini kwamba sheria hii itaweza kusaidia sana kuondosha matatizo haya.

Mhe. Spika, sheria hii pia itaweza kuondosha malalamiko makubwa ambayo yalikuwa yanatolewa wakati wa uchaguzi. Kuna watu ambao walikuwa sio Wazanzibari wanashiriki kinyume na sheria na utaratibu katika kupiga kura na hatimaye wanafanya mambo yao bila ya sheria. Naamini kwamba sheria hii itasaidia sana kutoa haki na naamini kwamba aliyekuwemo atakuwa hatoki na asiyekuwemo atakuwa haingii.
Mhe. Spika, niseme kama nilivyosema awali kuwa sitokuwa na mchango mkubwa lakini nimesimama hapa kwa sababu nina haki ya msingi nimechaguliwa ili kuweza kusema na sheria hii inatuhusu sisi Wazanzibari, nina wajibu mkubwa na mimi kuchangia Mswada huu. Kwa kumalizia niseme kama nilivyosema awali naiunga mkono sheria hii mia juu ya mia, tuifanyie marekebisho lakini tuipitishe ili iweze kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria tulivyoipanga.

Lakini pia Mhe. Spika, niipongeze sana Idara hii ya vitambulisho, ni lazima tuwe wakweli wenzetu hawa wa Idara ya Vitambulisho wanafanya kazi ngumu, lakini pia wanafanya kazi katika mazingira magumu mno. Sote ni mashahidi pale tunapokuwa na matatizo yetu, Waheshimiwa Wajumbe, Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo mbali mbali, tunakwenda pale katika Idara ya Vitambulisho na tunatoa malalamiko yetu na kwa kweli wenzetu hawa ni wasikivu mno. Tunapokwenda pale kwa kweli wanatusikiliza na hawachukui muda mrefu wanatekeleza.

Sasa hivi kuna wananchi wengi Wazanzibari wamepata vitambulisho. Mhe. Spika, miye niliombe Baraza lako hili tukufu tunapochangia tusiwe na jazba, wala tusitumie siasa zaidi. Tuko hapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar. Baada hapo naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kuweza kusimama hapa na kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya mwaka 2005 na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii pia na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa uteuzi wake aliouteuwa jana kwa baadhi ya watendaji na viongozi mbali mbali na niwaombee kila la kheri katika kazi zao mpya, Mwenyezi Mungu awajaalie na atawawezesha ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vitambulisho vya Mzanzibari kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na baadaye kutuletea Mswada huu hapa. Pia niwapongeze Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Serikali kwa kurekebisha Mswada huu na kutuletea hapa kwa mfumo walioutumia wa kuwashirikisha wadau mbali mbali vikiwemo vyama vya siasa, ili kuweza kuleta usawa na kuweza kuupitisha vizuri Mswada huu ili kupunguza malalamiko ambayo yapo na yanaendelea kutolewa kila siku.

Mhe. Spika, kwa kuendelea nipongeze kwa dhati wazo la Mhe. Waziri kwa kuleta kwa Mswada huu kwa marekebisho na kuleta vitambulisho vya Wazanzibari ambao sio wakaazi wanaokuja kwa shughuli mbali mbali, zikiwemo labda za biashara, wanafunzi na wengineo. Nadhani suala hili sio geni kwetu, serikali ilipoanzisha utaratibu wa vitambulisho kuna baadhi ya wenzetu walilichukulia kisiasa suala hili na kuhamasishana kwamba havina maana. Baada ya kuona kheria zake sasa hivi imekuwa kero na lawama kubwa zinatolewa kuhusu vitambulisho hivi.

Mhe. Spika, serikali ilipoweka sheria hii pia iliweka na utaratibu wa jinsi gani na njia mbali mbali za kupita mpaka mtu aweze kukipata kitambulisho kile. Sheria hizo ni rahisi sana na hakuna sababu ya kwamba leo hii kuna lawama mbali mbali ambazo zinatolewa kuhusu vitambulisho hivi.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kuchangia isipokuwa nawaomba viongozi wenzangu tuzidi kuwaelimisha wananchi wetu kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Nadhani katika kipindi cha Bajeti kilichopita Mhe. Waziri alilitolea ufafanuzi mzuri suala hili la vitambulisho na akasema kwamba kuna vitambulisho vingi sana katika Afisi yake ambavyo bado havijachukuliwa na ameleta takwimu ya kila wilaya na akatuletea idadi kamili ya vitambulisho mbali mbali ambavyo vimo bado katika Mawilaya havijachukuliwa. Lakini leo bado Waheshimiwa viongozi tunalalamika kuhusu vitambulisho.

Nawaomba Waheshimiwa viongozi tuwahamasishe watu wetu, watumie taratibu zilizokuwepo, wajiandikishe halafu vikishakuwa tayari waende wakavichukue. Isiwe wanavilalamikia halafu vinabaki kurundikana katika Mawilaya na hadi leo vitambulisho hivyo vipo havijachukuliwa.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa watendaji wa Idara ya Vitambulisho wanafanya kazi zao nzuri, wanafanya kazi kwa uadilifu, tunakwenda wanatusaidia, pale panakuwa na matatizo na malalamiko wanatutatulia matatizo yetu, hatimaye vitambulisho hivyo vinapatikana bila ya matatizo yoyote. Mhe. Spika, naomba tuzidi kuwaelimisha watu wetu, pia viongozi wenzetu tuende kwa wenzetu na tufate taratibu za kwenda kuwasaidia wanachama wetu. Mwisho kabisa Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusinu Unguja na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza machache katika kuchangia Mswada huu muhimu, Mswada wa Wazanzibari, ambao kwa siku ya leo tunafikia pengine *In Sha Alla* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafikia tamati.

Mhe. Spika, mimi nianze kama wale wenzangu walivyokuwa wametangulia kuanza kushukuru na kupongeza juu ya uteuzi ambao Mhe. Rais ameufanya jana, tunawaombea wale ambao walibahatika kupata nafasi za kuongoza kila la kheria na waendeleze gurudumu la maendeleo katika visiwa vyetu vya Zanzibar na Pemba.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nije kwenye yale ambayo mengi yamekuwa yakizungumzwa na wenzetu ambao wametangulia kuanza kusema hapa juu ya namna ambayo tuna wa-*criticize* hawa watendaji wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika, kila binaadamu katika dunia ana mapungufu yake, sisi kama viongozi na sifa ya viongozi ni kuonesha njia kwa wale ambao tunawaongoza. Sasa inapotokea kama watendaji tunahisi wanafanya vile ambavyo sivyo sio muelekeo unaotakikana, sisi kama viongozi tuliokuwa tumechaguliwa kwa maslahi ya maendeleo ya nchi hii, tuchukue fursa hiyo basi kuwaelekeza, kuwafahamisha, kuwafanya ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Si vizuri kila watendaji wanalolifanya kuwa tunawa-*criticize* kila mara tutakuwa tunawandoshea ile ari ya kuweza kutenda kazi zao vizuri na kuweza kujiona kwamba wanachokifanya baadhi ya mambo ni sahihi na ndio ambayo yanahitajika kufanywa na watendaji kama wao, isipokuwa sisi tuwasaidie zaidi.

Halafu vile vile wenzetu waliokuwa wametangulia hapa nilikuwa nikisikiliza mjadala vizuri sana, wako ambao walikuwa wanazungumzia suala la uhamasishaji kama imekuwa pahala pa malumbano vile. Ningelipenda kuchukua fursa hii kusema kwamba sisi ni Wawakilishi ambao tumechaguliwa na wananchi, tumekuja hapa kwa nia moja tu ya kuwatendea haki wananchi wetu na kuweza kufanya yale ambayo kama viongozi tunatakiwa tuyafanye. Muhimu ambalo tulipaswa sisi kulifanya ni kuwasaidia wananchi wetu kuwaelekeza na kuwafahamisha kwamba sheria ndio msingi wa maendeleo ya mambo yote. Bila ya kufuata sheria mambo yetu yatakwenda korogo vyogo, tujitahidi kuwaelekeza wananchi wetu waweze taratibu, waweze kufuata sheria na mambo yaweze kwenda vizuri. Isiwe sisi kama viongozi ndio tunaosababisha kuzivunja sheria hizo na kuwaelekeza wananchi wafanye mambo ambayo hayana muelekeo.

Jengine Mhe. Spika, ambalo kwa leo nataka kulizungumzia hapa leo kuna kitu kimejitokeza Mhe. Spika, na jambo moja kubwa ambalo limejitokeza siku ya leo ni yale mapungufu ambapo yapo katika Wizara ya Elimu juu ya namna ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu na watoto wetu katika kuwasomesha somo la historia. Somo la historia hapa ndio kichocheo ambacho kilikuwa ni tatizo kwa wazanzibari hata tukaweza kufikia pahala ambapo sasa tupo. Kwa kutumia kikao hiki ningeomba basi Wizara ya Elimu iweze kufikiria namna gani kuweza kurudisha somo la historia katika maskuli yetu ili watoto wetu waweze kufahamu hasa nini historia ya Zanzibar na watu wake na asili yake ilivyo kwa wazanzibari wote. Ningeliomba serikali hususan Waziri husika alichukue hili na tulifanyie kazi.

Asubuhi hapa katika michango mbali mbali Mhe. Spika, kuna baadhi ya Wajumbe tulikuwa tukichangia kwa jazba vile vile kuelezea masuala mazima ya uzanzibari ukaazi pamoja na wageni ambao walikuwa wanapewa vitambulisho katika utaratibu ambao sio na ule uraia. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi nilipokuja hapa leo jioni hii nimekuja na kadi yangu ya uzanzibari, kadi ya uraia niweze kusema hii hapa. Kadi hii Mhe. Spika, ni katika urathi ambao nilipewa kutoka kwa marehemu baba yangu, ndani yake humu mna karatasi mbili, mna hii kadi ya kijani ya uraia lakini vile vile mna stakabadhi ambayo imeandikwa Idara ya Uandikishaji Uraia na Wakaazi.

Kwa hivyo suala la ukaazi si suala jipya, tupo ambao tulichangia hapa tukasema kwamba suala la ukaazi hapa kwetu ni suala ambalo si sahihi tu sio na viatambulisho vya uzanzibari mkaazi, bali tuwe na vitambulisho vya uzanzibari tu. Hata hizi kadi za uraia ambazo kuwa tumezipata Mhe. Spika, zimeandikwa kwamba zimetolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimetoka mwaka 1966/1967 hizi. Vile vile chini kabisa imeandikwa hapa kwamba hii imetokea Zanzibar na Wazanzibari ndio wanapaswa kupata hii.

Vile vile Mhe. Spika, nilipokuwa nakuja hapa kutaka kuja kuchangia katika hoja hizi nilikwenda juu kuangalia *hansard*, nilipofika chumba cha *hansard* kule nilivuta *hansard* ya tarehe 11/4/2005, *hansard* hii ilitolewa maelekezo na Mhe. Ali Mzee Ali kwa kipindi hicho cha mwaka 2005. Humu mna hadithi yote katika haya mambo ambayo tunajadiliana hapa hakuna jipya wala hakuna sababu ya kuvutana katika suala hili, humu yameelezwa yote kwa ufanisi na kwa ufasaha kabisa, ningeliwaomba Wajumbe wenzangu tuende katika chumba cha *hansard* tukaangalie

hii *hansard* ambayo imetolewa na Mheshimiwa mwenzetu, kwa bahati nzuri alikuwa Mwakilishi kipindi kile, na leo sasa hivi tunae hapa tunamwita *professor* yumo humu ndani. Ningeliwaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hebu twendeni kwa mujibu wa *records*, tusende tu tukafanya mambo tukafika pahala kama Mhe. Spika, anavyosema tumeshachafua mawazo ya watu nje huko, kwa kitu ambacho tulikubaliana kwa ridhaa zetu, kwa umoja wetu, na kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Ndugu zangu katika *hansard* hii kuna vipengele viwili vitatu Mhe. Spika, ningeliomba kuvinukuu. Kwanza kabisa ninakuja katikati hapa ambapo Mhe. Ali Mzee alisema, sasa Mhe. Spika, nani mzanzibari, mzanzibari ametungiwa sheria namba 5 yeye wakati ule amesema namba 5 lakini nilipoangalia hii niliona kwamba ni namba 7. Sasa kama kuna matatizo ya kibinaadamu hapa au ya *typing error* yamejitokeza naomba radhi kwa hilo. Mwaka 1985 sheria ambayo inasema *'the act to define Zanzibaris and provide for other matters connect* sheria hii imetiwa saini na Rais wa awamu ya tatu Mhe. Ali Hassan Mwinyi na karani wa Baraza la Wawakilishi kwa wakati huo alikuwa bwana Iddi Pandu Hassan.

Lakini vile vile kulikuweko na Kamati ambayo alikuwepo Mhe. Abubakar Khamis Bakary ndie aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi kwa wakati huo, jamani kila kitu kimo humu. Tukienda *through* katika hizi *document* tutaweza kupata kila kitu. Sasa hapa asubuhi leo tulikuwa tunazungumzia wazanzibari wanapewa watu wanyamwezi, wamakonde na watu wengine. Mimi ningelipenda kuzungumzia historia.

Katika nchi ya Zanzibar Mhe. Spika, mwaka 1820 watu ambao walikuwepo hapa, siendi mbali sana walikuwa ni wazaramo ndio waliokuwa na asili ya hapa na uthibitisho wa maneno yangu ninayazungumza watu waende *archives* watapata. Lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Spika, kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuna eneo pale pana makaburi yamezunguka yale ni makaburi ya wazaramo, wale ndio wenye asili ya Zanzibar kwa wale ambao walikuwa hawajui.

Lakini kama hiyo haitoshi tukiondoka hapo tutakwenda zetu kwa Mamwinyi Wakuu waliokuwa wameanza kuja hapa, wale mwinyi wakuu tukienda tukitafuta historia zao ni wamanyema na wao wametokea Bara vile vile ndio ambao wamekuja hapa wakaweza kutengeneza hiyo historia ikaweza kupatikana historia ya Zanzibar. Sasa leo unaposema kwamba kuna watu wa namna fulani au wa kabila fulani ndio ambao wana haki na wajibu wa kuitwa wao ndio wazanzibari. Jamani huyu Mfalme Said bu Said aliyekuja mwaka 1931 alifika katika visiwa vya Zanzibar akitoka hapa alikuwa akielekea Pemba, alikua hashuki kwenye meli yule. Anakaa kwenye meli anatizama watu wa Pemba kule kwa darubini ndio utaratibu ambao ulikuwa ukitumika.

Sasa hili suala la ubora na sio bora sio hasa ambalo limetuleta hapa. Jambo la msingi tuzungumzie historia kwa mujibu ilivyo, tuzungumze maendeleo yetu kwa mujibu wa taratibu zinavyotaka, tusifanye vitu ambavyo havina muelekeo hususan tukaweza kuwapotosha watu ambao tunawaongoza katika maeneo yetu.

Halafu vile vile katika uchangiaji hapa tulifika pahala tukawa tunazungumzia suala la *document* za *forgery* na watu wanavyokuwa watendaji hawa wana-*forge* vitu jamani kwa nani asiyeelewa kwamba *forgery* tunafanya wenyewe. Soko kubwa la kuweza kufanya hivi siwezi kumtaja ni akina nani, lakini mambo haya yote yanafanyika makao makuu Darajani, pale ndio chaka pa kufanyika mambo mengi sana hata hao ndugu zetu ambao wameweza kuondoka wakaenda zao Uingereza wapi wapi wengi wameondoka katika majina si yao, majina ya kutengeneza watengenezaji ni nani, tutaenda kutafiti huko tutakwenda kuyajua kila mmoja kwa namna yake.

Lakini hapo hapo tumefika pahala mpaka na viongozi wetu wakaja wakashtakiwa kutokana na *forgery* za kuweza kuwaondosha watu kinyume cha taratibu. Sasa tunapofika hapa tukaja tukaanza kuvuana nguo kwamba huyu amefanya *forgery* aa, mimi nahisi si katika mambo mazuri. Tuendeni katika taratibu za kisheria, tulitumie Baraza la Wawakilishi kama Baraza la kutunga sheria, tuendesheni shughuli zetu kwa mujibu wa taratibu ili wale tunaowaongoza wajue tunakuja humu kuzungumzia vitu kwa hoja za msingi ambazo tunazitengeneza na kuweza kuzitetea pamoja na kuwafahamisha watu wetu ili waweze kutuelewa, kutufahamu na kuweza kushirikiana kwa pamoja kuendeleza Zanzibar yetu. Zanzibar bila ya kuhangaishana na kutupiana majungu inawezekana. Ningeliwaomba wazanzibari wote tuende kwa pamoja tuongoze nchi yetu kwa umoja na tuweze kuishi kwa salama na amani.

Na kitu chengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka kukizungumzia ambacho nili-*quote* katika ile *hansard* ambayo nimeichukua juu, kuna eneo hapa Mhe. Ali alikuwa analizungumza naomba nilisome kwa niaba anasema, kule

Dubai wapo wazanzibari huwi mzanzibari mpaka uwe mtanzania. Kwa taarifa ya Baraza hili wapo wazanzibari wanaishi Dubai na ni watanzania wana paspoti ya Tanzania wapo wanoishi Canada, Oman, lakini wao bado sheria hii ya ukaazi wanayo na wanaitumia. Lakini kule Dubai wanapata ikama, yaani wanakaa pale wanapata baadhi ya haki ijapokuwa ni mtanzania, lakini anapata haki ya pale sio haki kubwa za kupiga kura nyengine, isipokuwa ni kupata haki ndogo ndogo za kuweza kupata kazi na mambo mengine.

Kwa hivyo utaratibu ambao unatakiwa kutumika hapa sasa hivi kutoa vitambulisho katika *category* tofauti ni katika kuyakubali haya ambayo watu walikuwa wamekubaliana tokea mwaka 2005 si jengine Mhe. Spika. Kwa hivyo ningeliwaomba sana wenzangu waende wakasome hizi *hansard* ili waweze kuzifahamu, ili waweze kujua wenzetu wanafanya nini, na sisi tuweze kutambua wajibu wetu ni nini tunapokuwa tunakaa katika maeneo haya.

Na mwisho kabisa nimalizie kwa taarifa ambayo ipo hapa, anasema hapa Zanzibar kuna watu kwa mfano kuna waingereza, kuna wachina, wanaishi hapa Zanzibar wanapata *resident permit* yaani *permit* ya kukaa sasa hii *resident* ni lugha ambayo ni *international.* Sasa kitu hiki kipo duniani kinafanyika, na sisi tunawapa hii wakaazi wetu Mwenyezi Mungu atakapotujaalia na pesa nyingi tutawapa watu ambao sio raia, lakini hapa suala la uzanzibari ataendelea kupewa mzanzibari mkaazi tu.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, mimi binafsi, na kwa niaba ya wananchi ninaowatumikia wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsanteni sana.

**Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum):** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mswada huu wa kuwasajili wazanzibari wasiokuwa wakaazi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima, lakini pia nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa mswada huu.

Mhe. Spika, nimefuatilia mazungumzo au michango ya Waheshimiwa wengi, sasa wengi wetu tumetoka nje ya mswada lakini nahisi pia ni uchangiaji wenye maana kwa sababu pia unatuonesha pale ambapo kasoro zipo.

Mheshimiwa mimi nianze kwa kusema kwamba kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia. Lakini pia naomba niwakumbushe wenzangu kwamba kwenye Baraza hili sio chimbuko la kuzozana isipokuwa kujenga hoja. Na ukiangalia Katiba yetu ya Zanzibar inazungumza mzanzibari ni nani, lakini Katiba inasema kwamba masharti ya mzanzibari itakuwepo katika sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Sasa sheria ipo ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi inayozungumza mzanzibari ni nani, na nafikiri katika miaka ya 2000 pengine 2003 ama 2004 tulifanyia marekebisho masharti ya kuwa mzanzibari. Kwanza ilikuwa kwa miaka kumi kwa mtanzania ambaye anaishi Zanzibar anaweza kuwa mzanzibari, lakini nakumbuka tuliishusha mpaka miaka 7 kama sikukosea.

Sasa ile hoja ya kusema kwamba huyu Mmasai, huyu Mhindi, huyu Mndengereko haina msingi kama mtanzania kwa sababu sharti hilo ukiwa mtanzania ambaye umeishi Zanzibar zaidi ya miaka 7 unaweza kuwa mzanzibari. Na mzanzibari yoyote mwenye sifa za uzanzibari anakuwa ni mtanzania. Kwa hivyo haya malumbano yanakuwa hayasaidii sana isipokuwa yanatoa mgawanyiko. Mimi niseme kwamba sheria hii ya mzanzibari ile mama yenyewe ni muhimu sana kwa maendeleo ya Zanzibar.

Na ningeliwaomba wenzangu waelewe kwamba sheria ile ni ya mzanzibari mkaazi, si mzanzibari tofauti pengine hata na hii vitambulisho vitakavyokuja vya mtanzania. Vile vitambulisho vya mtanzania sehemu yoyote unayoishi maadam ni mtanzania utapata kitambulisho. Lakini hii ya mzanzibari mkaazi sharti lake kubwa kwamba uwe umeishi katika eneo ndio upate kitambulisho chako cha mzanzibari. Na mimi nina hakika kwamba kwa mzanzibari aliyekuwepo Zanzibar kila mmoja anayo sehemu ya kwenda kujiandikisha na kupata cheti cha kuzaliwa lakini pia na kupata kitambulisho cha mzanzibari mkaazi.

Kwa sababu bahati nzuri Zanzibar sio kama nchi nyengine, kuna baadhi ya nchi kuna wananchi wanoitwa wa kutanga tanga, leo wanaishi hapa kesho pale na zaidi wafugaji, kwetu sisi hatuna utaratibu huo. Tunao watu wanaishi, na sheria zipo mimi sasa hivi sehemu moja ninaishi Chukwani, Chukwani kuna shehia lakini sijaenda

kujiandikisha kwa Sheha kwa sababu sitaki kupoteza haki zangu za shehia yangu ya Muembemakumbi. Kwa hivyo bado ni mkaazi wa Muembemakumbi na haki zangu ziko Muembemakumbi. Kwa hivyo nilikuwa nawasihi Waheshimiwa wenzangu kwamba tujitahidi sana kufuata sheria, tusilalamike, tufuate taratibu nina hakika kila mmoja atafanikiwa kupata suala lake.

Lakini nije katika lengo la mswada huu wa leo, Mhe. Spika, mswada huu lengo lake ni kuwatambua wazanzibari zaidi wageni. Hapa Zanzibar tunao watu wamekuja kwa njia mbali mbali hata hao watanzania wengine ambao wanaishi Zanzibar bado hawajawa na sifa na kuwa mzanzibari mkaazi. Lakini pia wageni wanaotoka nje ya nchi hii wanakuja hapa kufanya shughuli zao za kikazi na biashara, hivi hawa tuwaache bila kuwapa kitu chochote cha kuwatambua? Ndio maana serikali ikaamua sasa tuwape vitambulisho ambavyo vitakuwa tofauti na hivi vitambulisho vya mzanzibari mkaazi, ili kila mmoja muweze kumtambua na yeye yule mtu apate haki zake.

Leo hii tulipata ajali hapa za kuzama meli lakini serikali ilisumbuka sana kuwatafuta uasilia wa wale wageni, ilibidi ichukuliwe juhudi kubwa sana mpaka kuwatambua. Lakini laiti kama na hii sheria inasema ndani ya siku 60 baada ya mgeni kufika nchini ama yeye mwenyewe ama mwajiri wake aripoti ili yule mtu aweze kupata kitambulisho cha mzanzibari mgeni sio mkaazi. Na hili litaondoa lile tatizo ambalo wenyewe tunalizungumza kwamba kwa sababu mtu hana njia nyengine na yeye anaishi Zanzibar na anajua kwamba Zanzibar kuna vitambulisho vya mzanzibari mkaazi, hata akikaa mwezi mmoja anaweza akafanya mipango akapata kile kitambulisho. Kwa sababu kizuri, kina manufaa lakini sasa itakuwa haina haja ya kuvamia katika maeneo ya mzanzibari mkaazi. Atafika yeye atakwenda kwenye uongozi atasajiliwa na kupewa kitambulisho chake cha mzanzibari mgeni.
Kwa hivyo Mhe. Spika, nahisi mimi kwamba tusichanganye mambo, hapa yamezungumzwa mambo mengi Mhe. Spika, mimi nashangaa mpaka mambo ya uchaguzi wa Bububu yanaletwa katika sheria hii. Lakini ukiangalia hata Bububu tulifanya makosa sisi, pale tulikuwa tunatawaliwa na sheria ya Tume ya Uchaguzi. Mimi nilienda Bububu, lakini sikwenda kama Waziri nilienda kama Mwakilishi wa chama na nilipewa kitambulisho na Tume ya Uchaguzi kwamba hichi ukienda uende nacho ndio upate ruhusa ya kufanya kazi. Lakini wenzetu wengine walikwenda bila ya vitambulisho na wakafanya kazi za Tume ambao si sheria, kwa hivyo hayo ni makosa.

Sasa kama yale yametupitikia bila kujua tuone kwamba tulifanya makosa, na binaadamu akifanya kosa anakiri kama mimi nilikosea niliteleza. Kwa sababu kwa sheria Tume ina sheria zake, ina taratibu zake. Mhe. Haji nilikuwa naye katika kampeni zetu zile, lakini Mhe. Haji nilimwambia wewe huna kitambulisho cha kuingia Bububu kaa pembeni tusubiri katika Ofisi ya CCM ya Mkoa, tukamfungia ndani yeye ni Waziri lakini hakuweza kwenda na mawaziri wengine walikuwepo hawakufika pale, kwa sababu hawakuwa na vitambulisho vya Tume. Mimi nilipata kwa sababu ni mkuu wa Idara kwenye CCM, kwa hivyo nilipata kitambulisho changu na nikaenda na kuangalia taratibu naingia natoka naenda zangu wala sikumhoji mtu kwa nini wewe ulikuja kupiga kura, hebu nioneshe kitambulisho chako cha kupigia kura si kazi yangu, kwa hivyo sikufanya. Lakini vyumba vyote niliingia ndani na nikahakikisha kwamba zoezi linaendelea vyema nikaendelea na shughuli zangu.

Kwa hivyo Waheshimiwa mimi nafikiri tungelizungumzia sana umuhimu wa huu mswada wenyewe wa leo. Na kitambulisho hiki sisi wazanzibari wakaazi tutakuwa na kitambulisho chetu kile kile hakibadilishwi kwa hiki, kwa hivyo ninafikiri tusichanganye lakini sisi tutapata chengine cha mtanzania. Huyu atakayekuja kupata kitambulisho kichi tofauti na huyu mtanzania tofauti na hichi cha mzanzibari. Huyu kama mtanzania atakuwa navyo viwili kile cha kule Tanzania na hiki cha ugeni wake hapa. Lakini kwa watanzania kuna faida nyengine akifika muda wake wa kuwa na masharti ya kisheria ya kuwa awe mzanzibari mkaazi basi ni rahisi ya kum-*transfer* kutoka eneo moja kwenda eneo jengine. Lakini kwa wageni wa nje ya nchi hawawezi kubadilika watakuwa nacho kile kile tu, kwa hivyo Mhe. Spika, nafikiri hili lisituvuruge mimi naomba Baraza hili tuende tuzungumze vizuri. Mimi nahisi mambo yetu yanakwenda vizuri lakini tukizungumza kwa hamasa humu Barazani tutajivuruga wenyewe.

Mimi nawaomba Waheshimiwa wenzangu tusirudi tulikotoka, tujitahidi sana kujenga mshikamano na kujenga amani na tuiamini serikali yetu kwa sababu haya mambo yamefanywa kwa pamoja, na nina hakika huu mswada tumeujadili sote serikali nzima kwa pamoja, kasoro zimeonekana na kasoro zimeondolewa. Kwa hivyo Waheshimiwa wenzetu wa Baraza ninafikiri tuchangie tutoe mawazo yetu lakini mswada huu ni mzuri, suala hili ni jema na mfupi sana huu mswada lakini una mambo mazuri sana kwa kujenga mustakbali wa Zanzibar. Wale ambao wanalalamikia ile sheria mama, sheria wanasema watu, sheria ikiwa haifanyiwi mabadiliko ina maana hiyo sheria huwa hawajali kuitekeleza.

Lakini sheria inapotekelezwa na mabadiliko lazima yawepo. Kwa hivyo wale watu wanaozungumza kwamba mbona sheria inarekebishwa, sheria yoyote nzuri lazima irekebishwe kwa sababu inapotumika ndio inapoonekana makosa yake yanayofanyika.

Sasa mimi Mheshimiwa naomba nimalizie kwa kusema kwamba wakati umefika wa kuunga mkono sheria hii lakini pia niwaombe watendaji wa Mhe. Waziri kwamba wajitahidi sana kwamba sheria hii ikipitishwa tu shughuli hii ianze mara moja, ili na wageni wetu nao wajisikie na wapate faraja ya kupata vitambulisho ambavyo sio sawa na hivi vya mzanzibari mkaazi. Kulikuwa na tatizo hilo la kusema kwamba kunanyimwa watu lakini kama nilivyosema mwanzo mimi nina hakika kama kila mmoja atakwenda kuchukua pale ambapo anastahiki kuchukua, na bado utakuwa unabakia na uzanzibari wako ukaazi mimi nina hakika kila mmoja atapata faida hiyo, na tutaondoa zile tuhuma kwamba wageni na wasiostahiki wanapata vitambulisho hivyo.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kuchangia hayo lakini narejea tena kwamba naunga mkono sheria hii au mswada huu na tujitahidi kwa pamoja sote tuunge mkono ili sheria hii iweze kufanya kazi. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wwajumbe nafikiri tumefikia pahala tumezungumza kiasi cha kutosha mswada ni mfupi sana kati ya miswada ambayo imekuja Barazani huu ni mfupi mno, lakini maneno yake ni mengi. Sasa kwa kuwa kuna mambo mengi yamezungumzwa inafaa basi Waziri nae apate nafasi akatizame hayo maelezo aje atoe hapa tuimalize kazi hii wakati kila mmoja amefika pahala ameridhika. Na kwa sababu hiyo nimenong'ona mapema na Mhe. Waziri kwamba majumuisho yafanyike kesho ili apate muda wa kujiweka vizuri wa kutoa maelezo muafaka kwa yale maelezo yaliyoulizwa, na mengine mengi yametajwa katika mswada huu.

Kwa sababu hizo basi sasa tusitishe shughuli zetu hizi na kuakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 17/10/2012 saa 3.00 barabara za asubuhi.

*(Saa 12.51 jioni Baraza liliakhirishwa hadi*
*tarehe 17/10/2012 saa 3.00 asubuhi)*